ATHARI ZA EKEGUSII KATIKA KISWAHILI NA ZINAVYOCHANGIA MATOKEO MABAYA YA MTIHANI WA KITAIFA WA KISWAHILI KWA WANAFUNZI WAKISII WILAYANI KISII KUSINI

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

DAUDI O. MANGWA

A33 / O244 / 99

Tasnifu inayowasilishwa katika Graduate School ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili (Kiswahili) katika Idara ya Lugha na Isimu, Kitivo cha Sanaa na Sayansi, Ndaki ya Egerton.

NDAKI YA EGERTON

2005

EULIB
027 109

2007/12690

UNGAMO

Kazi hii ya utafiti ni yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Ndaki yoyote ile.

Daudi O. Mangwa Sahihi _____ Tarehe 04/04/05

Kazi hii imewasilishwa katika Ndaki ya Egerton kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Kiswahili kwa idhini yetu kama wasimamizi.

Dkt. S.K. Beja Sahihi _____ Tarehe 18/4/05

Dkt. J. N. Kimemia Sahihi _____ Tarehe 18/4/2005.

2007/72.692

SHUKURANI

Kwanza namshuru Muumba wangu kwa kunipa afya njema, maarifa na kunikinga dhidi ya hatari za aina nyingi za dunia . Nawashukuru kwa dhati wote walionisaidia na kunipa moyo wa kujiunga na kumaliza masomo haya miongoni mwao ni Prof. Rocha M. Chimera, Dkt Mosonok Arap Korir, Prof. D. Nassiuma na Dkt I.Y Mwamzandi.

Shukrani za dhati ni kwa wahadhiri, wasimamizi na washauri wangu miongoni mwao ni Dkt C. Kitetu, Dkt. S.K. Beja, Dkt. J. N. Kimemia, Marehemu Dkt A. Mwaro - Were, Dkt Aswani Buliba na Mw. D. Chacha.

Nawashukuru wafanya kazi wenzangu walionisaidia wakati wa masomo yangu miongoni mwao ni Dkt Wataka Wakube, Jared M. Omao, Ronald O. Omenge na Japhet O. Onserio.

Shukrani kwa waliokuwa wanafunzi wenzangu mabwana Mohamed Y. Mwamzandi na Robert Olodo kwa kunitia motisha na kunishauri. Wafanyakazi wa maktaba za vyuo vikuu vya Egerton na Kenyatta kwa kunihudumia kila nilipohitaji msaada wao. Pia ninawashukuru wote ambao walinipa moyo kwa njia moja au nyingine wakiwamo Mw. Isaac Arwasa Osero, Mw. Nathan Anyona, na Dkt Mwenda Mukuthuri,

Shukrani nyingi sana kwa mke wangu Prisca Moraa, wanangu Daniel Onsase, Lilian Nyabonyi (Lila), Juma Nunni, Idd Matano, Zeituni Mosiara na Zainabu Tatu kwa kuvumilia usumbufu wangu nilipoondoka mapema na kurudi nimechelewa.

Shukrani za dhati kwa walimu wa Kiswahili na wanafunzi wa shule zote zilizohusishwa kwenye ukusanyaji wa data yangu kwa ushirikiano na usaidizi wao.

Ni wengi walionisaidia kwa njia moja ama nyingine lakini si rahisi kuwataja wote. Kwa jumla nasema, ahsanteni nyote.

TABARUKU

Kwa mke na watoto wangu wapendwa

IKISIRI

Kazi hii imeshughulikia swala la athari za Ekegusii katika Kiswahili kwa wanafunzi Wakisii wa kidato cha nne wilayani Kisii Kusini katika mtihani wa kitaifa wa Kiswahili. Katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita, wilaya ya Kisii Kusini imekuwa ikiorodheshwa miongoni mwa wilaya zenye matokeo mabaya sana ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili kote nchini Kenya. Hakuna utafiti wa kina uliowahi kufanywa kubainisha sababu za kiisimu za matokeo haya duni ndio maana utafiti huu ukafanywa. Utafiti huu ulishughulikia makosa ya kisarufi, kifonefiki na kifonolijia yaliyotokana na athari za Ekegusii katika Kiswahili. Data ilikusanywa kutokana na mazungumzo ya wanafunzi kwenye mijadala waliyoandaliwa na kutokana na makaratasi ya majibu ya mtihani wa mwigo wa wilayani wa Kiswahili. Shule kumi na tano kati ya arobaini na tisa ziliteuliwa kwa mtindo wa bahati na sibu na wanafunzi kumi kutoka kila shule (isipokuwa moja ambayo ilikuwa na wanafunzi sita) walihusishwa. Wanafunzi hao kumi waliteuliwa kwa mtindo wa bahati na sibu katika mijadala na hao ndio makaratasi yao ya mtihani wa mwigo yalitumiwa katika kubainisha na kuainisha makosa yaliyokusudiwa. Nadharia ya uchanganuzi Linganishi ilitumika katika kulinganisha na kutofautisha vipengele mbalimbali vya lugha za Ekegusii na Kiswahili. Nadharia ya Uchanganuzi makosa ilitumiwa katika kubainisha na kuainisha makosa ya kisarufi, kimsamiati na kihijai yaliyojitokeza. Nadharia ya Sifa Bainifu za Sauti ilitumika katika kuchanganua utata wa kisauti waliokuwa nao wanafunzi Wakisii katika mazungumzo na uandishi. Data ilichanganuliwa kwa kutumia uchanganuzi thamano na wingi dadi. Hatimaye ilibainika kwamba athari za Ekegusii katika Kiswahili zilichangia matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili kwa wanafunzi Wakisii.

ABSTRACT

This study deals with the phenomenon of the influence of Ekegusii on Kiswahili in respect to form four Kisii students in Kisii South District in their Kiswahili National Examinations. In the past one decade the district has been rated amongst those with the poorest Kiswahili results in the Kenya Certificate of Secondary Education. There has been no research done to establish linguistics causes of the dismal performance hence need for this study. The study dealt with the grammatical, phonetic and phonological errors which emanated from the influence of Ekegusii on Kiswahili. Data was collected from tape recorded speeches of students who were engaged in debates and from their Kiswahili District Mock Examination. Fifteen out of forty nine secondary schools in the district were randomly selected for data collection. Ten students from each school (except one where six) were tape recorded during the debates. Kiswahili District Mocks Examination papers of the same students were used to identify and classify errors. The comparative Analysis Theory was used to compare and contrast various language structures between Ekegusii and Kiswahili. The Error Analysis Theory was used to identify and classify grammatical, phonetic and phonological errors of the students. Also, the Theory of Distinctive Features of sounds was used to identify and describe sounds as produced by Kisii students during debates and in writing. The data collected was analysed both qualitatively and quantitatively. At the end it was established that Kisii form four students do perform poorly in the Kiswahili National examination because of the interference of Ekegusii on Kiswahili.

MAELEZO YA VIFUPISHO VYA MANENO

(i) N.U.M __ Nadharia ya Uchanganuzi Makosa.
(Errors Analysis Theory)

(ii) N.U.L __ Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi.
(Contrastive Analysis Theory)

(iii) L.A.D __ Language Acquisition Device.
(Cheche ya Upataji na Ujifunzaji Lugha)

(iv) K.N.E.C __ Kenya National Examination Council.
(Baraza la Mitihani ya Kitaifa la Kenya)

(v) K.C.P.E __ Kenya Certificate of Primary Education.
(Hati ya Elimu ya Msingi ya Kenya)

(Vi) K.C.S.E. __ Kenya Certificate of Secondary School Education.
(Hati ya Elimu ya Upili ya Kenya)

MAELEZO YA ISTILAHI

1. Athari za lugha.

   Ni ujuzi wa lugha fulani ambao ni tofauti na lugha nyingine unaoweza kuvuruga au kuvunja mfumo na mpangilio wa lugha hiyo nyingine.

2. Hijai.

   Utaratibu maalum unaokubalika wa kuandika katika lugha fulani. Tahajia

3. Kichocheo.

Jambo au kitu kinachosababisha msukumo au ushawishi wa kutenda jambo fulani ili kuunga au kupinga uamuzi au ugunduzi wa awali.

4. Mikakati.

   Mbinu zinazotumiwa ili kufanikisha jambo au lengo fulani.

5. Natija.

   Manufaa au umuhimu wa jambo, tukio, au kitu fulani.

6. Fonetiki.

   Ni uchanganuzi wa kisayansi wa sauti mbali mbali za lugha. Husaidia katika kuainisha uhusiano uliopo kati ya hijai na lugha zungumzi.

7. Fonolojia.

   Ni taaluma inayohusu muundo wa lugha kisauti. Ni sayansi ya lugha inayochunguza mfumo wa sauti.

8. Mifanyiko ya kifonolojia.

   Mabadiliko yanayotokea katika kuelekea kubadilisha sifa au sauti za lugha.

YALIYOMO

Ungamo..... ii

Shukrani iii

Tabaruku iv

Ikisiri v

Abstract vi

Maelezo ya Istilahi vii

Maelezo ya vifupisho vya maneno viii

SURA YA KWANZA

1. Utangulizi 1

1.1. Usuli wa mada 1

1.2. Mada ya utafiti 6

1.3. Madhumuni ya utafiti..... 6

1.4. Nadharia tete 7

1.5. Upeo wa utafiti 7

1.6. Umuhimu utafiti 8

1.7. Mbinu za utafiti 8

1.7.1. Ukusanyaji wa data 9

1.7.2. Uchanganuzi wa data 11

SURA YA PILI

2.0. Uhakiki wa maandiko na nguzo za kinadharia 13

2.1 Uhakiki wa maandiko 13

2.2 Nguzo za kinadharia 17

2.2.1 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa (NUM) 17

2.2.2 Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi (NUL) 19

2.2.3 Nadharia ya Sifa Bainifu za Sauti 23

SURA YA TATU

3.0 Makosa ya kisarufi..... 24

3.1 Utangulizi 24

3.2. Ngeli za Ekegusii 24

3.2.1 Maelezo 24

3.2.2 Upatanisho wa nomino-kivumishi 33

3.2.2.1 Vivumishi vimilikishi 33

3.2.2.3 Vivumishi vya sifa 36

3.2.2.4 Vivumishi vya {- enye} na {-enyewe} 38

3.2.2.5 Vivumishi vya {-ote} na {-o-ote} 41

3.2.2.6 Vivumishi vya {-a-} unganifu 44

3.2.2.7 Upatanisho wa nomino - tarakimu..... 45

SURA YA NNE

4. 0 Makosa katika mazungumzo 48

4.1 Utangulizi..... 48

4.1.1 Makosa katika upatanisho wa kisarufi kuzingatia ngeli..... 48

4.1.2 Makosa katika kisarufi kwa kuzingatia Vivumishi 49

4.1.2.1 Vivumishi vya sifa 49

4.1.2.2 Vivumishi - vimilikishi 50

4.1.2.3 Vivumishi vya {-enye} na {-enyewe}..... 50

4.1.2.4 Vivumishi vya {-ote} na {-o-ote}..... 51

4.1.2.5 Vivumishi vya {–a-} unganifu..... 51

4.1.2.6 Matumizi ya vivumishi vya idadi..... 52

4.1.2.6.1 Matumizi ya vivumishi vya idadi ya jumla 52

4.1.2.6.2 Matumizi ya vivumishi vya idadi kamili 53

4.1.2.7 Viashirii 54

4.2 Makosa katika matamshi ya msamiati wa Kiswahili 54

4.2.1 Matumizi yasiofaa ya msamiati wa Kiswahili..... 55

4.2.2 Matamshi yasiofaa ya msamiati wa Kiswahili 55

4.2.3 Tafsiri kutoka Ekegusii hadi Kiswahili..... 56
4.2.4 Matumizi ya msamiati wa Kiingereza..... 56
4.3. Sauti za Ekegusii na Kiswahili 57
4.3.1 Sauti za Ekegusii 57
4.3.2 Sauti za Kiswahili 58
4.4. Sauti na mahali pa kutamkia 59
4.4.1. Sauti za midomo 59
4.4.2. Sauti za midomo – meno 59
4.4.3. Sauti za ufizi 59
4.4.4. Hali ya glota na mahali pa kutamkia na jinsi ya kutamka 60
4.4.5 Mahali pengine pa kutamkia 60
4.4.5.1. Sauti za kaa kaa gumu na ulimi 60
4.4.5.2. Sauti za kaa kaa laini 60
4.4.5.3. Sauti za koromeo 60
4.5. Vituo 60
4.5.1. Vipasuo 60
4.5.2. Vizuiwa – kwamizwa 61
4.5.3. Vikwaruzo / vikwamizo 61
4.5.4. Sauti za Nazali / vipua / ving'ong'o 61
4.5.5. Sauti za kitambaza 62
4.5.6. Sauti za kimadende 62
4.6.. Tatizo la kisauti 62
4.3.4. Mifanyiko ya kifonolojia 62
4.6.1.1. Sauti za [b] na [p]..... 63
4.6.1.2. Sauti za [t, d, θ, na ð]..... 64
4.6.1.3. Sauti za [č] na [ʄ] 66
4.6.1.4 Sauti za [f] na [v] 67
4.6..1.5. Sauti za [s],[z] na [ʃ]..... 68
4.6.1.6 Sauti ya [h] 69
4.6.1.7. Sauti za [l] na [r]..... 70

4.6..4.2. Hitimisho 70

SURA YA TANO

5.0 Makosa katika uandishi wa insha kwa Kiswahili 72
5.1 Makosa ya sarufi 72
5.1.1 Kutozingatia ngeli 72
5.1.1.1 Kutozingatia ngeli ya {N-N}..... 73
5.1.1.2 Ngeli ya {Ji – Ma} 73
5.1.2 Upatanisho wa kisarufi 73
5.2.1 Vivumishi vya sifa 74
5.2.2 Vivumishi - vimilikishi..... 75
5.2.3 Virejeshi..... 75
5.2.4 Viashirii 76
5.2.5 Viunganishi 77
5.2.5.1 Kiunganishi {na}..... 77
5.2.5.2 Kiunganishi {ni }..... 77
5.2.5.3 Kiunganishi {kwa}..... 77
5.2.5.4 Kiunganishi {katika}..... 78
5.3 Athari za Ekegusii katika matumizi ya msamiati wa Kiswahili ... 78
5..3.1 Matumizi ya msamiati wa Ekegusii 78
5.3.2 Tafsiri kutoka Ekegusii hadi Kiswahili 80
5.3.3 Matumizi ya Msamiati wa Kiswahili kimakosa 81
5.3.4 Matumizi ya Msamiati wa Kiingereza 82
5.3.5 Matumizi yasiyofaa ya tamathali za lugha ya Kiswahili 83
5.4 Makosa ya kitahajia katika uandishi wa insha..... 83
5.4.1 Fonimu za Ekegusii na Kiswahili..... 84
5.4.1.1 Fonimu za Ekegusii 84
5.4.1.2 Fonimu za Kiswahili 84
5.4.1.3. Tatizo la kisauti 85
5.5 Makosa ya kitahajia katika insha kwa Kiswahili 85
5.5.1 Fonimu za / b / na / p /..... 85

5.5.2. Fonimu za / d / ,/ θ/ , / ð /..... 86

5.5.3 Fonimu za / f / na / v /..... 88

5.5.4. Fonimu za / ɣ /..... 88

5.5.5. Fonimu za / h /..... 89

5.5.6. Fonimu za / č / na / ɟ /..... 90

5.5.7. Fonimu za / l / na / r /..... 91

5.5.8. Fonimu za / s /, / z / na / ʃ /..... 92

SURA YA SITA

6.0 matokeo ya utafiti 94

6.1 Makosa katika mijadala 94

6.1.1 Wastani wa makosa kwa kila kitengo 95

6.1.2 Mchango wa makosa kwa kila kitengo 96

6.1.3 Makosa katika uandishi wa insha 96

6.2. Wastani wa makosa 97

6.2.1 Wastani wa makosa kwa kila kitengo katika insha 97

6.2.2 Mchango wa makosa kwa kila kitengo katika insha..... 98

6.2.3 Matamshi na tahajia 98

6.3 Hitimisho na mapendekezo 99

6.3.1 Hitimisho 99

6.3.2 Mapendekezo 100

Marejeleo 101

Viambatisho 105

5.5.2. Fonimu za / d / ,/ θ/ , / ð /..... 86

5.5.3 Fonimu za / f / na / v /..... 88

5.5.4. Fonimu za / ɣ /..... 88

5.5.5. Fonimu za / h /..... 89

5.5.6. Fonimu za / č / na / ʄ /..... 90

5.5.7. Fonimu za / l / na / r /..... 91

5.5.8. Fonimu za / s /, / z / na / ʃ /..... 92

SURA YA SITA

6.0 matokeo ya utafiti 94

6.1 Makosa katika mijadala 94

6.1.1 Wastani wa makosa kwa kila kitengo 95

6.1.2 Mchango wa makosa kwa kila kitengo 96

6.1.3 Makosa katika uandishi wa insha 96

6.2. Wastani wa makosa 97

6.2.1 Wastani wa makosa kwa kila kitengo katika insha 97

6.2.2 Mchango wa makosa kwa kila kitengo katika insha..... 98

6.2.3 Matamshi na tahajia 98

6.3 Hitimisho na mapendekezo 99

6.3.1 Hitimisho 99

6.3.2 Mapendekezo 100

Marejeleo 101

Viambatisho 105

Majedwali na michoro

Jedwali (i)	**Matokeo ya mtihani wa Kiswahili (1997 – 1999)**	**3**
Jedwali (ii)	**Matokeo ya mtihani wa Kiswahili (1983 – 1985)**	**3**
Jedwali (iii)	**Matokeo ya kidhahania (shule moja)**	**11**
Jedwali (iv)	**Makosa katika mijadala**	**91**
Jedwali (v)	**Makosa katika insha**	**93**

Mchoro

Vokali za Ekegusii **57**

SURA YA KWANZA

1. UTANGULIZI

Sura hii inatoa maelezo juu ya tatizo la matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili wa kidato cha nne wilayani Kisii Kusini. Inaanza kwa kueleza umuhimu wa lugha katika jamii. Kunaonyeshwa jinsi serikali ya Kenya inajaribu kuiendeleza lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa na kubainisha jinsi matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili katika kidato cha nne ni moja ya vipingamizi vya juhudi hizo. Madhumuni na natija ya utafiti huu vinadhihirishwa. Maelezo ya kindani yametolewa juu ya mbinu za utafiti na uchanganuzi wa data zilizotumika.

1.1 Usuli wa mada

Watu hujifunza lugha ya pili kwa mahitaji ya mawasiliano mapana katika shughuli kama vile utawala, biashara na elimu. Ni kwa sababu hizi Kiswahili kimekuwa na kinaendelea kusisitizwa na kuendelezwa nchini Kenya (Mbaabu, 1985). Lugha hutumika kama chombo cha mawasiliano katika jamii. Huwa ni kiunganishi cha jamii kinachowawezesha wanajamii kuwasiliana, kujumuika na kuelewana kwa mambo fulani yanayowahusu.

Nchini Kenya kuna lugha tofauti zaidi ya arobaini (Mbaabu, 1985). Lugha hizi huzungumzwa na jamii tofauti na hivyo husababisha matatizo ya mawasiliano mapana kwa Wakenya. Ni kwa sababu hii ndipo Kiswahili kiliidhinishwa kuwa lugha ya taifa ili kitumiwe katika mawasiliano mapana. Kiswahili kiliteuliwa kuwa lugha ya taifa kwa sababu ni lugha ya Kiafrika ambayo hueleweka zaidi miongoni mwa jamii za Kenya.

Katika mwaka wa 1984, somo la Kiswahili lilipewa umuhimu wakati mfumo wa elimu wa 8-4-4 ulipoanzishwa rasmi nchini Kenya. Somo hili lilifanywa moja ya masomo ya lazima yaliyotahiniwa kuanzia shule ya msingi hadi ya upili. Jambo la kutoridhisha ni kwamba matokeo ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili yamekuwa si mazuri katika mwongo uliopita.

Matokeo mabaya ya somo hili yamekuwa yakishuhudiwa mwaka baada ya mwingine kama ilivyothibitishwa na ripoti ya Baraza la Mitihani ya Kitaifa la Kenya (KNEC) mwaka 1992. Kamati hii iliripoti ifuatavyo;

> *Matokeo ya wanafunzi katika Kiswahili hayakuridhisha. Kazi ya wanafunzi, hasa katika insha za Kiswahili, ilionyesha tofauti ndogo sana kutoka kwa ile ya mwaka 1989. Wanafunzi wachache sana walipata alama thelathini na zaidi.* *

Hali iliendelea kuwa mbaya na miaka sita baadaye KNEC (1998) ilieleza kwamba;

> *"Wanafunzi wengi bado wanaendelea kufanya vibaya katika Kiswahili hasa katika uandikaji wa insha."* **

Kutokana na maelezo hayo ni wazi kwamba matokeo mabaya ya mtihani wa Kiswahili katika kidato cha nne ni tatizo la kitaifa. Sehemu mbali mbali kote nchini zinaathiriwa na hali hii. Sehemu mojawapo ni wilaya ya Kisii Kusini, ambayo imekuwa ikiorodheshwa miongoni mwa wilaya za mwisho kote nchini katika somo la Kiswahili.

Katika uchunguzi wake wa awali, mtafiti alifanikiwa kupata takwimu inayodhihirisha baadhi tu ya matokeo mabaya kama yanavyoonyeshwa katika jedwali (i) Ukurasa 3

Ushahidi unaotokana na jedwali hili unadhihirisha wazi kwamba wanafunzi wengi wilayani Kisii Kusini hupata alama duni kuanzia [D]na kuendelea chini ilhali ni wachache sana ambao hupata alama kuanzia [C+]na zaidi.

Tatizo la matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili wa kidato cha nne linadhihirika kuwepo hata kabla ya mfumo wa elimu wa 8-4-4. Jedwali (ii) Ukurasa 3, linaonyesha jinsi matokeo ya mtihani wa Kiswahili wa kidato cha nne yalivyokuwa yakididimia mwaka baada ya mwingine. Pia mtafiti anafanya ulinganishi wa kubainisha ni katika kipindi kipi matokeo haya yalikuwa mabaya zaidi.

N/B. Ripoti (*) na (**) zilitoka Ofisi ya Baraza la Mitihani ya Kitaifa la Kenya.

Jedwali (i). *Takwimu ya matokeo ya mtihani wa Kiswahili 1997 - 99*

ALAMA	1997	1998	1999
A	12	10	5
A-	28	27	7
B+	121	117	19
B	204	213	97
B-	344	337	121
C+	496	483	293
C	612	598	492
C-	577	559	621
D+	661	597	687
** D	1,239	1,465	1,645
D-	596	610	835
E	84	63	112
Jumla ya watahiniwa	**4,974**	**5,079**	**4,934**

Jedwali (ii). Matokeo ya mtihani wa Kiswahili kabla ya mfumo wa 8-4-4

ALAMA	1983	1984	1985
Vyema sana - 1	5	0	0
Vyema sana- 2	17	19	22
Vyema - 3	35	39	36
Vyema - 4	68	63	69
Vyema - 5	102	91	100
Vyema - 6	110	108	128
Kufaulu - 7	131	170	163
Kufaulu - 8	137	152	168
Kuanguka - 9	35	46	63
Jumla ya watahiniwa	**640**	**691**	**746**

Takwimu kutokaOfisi ya Elimu ya Wilaya, Ogembo, Kisii Kusini na Ofisi ya Elimu ya Mkoa wa Nyanza, Kisumu.

Kutokana na majedwali mawili (a) na (b) mambo yafuatayo yanajitokeza wazi:-

(i) Katika miaka ya 1983,1984 na 1985 ni watahiniwa 63 tu kati ya 2077, yaani 3%, waliopata alama za juu sana kiwango cha 1 na 2. Ingawa kiwango hiki ni kidogo bado ni afadhali kuliko hali ilivyokuwa katika miaka ya 1997,1998 na 1999. Katika miaka hiyo ni watahiniwa 89 tu kati ya 14,987 yaani 0.59% waliopata alama za juu kabisa , tuzo [A]na [A-]

(ii) Katika kipindi cha 1983 hadi 1985, watahiniwa 949 kati ya 2077 yaani 45.69 % walipata alama kiwango kizuri (3 hadi 6) ilhali ni watahiniwa 6,304 kati ya 14,987 yaani 42.06% waliopata alama [C-] hadi [B+] katika kipindi cha miaka ya 1997 hadi 1999.

(iii) Watahiniwa 921 kati ya 2077 yaani 44.3% walikuwa katika kiwango cha chini cha kufaulu kati ya 7 na 8 katika kipindi cha miaka ya 1983 hadi 1985 ilhali katika kipindi cha miaka ya 1997 hadi 1999 ni watahiniwa 8,367 kati ya 14,987 yaani 55.83 % waliopata alama [D-] hadi [D+] ambazo ni alama za chini.

(iv) Walioanguka katika kipindi cha miaka 1983 hadi 1985 ni 144 kati ya 2077 yaani 6.93 % ilhali walioanguka katika kipindi cha miaka ya 1997 hadi 1999 ni 259 kati ya 14,987 ambayo ni 1.7%.

Kutokana na takwimu hizi zilizopatikana, inadhihirika kwamba kumekuwepo na matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa katika somo la Kiswahili wilayani Kisii Kusini. Utafiti huu ulilenga hasa kutafuta kiini cha kiisimu cha matokeo haya mabaya.

Whiteley (1969:3), anatoa sababu za tatizo linaloshughulikiwa hapa kwamba linatokana na matumizi ya lugha za mama ambazo si Kiswahili, jambo ambalo huathiri lugha ambazo mwanafunzi atajifunza baadaye. Utafiti huu ulikuwa na lengo la kubainisha jinsi lugha ya mama humwathiri mwanafunzi katika kujifunza lugha ya pili na kuathirika katika mtihani. Whiteley (1969:3) amewagawa watumiaji wa Kiswahili katika vikundi vinne vifuatavyo:

Wale ambao Kiswahili ni lugha yao ya kwanza.

Wale ambao Kiswahili ni lugha yao ya pili kupitia shuleni au mahali penginepo ambapo huingiliana na wasemaji wa Kiswahili.

Wasemaji wa Kiswahili kwa nadra sana kwa mfano pale wanaposafiri au kutembelewa na wageni wazungumzao Kiswahili.

Wale wanaolazimika kusema Kiswahili katika kipindi au mazingira maalum kama vile utoaji wa hotuba rasmi, hali ya ugonjwa au katika mahojiano na walinda usalama kama maafisa wa polisi.(Tazama Whiteley,1969:3)

Kutokana na maelezo ya Whiteley (1969), inadhihirika kwamba wanafunzi wa kikundi cha (i) huwa tayari wana ujuzi wa Kiswahili kuliko wanafunzi wa vikundi vya (ii) hadi (iv). Kadhalika, inadhihirika kwamba mwanafunzi anayesoma Kiswahili kama lugha ya pili ni lazima afundishwe na mara nyingi huwa anafanya mazoezi akiwa nje ya shule (kama vile kutoka miongoni mwa jamii , vyombo vya habari na hotuba za hadhara.) Kasoro iliyopo hapa ni kwamba Kiswahili kutoka nje ya shule kinaweza kuwa si sanifu kwani kinaweza kuwa kinatoka kwa wasiokijua vyema hasa kikitoka kwa wasemaji ambao lugha zao za kwanza si Kiswahili.

Kimemia (2001:21-27, 38-40) anaelezea kwa undani jinsi wingi wa lugha asili za Kenya unavyoathiri maendeleo ya Kiswahili nchini. Anabainisha matatizo yanayoibuka kutokana na tofauti ya makundi ya kijamii yaliyoko nchini kama vile Wabantu, Wanaili, Wakushi na mseto wa Wanaili-Wahamiti. Anaeleza jinsi kila kundi huchangia au kuzorotesha Kiswahili. Hata hivyo, anafafanua kwamba licha ya kuwepo tofauti hizi, bado Kiswahili ni lugha ya mawasiliano mapana nchini Kenya. Mtaalamu huyu anachambua kwa undani tatizo la matumizi ya lugha tatu; lugha za asili, Kiswahili na Kiingereza, katika kufundishia. Lugha za asili hutumiwa katika shule za vijijini katika elimu ya msingi, Kiswahili hutumiwa kufundishia katika shule za upili na vyuoni kwa nadra sana ilhali Kiingereza hutumiwa sana kufundisha katika shule za upili,vyuo vikuu na taasisi mbali mbali za elimu ya juu. Licha ya kutotiliwa maanani, mtaalamu huyu anakiri kwamba Kiswahili ni lugha muhimu ambayo inahitaji kuzingatiwa na kupewa kipa umbele kielimu na kisiasa. Matatizo mengine ni ukosefu wa sera imara ya lugha na fedha miongoni mwa mengine.

Katika kazi hii, mtafiti ameshughulikia jinsi mwanafunzi wa Kiswahili huathiriwa na athari za lugha yake ya kwanza na kubainisha matatizo yanayokumba matumizi ya Kiswahili kwa jumla ambayo huchangia matokeo mabaya. Makosa yanayotokana na athari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili zinaweza kubainishwa katika uandishi wa insha za Kiswahili sehemu ambayo mwandishi hupaswa kudhihirisha ubunifu wake, mtiririko wa mawazo, uamuzi bora juu ya jambo analoliezea na kujieleza wazi.

Baraza la mitihani ya Kitaifa la Kenya (1998), lilitoa sababu za kuanguka katika insha kuwa ni:

matumizi ya lugha isiyo sanifu

msamiati usiofaa / hafifu

kutozingatia njeo/ngeo

1.2. Mada ya utafiti

Tatizo kuu lililoshughulikiwa katika utafiti huu ni matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili wa kidato cha nne kwa wanafunzi Wakisii wilayani Kisii Kusini.

Utafiti huu unashughulikia makosa ya kiisimu yanayotokana na Ekegusii yanayofanywa na wanafunzi Wakisii na ambayo hatimaye huchangia matokeo mabaya katika wilaya hii. Katika kazi hii kumebainishwa makosa ya kiisimu kama vile kisarufi, kihijai na kimsamiati ambayo hufanywa na wanafunzi wa kidato cha nne kwenye mitihani yao ya kitaifa katika lugha ya Kiswahili.

Inadhihirishwa wazi jinsi lugha ya Ekegusii inavyoathiri wanafunzi Wakisii katika matumizi yao ya Kiswahili katika mtihani wa kitaifa wa somo la Kiswahili. Mtafiti ameshughulikia pia sababu hizi za kiisimu na athari zake katika uandishi mbaya wa insha.

1.3. Madhumuni ya utafiti

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa:

Kuchunguza na kudhihirisha kiini cha kiisimu cha matokeo mabaya katika somo la Kiswahili katika mtihani wa Kiswahili wa kidato cha nne wilayani Kisii

Kusini.

Kuchunguza na kuainisha makosa ya kisarufi, kihijai na kimsamiati yanayotokana na athari za Ekegusii na kubainisha ni kwa kiwango gani makosa hayo husababisha matokeo mabaya kwa wanafunzi hao katika mtihani wa mwigo wilayani na hatimaye yale ya kitaifa.

Kupendekeza jinsi ya kurekebisha matatizo ya lugha ya Kiswahili ya wanafunzi wakisii yanayotokana na athari za Ekegusii.

1.4 Nadharia tete

Nadharia tete zilizozingatiwa ni:

Wanafunzi Wakisii wanapojifunza na kutumia Kiswahili sanifu hufanya makosa ya kisarufi, kimsamiati na kihijai yanayosababishwa na athari za Ekegusii.

Makosa ya kisarufi, msamiati na hijai katika Kiswahili cha wanafunzi Wakisii yanaathiri vibaya na kudhoofisha matokeo ya mtihani wa Kiswahili wa mwigo wa wilayani na hatimaye yale ya kitaifa ya kidato cha nne.

Makosa ya kisarufi, msamiati na hijai yanayofanywa na wanafunzi Wakisii katika Kiswahili sanifu yanaweza kurekebishwa kwa kuzingatia mapendekezo ya utafiti huu.

1.5 Upeo

Kazi hii inachanganua na kueleza makosa yanayotokana na uziada wa kisarufi katika vitengo vya sarufi (kama vile ngeli, vivumishi mbalimbali, virejeshi, viunganishi na viashirii), msamiati na hijai. Hata wataalam Polome (1967:137) na Littlewood (1984:28), wanaamini kwamba uziada hudhihirika zaidi katika vivumishi, virejeshi, nafsi na tarakimu. Katika utafiti huu mtafiti anajaribu kuyachunguza maoni ya wataalamu hawa ikiwa ni kweli uziada huo unajitokeza wakati wanafunzi wakisii wanapozungumza na kuandika Kiswahili sanifu.

Mtafiti ametumia wanafunzi wa kidato cha nne kwa sababu wanafunzi hawa wamefundishwa kwa muda mrefu na wamepitia viwango vingi vya masomo. Wanafunzi hawa wanatarajiwa kuwa wameimudu lugha ya Kiswahili kwa

kiwango cha juu kiasi cha kutofanya makosa ya kisarufi katika matumizi yao ya Kiswahili sanifu. Walitarajiwa kuwa wamejifunza kikamilifu kabla ya kuukabili mtihani wa kitaifa wa Kiswahili.

1.6 Umuhimu wa utafiti

Hakuna utafiti wowote uliowahi kufanywa kuchunguza kiini hasa cha matokeo mabaya ya lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi Wakisii wa kidato cha nne wilayani Kisii Kusini. Utafiti huu umeliwekea suala hili msingi utakaojengewa na watafiti wa baadaye.

Utafiti huu ni wa manufaa kwa wanafunzi wa Kiswahili kwa sababu unafichua makosa ya kisarufi, kimsamiati na kihijai wanayofanya wanafunzi Wakisii katika Kiswahili sanifu ili wajirekebishe. Kwa kuzingatia mapendekezo ya utafiti huu, wanafunzi wataweza kujirekebisha kisarufi, kimsamiati na kihijai ipasavyo na hivyo makosa haya ya wanafunzi yatapunguka na hatimaye kuimarisha matokeo ya mtihani wa Kiswahili wilayani Kisii Kusini. Walimu watanufaika kwa sababu watapata ujuzi zaidi kutokana na utafiti huu ili waimarishe mbinu za ufundishaji na kukosoa wanafunzi wanapofanya makosa yatokanayo na athari za lugha zao za kwanza kwa jumla katika matumizi ya Kiswahili katika mtihani wa kitaifa wa Kiswahili. Kadhalika, utafiti huu ni mchango muhimu katika uwanja mpana wa ujifunzaji wa lugha ya pili katika taaluma ya isimu na pia changamoto kwa wasomi wengine wanaotaka kufanya utafiti zaidi katika taaluma hii. Wataalamu hawa wataweza, ama kujaza maeneo ambayo hayajashughulikiwa na utafiti, au kuuimarisha. Aidha, kwa misingi ya utafiti huu wataalamu na wanaohusika na mpango wa sera ya lugha wataweza kuweka mikakati ifaayo ya kurekebisha makosa na kuimarisha umilisi wa Kiswahili wa wanafunzi katika wilaya ya Kisii Kusini na kwingineko nchini.

1.7. Mbinu za utafiti

Mtafiti alitumia mbinu ya upekuzi wa vitabu, majarida na makala mwafaka katika maktaba mbalimbali nchini Kenya ili kudhibiti mada kabla ya kufanya utafiti nyanjani.

Mtafiti alikusanya data ya utafiti huu kutoka miongoni mwa wanafunzi wa kidato cha nne katika shule kumi na tano (15) wilayani Kisii Kusini. Watahiniwa kumi (10) waliteuliwa kutoka shule kumi na nne (14) na sita (6) kutoka shule moja iliyokuwa na wanafunzi hao sita) Shule hizi ziligawanywa katika vikundi vitatu yaani shule za wavulana pekee,wasichana pekee na zile za mseto.

Insha za watahiniwa mia moja na arobaini na sita (146) katika mtihani wa mwigo wa wilayani wa kidato cha nne zilitumiwa ili kubainisha makosa yaliyotokana na athari za Ekegusii katika Kiswahili sanifu ambayo watahiniwa waliyafanya na jinsi makosa hayo yalivyochangia katika matokeo ya wanafunzi katika mtihani wa mwigo wilayani.

Mijadala iliandaliwa wanafunzi wa kidato cha nne katika shule hizo kumi na tano (15). Mazungumzo yao yalinaswa kwa kinasa sauti. Kutokana na mazungumzo hayo, mtafiti aliorodhesha makosa ya wanafunzi kumi kutoka kila shule kwa shule kumi na nne, na sita kutoka shule moja, ambayo yalitokana na athari za Ekegusii katika Kiswahili sanifu na kubashiri kiwango ambacho makosa hayo yalichangia katika matokeo mabaya kote wilayani humo.

1.7.1 Ukusanyaji wa data

Wanafunzi wa kidato cha nne katika shule kumi na tano wilayani Kisii Kusini walihusishwa katika kupata data iliyokusanywa. Shule hizo kumi na tano ni sawa na sehemu moja ya tano ya shule zote wilayani Kisii Kusini. Hivyo, watahiniwa waliotumiwa kutoka shule hizi ni viwakilishi vya kutosheleza mahitaji ya utafiti huu. Shule hizi kumi na tano ziligawanywa katika makundi matatu. Shule tano ziliteuliwa kutoka maeneo matatu ya uwakilishi bungeni ya wilaya hii ili kuhakikisha uwakilishi sawa. Mtafiti alitumia mbinu ya bahati nasibu kuziteua shule zilizohusika.

Insha za Kiswahili katika mtihani wa mwigo wa wilayani kwa wanafunzi wote wa kidato cha nne zilitumiwa kudondoa, kubainisha na kuainisha makosa ya kisarufi, kimsamiati na kihijai yanayotokana na athari za Ekegusii katika Kiswahili. Insha ziligawanywa mara mbili. Swali la kwanza lilikuwa la lazima huku la pili likiwa la uchaguzi kati ya maswali mawili. Watahiniwa walipewa

muda wa saa moja na dakika arobaini kuandika insha zote kwa maneno kati ya mia nne na mia sita kwa kila moja. Aidha, kwa kushirikiana na walimu wa Kiswahili mtafiti aliandaa mijadala kwa wanafunzi wa kidato cha nne. Kutokana na mijadala hii wanafunzi waliweza kutoa mawazo yao yaliyofululiza kwa uhalisia wake na hivyo kubainisha ujuzi wao katika Kiswahili. Kila mzungumzaji alipewa fursa ya dakika tano.

Kisha, mazungumzo ya wanafunzi kumi kwa kila shule yalinaswa. Idadi iliyochaguliwa ilikuwa ni robo ya wanafunzi wa darasa moja. Mtafiti alidondoa makosa ya kimatamshi ya wanafunzi Wakisii yanayotokana na athari za Ekegusii katika Kiswahili. Mtafiti alifanya hivyo ili kuthibitisha kuwepo kwa uhusiano baina ya matamshi na hijai katika Kiswahili, jambo linalomfanya mwanafunzi kuandika maneno ya Kiswahili jinsi anavyoyatamka hasa kwa misingi na kanuni za Ekegusii.

Mtafiti aliwatumia wanafunzi wa kidato cha nne wa wilaya ya Kisii Kusini ili kutimiza mahitaji maalumu kama yaliyopendekezwa na Ellis (1985) ambayo ni kutumia wahojiwa wenye viwango sawa kama vile:-

elimu sawa.

mazingira yanayofanana.

matumizi ya vitabu sawa.

wazungumzaji wa lugha ya kwanza inayofanana.

Nemser (1971), anasisitiza kwamba wahojiwa (wanafunzi) kama hao wanaweza kuwa na viwango vya lugha vinavyolingana. Kuna mapendekezo ya Seliger na Shohamy (1989) na Larse-Freeman na Long (1994), juu ya mbinu za kukusanya data inayohusu makosa ya wanafunzi. Mbinu hizi ni:-

i) Kuwapa wanafunzi maswali ya tafsiri kwenye hojaji ili wayajibu.

ii) Kuwaambia wanafunzi waandike insha.

iii) Kuwaambia wanafunzi kusimulia hadithi fupi.

Kati ya mapendekezo ya wataalam hawa, mtafiti alizingatia lile la uandishi wa insha.

Fnz = Mwanafunzi

Baada ya kubainisha na kuainisha makosa katika viwango vyote mtafiti alichanganua na kueleza jinsi makosa hayo yanayotokana na athari za Ekegusii yanavyochangia kwa jumla katika matokeo ya kidato cha nne ya Kiswahili wilayani Kisii Kusini.

1.7.2 Uchanganuzi wa data

Etherton (1977), ameainisha mitazamo miwili ya uchanganuzi wa data.

1. Mtafiti kuamua aina ya makosa anayotaka kuchunguza katika kazi za wanafunzi.
2. Kuacha aina ya makosa yatakayochunguzwa yajitokeze yenyewe katika kazi hizo.

Katika utafiti huu mtafiti ametumia mtazamo wa kwanza (i) ambapo ameshughulikia makosa katika vitengo vya kisarufi kama vile ngeli, vivumishi, virejeshi, viunganishi na viashirii. Kisha mtafiti ameshughulikia msamiati na hijai.

Katika uchanganuzi wa data mtafiti alitumia uchanganuzi thamano na wingidadi ambapo alitumia mbinu za msambao wa umaratokezi na kipimo cha ulemeakati cha wastani wa kihesabu kama inavyoonyeshwa katika mfano dhahania ufuatao.

Asilimia tano ya wanafunzi arobaini walipata alama kumi na tano juu ya arobaini. Haya yanaweza kufupishwa kitakwimu kama ifuatavyo:-

5% ya wanafunzi 40 walipata 15/40.

Kwa kuzingatia mbinu zilizotajwa za uchanganuzi, mtafiti alidhihirisha ni kiwango gani athari za Ekegusii hudhoofisha matokeo ya mtihani wa Kiswahili katika vitengo vya sarufi, msamiati na hijahi.

Mtafiti alichanganua data ya makosa na kutoa matokeo yake kwa kuzingatia alama walizopata wanafunzi katika kila kitengo.

Jedwali (iii): ***Matokeo ya kidhahania ya wanafunzi katika kila kitengo (Shule moja)***

Kitengo	**Alama zote**	**Fnz A**	**Fnz B**	**Fnz C**	**Fnz D**	**Fnz E**	**Fnz F**	**Fnz G**	**Fnz H**	**Fnz I**	**Fnz J**	***Kipimo cha Ulemeakati cha wastani***
Sarufi	15	6	7	10	2	3	6	4	4	3	5	5
Msamiati	15	8	5	5	4	6	6	5	4	7	5	5.5
Hijai	10	6	6	8	5	7	5	4	4	5	3	5.3
Jumla	40	20	18	23	11	16	17	13	12	15	13	15.8

SURA YA PILI

2.0. Uhakiki wa maandiko na nguzo za kinadharia.

2.1. Uhakiki wa maandiko

Kuna tafiti nyingi ambazo zimefanywa juu ya ujifunzaji wa lugha ya pili na matatizo yanayoambatana nao. Baadhi ya wataalam walioshughulikia swala hili ni pamoja na Whorf (1956; Lado (1957), Whiteley (1964), Halliday (1974), Corder (1978), Wanyoike (1978), Dulay, Burt na Krashen (1982), Kress (1983), Idarus (1983), Mbaabu (1985), Njoroge (1987), Besha (1991), Were (1996) na Onyango (1997).

Onyango (1997), amemnukuu Whorf (1956) akieleza katika utafiti wake kwamba:

> *Tunavyoiona dunia, tunavyotofautisha vitu kulingana na mazoea yetu na kumlika mazingira; yote husababishwa na lugha yetu ya kwanza. Tunaona, tunahisi, tunaandika, tunaongea; vile tufanyavyo kwa sababu tabia za jamii zetu huhitaji uchaguzi fulani wa kufasiri. Kwa hivyo, tabia ya lugha ya kwanza huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili.*

Maoni haya yaliungwa mkono na Halliday (1964) na Corder (1973).

Lado (1957:102), anasema kwamba mwanafunzi anayekumbana na lugha ngeni atapata vipashio vyake fulani vikiwa rahisi na vingine vigumu sana. Zile sehemu zilizo sawa na zile za lugha yake asili zitakuwa rahisi kwake na zile ambazo ni tofauti zitakuwa ngumu. Iwapo mofimu fulani katika lugha ya kwanza haipo katika lugha ya pili, mwanafunzi atajaribu kuiongeza kwa kutumia mofimu ya lugha yake ya asili inayoonekana kukurubiana mofimu iliyo katika muundo mzima wa lugha yake ya kwanza (Tazama Lado 1957:102).Katika utafiti huu inabainka kwamba wanafunzi Wakisii huongeza mofimu za Ekegusii katika Kiswahili na hivyo kukiuka kanuni za Kiswahili,

Halliday (1964), anatufahamisha kwamba ujifunzaji wa lugha ya pili kwa kawaida hufanyika baada ya kujifunza lugha ya kwanza kumekamilika. Katika kiwango hiki ajifunzaye lugha huwa tayari amejenga umilisi wa kutosha wa

kimawasiliano katika lugha yake ya kwanza. Kutokana na hali hii, lugha ya kwanza ya mwanafunzi inaweza kuathiri kwa kiasi fulani lugha ya pili, ya tatu na zaidi (Tazama Halliday 1964: 113).

Maelezo haya yalifaa sana katika utafiti huu kwani mtafiti ameyathibitisha kwa kuzingatia wanafunzi Wakisii wa kidato cha nne. Wanafunzi hao, mbali na kuwa na umilisi wa lugha yao ya kwanza (Ekegusii) wamejifunza Kiswahili huku wakiathiriwa na Ekegusii.

Whiteley (1974), anadokeza kwamba tabia za lugha ya kwanza hujiingiza katika tabia za lugha ya pili. Kujiingiza kwa tabia za lugha za kwanza zimesababisha Kiswahili kinachojulikana kama "maeneo" ya ukubalifu mkubwa katika lugha ya Kiswahili. Katika hali hii msemaji [*A*]atakubali muundo wa lugha ya Kiswahili unaotumiwa na msemaji [*B]* ambao yeye [*A*]mwenyewe hangeweza kuutumia. Mfano aliotoa ni kama vile Kiswahili cha "Kijaluo", "Kikikuyu", "Kipsigis" "Kikamba" na "Kisetla". Utafiti huu unabainisha kwamba athari za Ekegusii hudhihirika katika matumizi ya Kiswahili hasa katika mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne na kwamba Kiswahili hicho kilichoathiriwa na Ekegusii kinaweza kuwekwa katika kiwango sawa na alivyofanya Whiteley(1969), yaani Kiswahili cha "Kikisii".

Kwenye utafiti wake Corder (1978), aligundua kwamba wakati watu wanapojifunza lugha ya pili, huwa tayari wanayo lugha ya kwanza. Baadhi ya kanuni wanazozielewa katika lugha ya kwanza hutumiwa katika usemaji na uwelewaji wa lugha ya pili. Kutokana na hali hii, kuna mazoea ya kuzitumia kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya pili na hivyo makosa hutokea. Utafiti huu unathibitisha ukweli huu kama unavyodhihirika miongoni mwa wanafunzi Wakisii wa kidato cha nne wilayani Kisii Kusini.

Wanyoike (1978), alishughulikia fonolojia ambapo anaonyesha mifano mbali mbali ya ukiukaji wa kanuni za matamshi ya Kiswahili sanifu unaofanywa na wanafunzi kutoka jamii kadhaa za Kenya kama Wajaluo, Wakikuyu, Wakamba, Wahindi na Wakalenjin. Wanyoike (1978), alitoa maoni kwamba kunahitajika sasa kufanywe uchunguzi unaohusiana na mafunzo ya Kiswahili ili kudhihirisha ni matatizo gani ya kipekee yanayowakabili watu kutoka jamii mbalimbali za

lugha wanapojifunza Kiswahili kwa ajili ya tofauti zilizoko kati ya lugha hii na lugha zao. Utafiti wa Wanyoike (1978), haukushughulikia sarufi na hivyo kuacha pengo lifaalo kuzibwa. Upungufu huu wa Wanyoike ulikuwa kichocheo cha utafiti huu.

Idarus (1983), ameainisha makosa ya kifonolojia na kileksia na anatambua chanzo chake katika lugha za kwanza za Tanzania. Inaelekea hakukusudia kuchunguza makosa katika kiwango kimoja cha lugha wala kuongozwa na nadharia za kisasa. Licha ya hivyo, kazi yake ni kichocheo cha uchunguzi zaidi kuhusu nafasi ya lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili na athari za makosa yanayojitokeza katika mitihani ya kitaifa ya somo la Kiswahili. Katika kazi hii mtafiti amechunguza athari za lugha ya kwanza katika ujifunzaji na matumizi ya lugha ya pili hasa katika mtihani.

Mbaabu (1985), alifanya utafiti ambapo hakuwalenga wanafunzi darasani. Alichunguza makosa ya kisarufi, kifonolojia na kisemantiki yanayofanywa na Wakenya mbali mbali wanaojifunza Kiswahili. Anasema kwamba baadhi ya makosa haya yanatokana na lugha ya kwanza. Pia, Mbaabu (1985) aliandika kuhusu makosa ya kawaida yanayotokea mara kwa mara wakati watu wanapojaribu kuzungumza na kuandika Kiswahili sanifu. Amekusanya na kuyasahihisha makosa yanayotokana na athari za lugha ya kwanza ambayo yanajumuisha yale ya kimsamiati na kifonolojia. Kadhalika, ameyachunguza makosa ya kimatamshi na kisarufi ambapo kanuni za matumizi ya viambishi hukiukwa. Aidha amegusia makosa yanayohusu virejeshi vya aina mbalimbali. Ingawa utafiti wa Mbaabu umezingatia karibu maeneo yote ya lugha na kutoa mwongozo unaofaa, ni uchunguzi jumuishi kinyume na utafiti ambao umejikita katika lugha ya Kiswahili. Hii ndiyo sababu utafiti huu umeshughulikia kwa undani suala la athari za lugha ya Ekegusii katika kiwango cha kisarufi, kimsamiati na kihijai na kuthibitisha jinsi athari hizi zinavyochangia katika kudhoofisha matokeo ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili wilayani Kisii Kusini.

Njoroge (1987), ameshughulikia kwa kina jinsi lugha za kwanza za watoto wa shule kutoka baadhi ya jamii za Kenya zinavyoingilia na kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiingereza. Kwa kufuata nyayo zake, utafiti huu umeshughulikia lugha

ya Kiswahili na jinsi mwingilio wa lugha ya kwanza ya jamii moja ya Kenya,Ekegusii, inavyoathiri ujifunzaji na utumiaji wa lugha ya Kiswahili.

Naye Besha (1991), alifanya utafiti uliowalenga watu wazima wa jamii ya Kimaasai wanaojifunza Kiswahili nchini Tanzania, upande wa matamshi, upangaji wa maneno, mfumo wa nomino (majina) pamoja na miundo ya vitenzi vya Kiswahili. Ameshughulikia ujifunzaji wa lugha ya pili lakini katika kazi hii mtafiti ameshughulikia jinsi ujifunzaji wa Kiswahili unavyoathiriwa na Ekegusii na hatimaye kuathiri matokeo ya mtihani wa Kiswahili.

Were (1996), ameshughulikia makosa ya kisarufi, kimsamiati na uendelezaji wa maneno yanayosababishwa na lugha ya kwanza ya wanafunzi Wabukusu wa kidato cha tatu wilayani Bungoma. Amezingatia data ya uandishi wa insha huku akionyesha kwamba 29% ya makosa ya kisarufi, 61.4% ya uendelezaji wa maneno na 56.3% ya makosa ya kimsamiati, yalisabibishwa na athari za Kibukusu katika Kiswahili sanifu. Kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi Makosa aligundua kwamba wanafunzi walitumia mbinu ya ujumulishaji mno walipojifunza kuandika Kiswahili sanifu. Kazi hii imemnufaisha sana mtafiti kwani Wakisii, sawa na Wabukusu, ni Wabantu ingawa lugha hizi zina vipengee kadhaa vinavyotofautiana kifonolojia na kimofonolojia. Kazi hii ya Were (1996), imelejelewa ili kudhibiti mada ya utafiti huu.

Campbell na Qorro (1997), walishughulikia hali ya matokeo ya wanafunzi wa shule za upili katika lugha ya Kiingereza nchini Tanzania. Waligundua kwamba matokeo yalikuwa mabaya na yalitokana na ukweli kwamba wanafunzi hao walikuwa na mizizi ya lugha nyingine, halafu Kiswahili na hatimaye Kiingereza kilikuwa nyuma sana. Waligundua kwamba Kiingereza hakikuwa lugha ya kwanza na wengi walikuwa na lugha zao za kwanza. Kiswahili kilikuwa lugha ya kwanza kwa wachache waliozaliwa mijini. Hivyo lugha za kwanza, miongoni mwao Kiswahili ziliathiri vibaya umilisi wao wa lugha ya Kiingereza katika shule za upili nchini Tanzania. Kazi ya wataalamu hawa ilimfaidi mtafiti kwa sababu utafiti huu umeshughulikia matokeo mabaya ya mtihani wa Kiswahili pia.

Onyango (1997), ameshughulikia tofauti za kisarufi zilizopo kati ya Kinyala na Kiswahili sanifu ili kuthibitisha iwapo tofauti hizo ni kikwazo kwa wanafunzi

wa Kinyala wanaojifunza Kiswahili sanifu. Katika utafiti huu amewalenga wanafunzi wa darasa la nane wilayani Busia. Alibainisha kwamba uziada wa kisarufi katika Kiswahili cha wanafunzi Wanyala, unatokana na misingi ya lugha ya Kinyala na unaathiri vibaya ujifunzaji wa Kiswahili. Katika utafiti huu mtafiti amechunguza jinsi wanafunzi Wakisii wilayani Kisii Kusini wanavyoathiriwa na Ekegusii katika viwango vya sarufi, msamiati na hijai.

Kutokana na tafiti hizi zilizopitiwa, mambo yafuatayo yanaonekana wazi:-

a). Lugha iliyoshughulikiwa zaidi ni Kiingereza.

b). Kiswahili kimeshughulikiwa na wataalamu wachache.

c). Kuna lugha kadhaa za kwanza za Kenya ambazo hazijashughulikiwa.

d). Kazi nyingi zinazopatikana hivi sasa zinashughulikia makosa ya kifonolojia, kisarufi, kisemantiki na wala hazizingatii matokeo ya wanafunzi wa somo la Kiswahili katika mitihani ya Kitaifa ya Kiswahili kidato cha nne.

Hivyo basi utafiti huu ulilenga kuziba mianya iliyotajwa hapo juu pamoja na kuchangia kitaaluma katika eneo hili pana la athari za lugha ya kwanza katika kujifunza Kiswahili. Pia utafiti huu umeonyesha athari ambazo hujitokeza katika matokeo duni katika mtihani wa kitaifa wa somo la Kiswahili.

2.2. Nguzo za kinadharia

2.2.1 Nadharia Ya Uchanganuzi Makosa (N.U.M)

Nadharia hii hutumiwa katika kuchunguza chanzo cha makosa ya aina mbali mbali katika lugha. Hutumiwa katika kuyapambanua, kuainisha na kufafanua makosa ya wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili.

Sridhar (1981:222), amezitambua daraja zifuatazo za mbinu za kutekeleza N.U.M:

a) Ukusanyaji wa data (ama kutoka katika insha za wanafunzi kuhusu mada fulani au kutokana na majibu ya mtihani).

b) Utambuaji wa makosa yenyewe.

i) Ukosefu wa uwiano katika matumizi ya njeo (nyakati)

ii) Udondoshaji wa viambishi vya kiziada

c) Uainishaji wa makosa hayo katika vikundi kama vile makosa ya upatanisho wa kisarufi, vibainishio na vitenzi

d) Kuonyesha idadi ya kila kikundi cha makosa yaliyoainishwa.

e) Utambuaji wa vipengele vinavyosababisha matatizo katika lugha ya pili.(L2)

f) Urekebishaji wa makosa (kama vile kutumia mazoezi ya kutosha wakati wa vipindi vya somo la lugha).

g) Kuchanganua vyanzo vya makosa (mfano, athari za lugha ya kwanza, uchanganyaji, ukosefu wa utaratibu mwafaka wa kuendeleza maneno ya lugha ya pili, (L2))

h) Kuonyesha kiwango cha athari inayosababishwa na tokeo la kosa hilo. mfano utatanishi wa mawasiliano, ukiukaji wa kaida ya mawasiliano n.k

Katika utafiti huu Nadharia ya Uchanganuzi Makosa (NUM) imetumiwa na mtafiti. Kulingana na mwongozo wa nadharia hii mtafiti alifuata hatua zifuatazo:-

i) Amekusanya data kutoka katika insha za wanafunzi kuhusu mada waliyopewa katika mtihani wa mwigo wa Kiswahili wilayani Kisii Kusini.

ii) Amebainisha makosa mbali mbali yaliyofanywa na wanafunzi Wakisii. Baadhi ya makosa hayo ni kama vile ukosefu wa uwiano katika matumizi ya nyakati na udodoshaji wa viambishi vya kiziada

iii) Ameainisha makosa hayo kulingana na vitengo mbali mbali kama sarufi, msamiati na hijai.

iv) Ameonyesha idadi ya kila kikundi cha makosa yaliyoainishwa.

v) Ametambua vipengele vinavyosababisha matatizo katika lugha ya pili.

vi) Amechanganua vyanzo vya makosa (mfano, athari za Ekegusii kama lugha ya kwanza, uchanganyaji, ukosefu wa utaratibu mwafaka wa kuendeleza maneno ya Kiswahili kama lugha ya pili)

vii) Ameonyesha kiasi cha athari inayosababishwa na tokeo la kosa hilo (mfano utatanishi wa mawasiliano, ukiukaji wa kanuni za mawasiliano n.k.)

Norrish (1983), anasema kwamba Nadharia ya Uchanganuzi Makosa inaweza kutumiwa katika kutoa picha ya aina ya matatizo yanayowakumba wanafunzi. Anaeleza kwamba utafiti kama huo ukifanywa kwa ukamilifu unaweza kusaidia katika uandishi wa miongozo ya masomo. Corder (1974), anasisitiza kwamba

nadharia hii inatoa mwangaza kuhusu mbinu anazotumia mwanafunzi ili kuepuka matatizo hayo katika kujifunza lugha ya pili.

Hata hivyo, Nadharia ya Uchanganuzi Makosa pekee haitoi picha kamili kuhusu uchanganuzi wa makosa yanayotokea wakati wa ujifunzaji wa lugha ya pili. Sababu ni kwamba Nadharia ya Uchanganuzi Makosa hutumiwa kumulika tu sehemu fulani ya lugha ya mwanafunzi, yaani makosa, huku ikipuuza kile anachojua mwanafunzi (Ellis, 1988). Nadharia hii pia haiwezi kutumiwa katika kubashiri makosa ya lugha ya mwanafunzi. Aidha, mwelekeo wake kuhusu 'makosa' haukubaliki kwani makosa huchukuliwa kama kitu kibaya kisichofaa kuonekana katika lugha ya mwanafunzi.

Licha ya upungufu wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa nguzo zake zilifaa sana katika utafiti huu ili kupambanua, kuainisha na kufafanua makosa ya Kiswahili yanayofanywa na wanafunzi Wakisii.

2.2.2 Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi (N.U.L)

James (1980:3) anaeleza kwamba uchanganuzi Linganishi ni uchanganuzi wa kisimu unaohusu ulinganishaji wa lugha mbili. Uchanganuzi Linganishi huchunguza jinsi lugha ilivyo katika kipindi fulani maalum. Pia huchunguza lugha katika vipindi tofauti. Kwa hivyo, James (1980), anasema kwamba Uchanganuzi Linganishi huchunguza katika kiwango cha mtu binafsi jinsi mzungumzaji wa lugha ya kwanza anavyoendelea kuimudu lugha ya pili. Mbali na isimu, Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi inahusiana pia na somo la uwili-lugha. Ingawa uwili-lugha ni hali ya utumiaji wa lugha mbili katika kiwango cha mtu binafsi au jamii nzima, Uchanganuzi Linganishi unahusu uwili-lugha katika kiwango cha mtu binafsi: yaani mtumiaji wa lugha moja anavyokuwa na lugha mbili. Uchanganuzi Linganishi unahusiana pia na masuala ya kisaikolojia kwa vile huchunguza dhana ya mwingiliano yaani dhana mbali mbali katika matamshi, sarufi na kadhalika, zitokanazo na kuingizwa kwa sauti na maneno ya lugha nyingine katika lugha pokezi.

Uchanganuzi Linganishi huchukulia kwamba watu hujaribu kuhamisha maana kutoka lugha zao za kwanza hadi lugha zao za pili. Kwa hivyo, Uchanganuzi

Linganishi unahusu namna lugha ya kwanza inavyomwathiri mwanafunzi wa lugha ya pili kisemantiki. Athari hizo zinaweza kurahisisha au kutatiza jitihada za kujifunza lugha ya pili. (Taz: Lado 1957:2)

Mwanaisimu Njoroge (1987), anatoa ufafanuzi wa kindani juu ya waasisi, waendelezaji na wapinzani wa Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi. Anaeleza kuwa nadharia hii iliasisiwa katika miaka ya 1940 ambapo ilitumiwa katika kulinganisha lugha moja katika hatua zake tofauti za kimaendeleo na kulinganisha lugha mbili au zaidi ili kuziainisha katika viwango vya kifonolojia, sintakisia na semantiki ambapo usawa na tofauti kati yao vilibainishwa. Mtaalamu huyu anaendelea kutufahamisha kwamba miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Fries. Waendelezaji wake walikuwa ni Weinreich, Haugen, na Lado. Anaeleza vile Duskova alivyochunguza chanzo cha makosa baina ya wanafunzi wa Kicheki waliokuwa wakijifunza Kiingereza. Alithibitisha kwamba makosa ya wanafunzi hayakutokana tu na athari za lugha ya kwanza bali kuathiriana kwa lugha. Matokeo haya yalichochea wanaisimu kueleza upya dhana ya uathiriano na pia kudadisi ukweli wa ubashiri na nguvu za maelezo ya nadharia tete ya Uchanganuzi Linganishi.

Njoroge (1987), anaendelea kutufahamisha kwamba licha ya ushahidi mbalimbali uliotolewa dhidi ya Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi, Schachter(1964), alitumia mbinu za nadharia hii. Alilinganisha tofauti za miundo katika vifungu husishi vya Kiajemi, Kiarabu na Kichina kwa nia ya kutaka kugundua ni nani baina ya wanafunzi wangeweza kupata matatizo ya kujifundisha vifungu vya vihusishi katika Kiingereza. Hatimaye Schachter (1964), alidai kwamba aliweza kufanya ubashiri wa maneno ambayo yangeweza kuwa na ugumu kwa wazungumzaji wa kila kikundi katika kutamka vifungu hivyo katika lugha inayolengwa.

Van Els na wenzake (1984), wameeleza kuwa Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi imejikita katika nguzo zifuatazo:-

a) Sababu kuu inayoleta matatizo na kuzua makosa katika kujifunza lugha ya pili ni zile athari za lugha ya kwanza.

b) Kadri lugha ya kwanza na ya pili zinavyotofautiana kimuundo ndivyo jitihada za kujifunza lugha ya pili zinavyotatizwa zaidi.

c) Matokeo ya kuzilinganisha lugha hizo mbili hutumiwa kubashiri yale matatizo na makosa yatakayotokea wakati wa kujifunza lugha ya pili.

Mwalimu wa lugha anahitaji kufunza zile tofauti zinazodhihiri kati ya lugha hizo mbili. Mwanafunzi hafai kufunzwa vipengele vinavyofanana kati ya lugha hizo.

Utaratibu unaofuatwa katika kuchanganua vipashio vya lugha ni kuzilinganisha na kuzitofautisha ili kudhihirisha zinavyofanana na kutofautiana. Ina maana kwamba tofauti kati ya lugha ya kwanza na lugha ya pili ndiyo itatizayo ujifunzaji wa lugha ya pili ilhali kufanana kwao hurahisisha ujifunzaji huo (Taz. Lado 1957:2).

Ellis (1985:25),amezitambua na kuziorodhesha daraja tatu za utaratibu wa Uchanganuzi Linganishi. Daraja hizo ni:-

a) Maelezo mwafaka ya lugha mbili husika.

b) Uamuzi kuhusu vipengele hivyo katika lugha hizo mbili.

c) Ubashiri wa sehemu fulani za lugha ambazo huenda zikasababisha makosa.

Baadhi ya waandishi wamepinga Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi. James (1980:146), anafikiria kwamba Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi inaweza kutumiwa kubashiri kutokea kwa kosa fulani la lugha lakini haiwezi kutumiwa kubashiri umbo halisi la kosa hilo litakavyokuwa (kama ni la kisarufi au kimuundo).

Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi imekosolewa pia kwamba inasisitiza zaidi sarufi mbili, yaani, sarufi ya lugha ya kwanza na sarufi ya lugha ya pili, huku ikipuuza yule anayejifunza lugha (Taz.Norrish: 1983:28). Aidha mtafiti akijifungia tu kwa Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi atakuwa amezipuuza mbinu zingine zinazoweza kutumiwa katika kujifunza lugha ya pili, ambazo zinaelezwa na nadharia zingine. Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi inachukulia kwamba kujifunza lugha kunafanana na tabia. Littlewood (1984:19-20), anaeleza kwamba Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi imekosolewa kwa maana msingi wake ni sawa na ule wa Nadharia ya Utabia iliyozungumziwa na Skinner (1954), ambaye anadai kwamba mtu

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

anapojifunza tabia mpya, huacha ile ya zamani. Kwa hivyo, Littlewood anasema kwamba kujifunza lugha ya pili kuko hivyo. Anaendelea kusema kwamba mtu hujifunza kwa kuiga maneno na sentensi anazosikia zikitamkwa na watu wengine.

Mtazamo huu wa tabia umepingwa vikali na nadharia tete ya Chomsky (1956) ya cheche za upataji na ujifunzaji lugha (Language Acquisition Device, LAD). Kulingana na nadharia hii, kila mtoto huzaliwa akiwa tayari na uwezo wa kiakili wa kujifunza lugha yoyote,mradi tu apate kongoo. Kongoo huwa kama kichocheo cha kifaa kinachomwezesha mtoto kutumia zile kanuni asilia za lugha, zenye usifabia, kumwongoza katika kujifunza mifumo ya kisarufi, kifonolojia na kisemantiki ya lugha. Mtoto huzaliwa na kanuni hizo za usifabia. Cheche ya upataji na ujifunzaji lugha (LAD), huanza kufanya kazi utotoni na nguvu zake kuendelea kuisha mtu anapobalehe au kuvunja ungo. Kuanzia umri huu mtu hutatizwa sana anapojaribu kujifunza lugha ya pili.

James (1980), na wasomi wengine wanapinga kwamba si vizuri Uchanganuzi Linganishi kudai kwamba wanafunzi wafunzwe tu zile tofauti zilizopo baina ya lugha ya kwanza na ya pili, bali wafunzwe kufanana kuliopo ili waweze kujigundulia ni wapi uhamishaji wao wa vipengele vya lugha ya kwanza hadi lugha ya pili hukubalika na ni wapi haukubaliki. Wataalamu hao wanasema kwamba si rahisi kukadiria kikweli viwango vya ugumu katika kujifunza vipengele mbali mbali vya lugha. Sababu hasa ni kwamba, ugumu hutegemea mtazamo na uwezo wa mwanafunzi mhusika. Ugumu huo hauwezi kukadiriwa kwa kuzirejelea tu zile tofauti za kiisimu zinazojitokeza. Hii ndiyo sababu Littlewood (1984), alidai kwamba `tofauti za kiisimu' na `ugumu wa kujifunza' si dhana zinazofanana. Anashikilia kwamba dhana ya kwanza inatokana na maelezo ya kiisimu ilhali ile ya pili inatokana na mifanyiko ya kisaikolojia. Kwa hivyo, hakuna sababu yoyote inayoonyesha kwamba dhana hizo zinalingana.

Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi imekosolewa kwamba haitoi maelezo ya kuridhisha kuhusu vigezo mwafaka vinavyoweza kutumiwa katika ulinganishaji wa lugha husika. James (1980) anasema ;

> *Licha ya kuwepo kwa sifabia za lugha, inafikiriwa kwamba baadhi ya lugha haziwezi kulinganishwa hata kama zina vitengo vya kisarufi*

vinavyojulikana kama istilahi zinazofanana mfano vitenzi, vivumishi na kadhalika.

Mtafiti alichanganua vyanzo vya makosa yanayotokana na athari za Ekegusii katika Kiswahili kwa kuzingatia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, na kisha akabainisha jinsi makosa haya yanavyoathiri matokeo ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili kwa wanafunzi Wakisii wilayani Kisii Kusini. Kadhalika, mtafiti alizingatia Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi katika kutoa maelezo mwafaka ya lugha za Ekegusii na Kiswahili ili kubainisha sehemu mbali mbali za lugha ambazo ndizo zinazosababisha makosa.

Mtafiti ametumia nadharia zote mbili kwa sababu swala aliloshughulikia halingeweza kushughulikiwa kikamilifu kwa kutumia mojawapo tu ya nadharia hizo. Hakuna nadharia inayojitosheleza yenyewe kwa vile kila mojawapo ina manufaa na upungufu wake. Pia zinatofautiana kwa namna fulani. Hata hivyo, zote zina lengo moja la kimsingi ambalo ni kufanikisha ujifunzaji (na ufunzaji) wa lugha ya pili kwa kuchunguza swala la makosa katika misingi ya kisayansi inayokubalika na nadharia ya kiisimu na ile ya ujifunzaji wa lugha ya pili.Aidha utafiti huu ulisaidiwa na Nadharia ya Sifa Bainifu za sauti ambayo ni nadharia ya kifonetiki iliyoasisiwa na Trubetzkoy (1957). Nadharia hii inasisitiza uelezaji wa sifa za sauti kulingana na namna ya kuzitamka, na kwamba sifa hizo ndizo zinazobainisha sauti moja na nyingine. Nadharia hii ilisaidia katika kubainisha baadhi ya sauti tata za Kiswahili katika mazingira ya Wakisii katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili

SURA YA TATU

3.0 Makosa ya kisarufi

3.1 Utangulizi

Sura hii inatoa maelezo ya kimsingi ya vipengele kadhaa vya kisarufi ambavyo katika utafiti huu ilibainika kwamba vinaleta utata katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi Wakisii kama lugha yao ya pili . Vipengele hivyo ni ngeli ,vivumishi vya aina mbalimbali, virejeshi,nafsi, na tarakimu. Maelezo haya yanahusu sarufi za Ekegusii na Kiswahili sanifu. Ulinganishaji unaotokana na sarufi hizi mbili unanuiwa kuangaza tofauti za kisarufi kama msingi wa kuelewa makosa yanayoyafanya wanafunzi Wakisii wanapojifunza na kutumia Kiswahili sanifu katika mitihani. Misingi ya Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi ndiyo inayotumika katika ulinganishaji huu.

3.2. Ngeli za Ekegusii

3.2.1. Maelezo

Mbaabu (1985), anaeleza kwamba, Ekegusii sawa na Kiswahili, ni mojawapo ya lugha za Kibantu. Anazidi kueleza kwamba lugha za Kibantu zina mfumo wa kisarufi unaokaribiana sana. Baadhi ya sifa za kiisimu juu ya lugha za Kibantu ni:

Mpangilio wa nomino katika ngeli.

Mnyambuliko wa vitenzi. Kitenzi kinaweza kunyambuliwa katika njia mbali mbali kama inavyodhihirishwa kwa ufupi hapa chini:

Aina ya jinsi	Ekegusii	Kiswahili
(i) jinsi ya kutendea	korugera	kupikia
(ii) jinsi ya kutendeka	korugeka	kupikika
(iii) jinsi ya kutendesha	korugia	kupikisha
(iv) jinsi ya kutendeana	korugerana	kupikiana

(c) Huwa na mfumo wa silabi-wazi kwa maana kwamba silabi ya neno lenye asili ya Kibantu huishia kwa vokali. Muundo huu hukosekana iwapo

konsonanti moja kati ya mbili zinazofuatana ni ya nasali.

(d) Huunganisha mofimu katika neno au sentensi ya neno moja (Uambishaji-Tamati kisarufi)

Kuna uwezekano wa kuunda nomino kutokana na vitenzi, kuunda vitenzi kutokana na nomino na pia kuunda nomino kutokana na vivumishi.

(e) Sentensi katika lugha hizi huwa na mpangilio maalumu wa maneno.

Sentensi huweza kugawanywa katika sehemu mbili zifuatazo:

(i) Kifungu nomino

(ii) Kifungu tenzi

Kwa hivyo kifungu tenzi (KT) huja baada ya kifungu Nomino (KN) yaani S→ KN + KT

Utafiti huu haushughulikii vitenzi na njeo kwa hivyo maelezo yaliyotolewa hapo juu yanathibisha tu kwamba Lugha ya Ekegusi ina mtindo sawa na lugha nyingi za Kibantu, Kiswahili kikiwa moja yao.

Licha ya ulinganifu uliofanywa hapo juu kwa kuzingatia vitenzi na minyambuliko ya vitenzi hivyo, kuna tofauti kadha wa kadha za kiisimu kati ya Ekegusii na Kiswahili sanifu tunapozingatia ngeli na vivumishi mbalimbali . Kwa maelezo ya Mbaabu (1985), utafiti huu utatumia mtindo wa kijadi wa utumiaji wa nambari wa uainishaji wa ngeli za Ekegusii.

(i) Ngeli za 1 na 2

Ngeli hizi huzingatia zaidi wanadamu

(i) a. Ngeli ya 1 - { o}

Ekegusii	Kiswahili	Ekegusii	Kiswahili
(i) omonto	mtu	(ii) omoana (omwana)	mtoto
(iii) omoiseke	msichana	(iv) omomura	mvulana
(v) omoremi	mkulima	(vi) omotugi	mfugaji

Inadhihirika hapa kwamba kiambishi cha Ekegusii {omo} ni sawa na kiambishi {m} katika Kiswahili ambapo huashiria ngeli ya 1. Hata hivyo

kunatokea tofauti katika nomino {omo-sae} ambapo katika Kiswahili neno kijana halianzi na kiambishi {m} na hapo mwanafunzi Mkisii anayejifundisha Kiswahili hukanganyika na huishia kuliingiza jina hilo katika mpangilio wa Ekegusii na kulitamka {m-kijana}. Nomino za Kiswahili ambazo huanza kwa kiambishi {Ki-}ambazo huleta utata kama huo ulioonyeshwa hapo juu ni pamoja na {kiongozi} na {kinyozi}, ambapo mwanafunzi Mkisii anaweza kutamka {muo-ngozi} au {mwo-ngozaji} na {m-nyoaji}.

(i) b. Ngeli ya 2 - { aβa}

Ngeli hii huwa ni wingi wa ngeli ya 1. Hivyo Nomino zote zilizoonyeshwa hapo juu hugeuka na kuannza kwa kiambishi [aβa] kama ifuatavyo:

Ekegusii	Kiswahili	Ekegusii	Kiswahili
(i) aβanto	watu	(ii) aβana	watoto
(iii) aβaiseke	wasichana	(iv) aβamura	wavulana
(v) aβaremi	wakulima	(vi) aβatugi	wafugaji

Pia inadhihirika hapa kwamba kiambishi cha Ekegusii {omo-}ambacho ni sawa na kiambishi {M-} katika Kiswahili ambapo huashiria ngeli ya 1 hubadilika na kuwa {aβa-} ambacho ni sawa na kiambishi {wa} kuashiria wingi wa ngeli ya 2. Tatizo lililojitokeza katika neno {omo-sae} ambalo kwa wingi ni {aβa-sae} linakuwa {vi}-jana katika Kiswahili badala ya kufuata mfumo wa Ekegusii ili liwe {wa-vijana}. Nomino Vijana haianzi na kiambishi {wa} na hapo mwanafunzi Mkisii anayejifunza Kiswahili hukanganyika na huishia kuliingiza neno hilo katika muundo wa Ekegusii na kulitamka {m-kijana}au {wa-vijana}. Nomino za Kiswahili ambazo huanza na kiambishi {vi-}ambazo huleta utata kama huo ulioonyeshwa hapo juu ni pamoja na{vi-ongozi} na {vi-nyozi}, ambapo mwanafunzi Mkisii anaweza kutamka {wa-ongozi} au {wa-ongozaji} na {wa-nyoaji}.

Kwa ufupi, ngeli za kwanza na pili zenye viambishi {omo – aβa} za Ekegusii ni sawa na viambishi {m - wa}katika Kiswahili ingawa kuna nomino chache za Kiswahili ambazo hazifuati muundo wa Ekegusii na hivyo kuwatatiza wanafunzi Wakisii wanaojifunza Kiswahili sanifu. Utata wa namna hii

(iii) Ngeli za 5 na 6

(iii) a. Ngeli ya 5 { e / oro }

Ngeli hii huhusisha majina yoyote yanayoanza na kiambishi{e} au {oro-} Majina haya yanaweza kuwa ni ya viungo vya mwili, wanyama, ndege, mimea, maumbile na vitu au vifaa mbali mbali

Ekegusii	Kiswahili	Ekegusii	Kiswahili
(i) embori	mbuzi	(ii) eng'ondi	kondoo
(iii) esese	mbwa	(iv) engoko	kuku
(v) endo	simba	(vi) engo	chui
(vii) enchoβo	ushanga	(viii) oroteru	pepeteo

(iii) b. Ngeli ya 6 { chi-}

Katika Ekegusii, ngeli {e- / oro } ni ya umoja ambayo hubadilika na kuwa {chi-} katika wingi kama ifuatavyo:

Ekegusii	Kiswahili	Ekegusii	Kiswahili
(i) chi-mbori	mbuzi	(ii) ching'ondi	kondoo
(iii) chisese	mbwa	(iv) chingoko	kuku
(v) chindo	simba	(vi) chingo	chui
(vii) chinchoβo	shanga	(viii) chinteru	pepeteo

Jambo linalojitokeza wazi kuhusu ngeli hii ni kwamba si Nomino zote za Ekegusii zinazofuata muundo sawa na zile za Kiswahili. Kwa mfano, majina mengi ya wanyama na ndege ambayo huwa katika ngeli ya Kiswahili ya (N -N) huwa katika ngeli ya {e- / oro- / chi- } ya Ekegusii. Katika mpangilio wa Ekegusii nomino katika ngeli huwa ni sawa ilmradi zianze kwa viambishi {e / oro-} katika hali ya umoja na {chi-} katika hali ya wingi. Mwanafunzi Mkisii hukanganyika na hulazimisha nomino hizo za Kiswahili kuwa na viambishi vya wingi kama ifutavyo:

(i) njia ... {ma-}njia (ii) kuku ... {ma-}kuku (iii) ndege ...{ ma-}ndege

Wanafunzi Wakisii hupata utata wa upatanisho wa kisarufi wanapotumia nomino zilizo katika ngeli hii wakati wanapozungumza au kuandika kwa Kiswahili sanifu. Mifano michache ifuatayo inadhihirisha utata huu:

Ekegusii	Upatanisho usiofaa	Upatanisho sahihi
umoja: eng'ombe ekanyenywa	ng'ombe ikachinjwa	ng'ombe alichinjwa
wingi: chiombe chikanyenywa	ng'ombe zikachinjwa	ng'ombe wakachinjwa

Tofauti kubwa inayodhihirika hapa ni kwamba nomino za Ekegusii zinazohusu binadamu haziwezi kutumiwa sawa katika upatanisho wa kisarufi. Katika Kiswahili nomino za bianadamu, wanyama, ndege na wadudu hutumiwa katika ngeli sawa. Tofauti hii humfanya mwanafunzi Mkisii kufanya makosa katika upanisho wa kisarufi na hatimaye kuathiri matokeo yake katika mtihani wa Kiswahili.

(iv) Ngeli za 7 na 8 { ege, eke - eβi }

Ngeli za 7 na 8 za Ekegusii huhusisha nomino za wanyama, wadudu, mimea, viungo vya mwili na maumbile ilmradi nomino hizo huanza kwa mofimu {ege-, eke- na e-} katika hali ya umoja na {eβi} katika hali ya wingi.

(iv) a. Ngeli ya 7 { ege-, eke- na e }.

Nomino katika ngeli hii huwa ni katika umoja na kulingana na mfumo wa Ekegusii huwa zinaanza na mofimu {ege-, eke- au e-} kama ifuatavyo:

Ekegusii	Kiswahili	Ekegusii	Kiswahili
(i) egento	kitu	(ii) egetaβu	kitabu
(iii) egesieri	mlango	(iv) egensinsi	sisimizi
(v) egetera	jaa la taka	(vi) egesimba	cheche
(vii) egesusu	sungura	(viii) egechure	paa (mnyama)
(ix) egesare	kunde	(x) egetugi	kisiki

(iv) b. Ngeli ya 8 – { eβi }

Nomino zilizoonyeshwa hapo juu katika hali ya umoja hubadilika na kuanza kwa kiambishi [eβi-], kuashiria hali ya wingi kama ifuatavyo:

Ekegusii	Kiswahili	Ekegusii	Kiswahili
(i) eβinto	vitu	(ii) eβitaβu	vitabu
(iii) eβisieri	milango	(iv) eβisinsi	sisimizi
(v) eβitera	mashimo	(vi) eβisimba	cheche
(vii) eβisusu	sungura	(viii) eβichure	paa (mnyama)
(ix) eβisare	kunde	(x) eβitugi	visiki

Ngeli za Ekegusii za{ege-, eke-} na {eβi } ni sawa na za Kiswahili za (Ki - Vi). Katika ngeli hii wanafunzi Wakisii hupata utata wanapotumia nomino za binadam, wanyama, ndege na wadudu. Kuambatana na muundo wa Ekegusii nomino zote zinazoanza na viambishi {Ki – Vi}huendelezwa katika upatanisho wa lugha kwa kutumia viambishi hivyo hivyo bila kuzingatia nomino za binadamu, wanyama, ndege na wadudu. Mifano ifuatayo inadhihirisha utata huu.

Ekegusii	upatanisho usio sahihi	Upatanisho sahihi
(i) Ekegwankwa giakure	kipepeo kimekufa	kipepeo amekufa
(ii) Ekerema kiararire	kilema kimelala	kilema amelala
(ii) Enguβo yasaoire roche	kiboko kimeingia mtoni	kiboko ameingia mtoni

Kwa kufuata muundo wa lugha ya Ekegusii wa ngeli ya {ege-, eke - eβi } mwanafunzi Mkisii huendeleza kimakosa nomino za binadamu, wanyama, ndege na wadudu zenye viambishi vya (Ki – Vi) katika Kiswahili. Makosa haya ya upatanisho wa kisarufi wa Kiswahili huchangia matokeo mabaya ya mtihani wa Kiswahili.

(v) Ngeli za 9 na 10 { e – e }

Ngeli hii katika Ekegusii huwa na majina ya vitu visivyohesabika kwa urahisi na Nomino hizi hazibadiliki katika wingi. Ngeli hii ni sawa na ile ya (N -N) ya Kiswahili. Mifano;

Ekegusii	Kiswahili	Ekegusii	Kiswahili
(i) etuki	nywele	(ii) erongori	uji

(iii) egesunte	giza	(iv) rimisu	harufu
(v) erioβa	mawingu	(vi) amara	utumbo
(vii) amasinyoro	mkojo	(viii) amaβere	maziwa

(vi) Ngeli za 11 na 12 { ri, eri, oko- – ama }

(vi) a. Ngeli ya 11 { ri / eri }

Nyingi ya Nomino za ngeli hii huanza kwa {ri-} au {eri-} katika hali ya umoja. Nomino hizi huwa na majina ya matunda,viungo vya mwili, majina ya sifa au hali ya ukubwa.

Ekegusii	Kiswahili	Ekegusii	Kiswahili
(i) eriogi	kelele	(ii) eriogo	dawa
(iii) eriso	jicho	(iv) erino	jino
(v) erieta	jina	(vi) eriβi	jizi
(vii) riaki	hongo	(viii) ribaga	nafasi
(ix) okogoro	mguu	(x) okoβoko	mkono

(vi) b. Ngeli ya 12 { ama-}

Nomino za ngeli (vi)a.. ziko katika hali ya umoja. Katika wingi Nomino hizi hubadilisha viambishi awali kwa kutupilia mbali {e- au ri-} na kuchukua {ama-}kama kiambishi awali kama inavyodhihirishwa hapa chini:

Ekegusii	Kiswahili	Ekegusii	Kiswahili
(i) amariogi	kelele	(ii) amariogo	dawa
(iii) amaiso	macho	(iv) amaino	meno
(v) amarieta	majina	(vi) amaiβi	majizi
(vii) amaaki	hongo	(viii) amaβaga	nafasi
(ix) amagoro	miguu	(x) amaβoko	mikono

(vii) Ngeli za 13 na 14 { aka -, aga - eβi }

Ngeli hii huonyesha hali ya chini, udogo, uchache au dharau. Ni ngeli maarufu sana miongoni mwa jamii ya Wakisii na wanafunzi hukanganyika na kuilazimisha katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

(vii) a. Ngeli ya 13 { aka -, aga}

Ngeli hii huwa na Nomino {majina} yenye kiambishi awali {aka- au aga-}

Ekegusii	Kiswahili	Ekegusii	Kiswahili
(i) aka-nyomba	kijumba	aka-mwana	ki-ji-toto
(ii) aka-nyoni	ki-ji-dege (kidege)	aka-nda	ki-ji-tumbo
(v) aga-iseke	ki-ji-sichana	aga-ke	kidogo

(vii) b. Ngeli ya 14 { eβi-}

Nomino za majina ya ngeli ya 13 zinapowekwa kwenye ngeli ya 14 huwa na kiambishi cha (eβi-) kama ifuatavyo:

Ekegusii	Kiswahili	Ekegusii	Kiswahili
(i) eβi-nyomba	vi-jumba	(ii) eβi-mwana	vi-jitoto
(iii) eβi-nyoni	vi-ji-dege (kidege)	(iv) eβi-nda	vi-ji-tumbo
(v) eβi-iseke	vi-ji-sichana	(vi) eβi-ke	vidogo
(vii) eβi-nto	vi-jitu	(viii) eβi-nchera	vijia

Utata unaojitokeza katika ngeli hizi ni kwamba wanafunzi huilazimisha katika Kiswahili na hivyo kufanya makosa ya kisarufi. Makosa wanayoyafanya ni kutumia viambishi –awali {ka}na {eβi} kuonyesha udogo au uchache wa binadamu, wanyama, ndege wadudu na vitu mbalimbali. Ifuatayo ni mifano ya makosa hayo:

Ekegusii	makosa ya upatanisho	upatanisho sahihi
(i) aka-nyomba ka-ne	ka-nyumba ka-ngu	ki-jumba changu
(ii) aka-ino ka-βunekire	ka-meno ka-mevunjika	ki-jino kimevunjika
(iii) aga-taβu ka-ino	ka-tabu ke-nu	ki-ji-tabu chenu

(viii) Ngeli ya 15 {oβo-au oβwe- au oβwa- au oβwo-}

Katika Ekegusii ngeli hii huonyesha sifa,vitenzi na vitu visivyohesabika yaani vitu vya kidhahania. Mifano ni kama ifuatayo:

Ekegusii	Kiswahili	Ekegusii	Kiswahili
oβorai	uongozi	oβuya	wema/uzuri
oβoremereria	uvumilivu	oβoitongo	ustaraabu

oβwerori	maringo	oβuenenu	kiburi
oβochai	dharau	oβwa-nchani	upendo

Kutokana na mifano iliyoonyeshwa hapo juu ngeli hii ni sawa na ya Kiswahili ambayo nomino zake huanza na kiambishi {u} katika hali za umoja na wingi. Wanafunzi Wakisii hawapati utata wowote katika upatanisho kwa sababu zinashabihiana.

3.2.2 Upatanisho wa Nomino - Kivumishi

3.2.2.1 Vivumishi vimilikishi. (Umoja)

	Ngeli	Nomino	V i m i l i k i s h i					
Gus.			-ne	-ito	-o	-ino	-ye	-βo
Kis.			-angu	-etu	-ako	-enu	-ake	-ao
Gus.	omo-	omwana	one	oito	oo	oino	oye	oβo
Kis.	m-	mtoto	wangu	wetu	wako	wenu	wake	wao
Gus.	omo-	omotwe	one	oito	oo	oino	oye	oβo
Kis.	ki-	kichwa	changu	chetu	chao	chenu	chake	chao
Gus.	e-	embori	ya ne	yaito	yao	yaino	yaye	yaβo
Kis.	N-N	mbuzi	wangu	wetu	wao	wenu	wake	wao
Gus.	e-	ekerogo	kiane	giaito	kiao	kiaino	kiaye	kiaβo
Kis.	ki-	kiti	changu	chetu	chako	chenu	chake	chao
Gus.	e-	etuki	yane	yaito	yao	yaino	yaye	yaβo
Kis.	N-N	nywele	yangu	yetu	yako	yenu	yake	yao

3.2.2.2. Vivumishi vimilikishi. (Wingi)

	Ngeli	Nomino	V i m i l i k i s h i					
Gus.			-ne	-ito	-o	-ino	-ye	-βo
Kis.			-angu	-etu	-ako	-enu	-ake	-ao
Gus.	aβa-	aβa-ana	βa-ane	βa-ito	βa-ao	βa-ino	βa-aye	βa-bo
Kis.	wa-	watoto	wangu	wetu	wako	Wenu	wake	wao

Gus.	eme-	emetwe	yaane	yaito	yaao	Yaino	yaye	yaβo
Kis.	vi-	vichwa	vyangu	vyetu	vyao	Vyenu	vyake	vyao
Gus.	chi-	chimbori	chiane	chiaito	chiao	Chiaino	chiaye	chiaβo
Kis.	i	mbuzi	wangu	wetu	wao	Wenu	wake	wao
Gus.	eβi-	eβi-rogo	βi-ane	βiaito	βi-ao	βi-aino	βi-aye	βi-aβo
Kis.	i	viti	vyangu	vyetu	vyako	Vyenu	vyake	vyao
Gus.	e-	etuki	yane	yaito	yao	Yaino	yaye	yaβo
Kis.		nywele	yangu	yetu	yako	Yenu	yake	yao

N/B. Gus – Ekegusii Kis. - Kiswahili

Katika muundo wa Ekegusii vivimishi- vimilikishi vinavyohusu binadamu hubadilika kutoka hali ya umoja hadi wingi ilhali katika Kiswahili vivumishi hivyo havibadiliki. Huwa ni sawa katika hali ya umoja na wingi pia.

Ekegusii	Kiswahili sanifu
1. omwana one	mtoto wangu
2. omochokoro one	mjukuu wangu
3. omosacha one	mme wangu
4. omogeni one	mgeni wangu

Kulingana na mfumo wa lugha ya Ekegusii, kivumishi kimilikishi {o-} hubadilika na kuwa {ba-} ilhali katika Kiswahili kivumishi kimilikishi huwa sawa katika hali za umoja {wa-}na wingi (wa-) kama inavyodhihirishwa katika mifano ifuatayo katika hali ya wingi.

Ekegusii	Kiswahili
1. aβana βa-ane	watoto wangu
2. aβachokoro βa-ane	wajukuu wangu
3. aβasacha β-ane	waume wangu
4. aβageni βa-ane	wageni wangu

Maelezo yaliyotolewa yanadhihirisha kwamba katika mfumo wa Ekegusii vivumishi- vimilikishi huwa vinatofatiana katika hali ya umoja na wingi wakati nomino zinazotumiwa ni za binadamu. Imedhihirika pia kuwa katika mfumo wa Kiswahili vivumishi vimilikishi hubakia sawa wakati nomino za binadamu,

wanyama, ndege na wadudu zinapotumiwa. Kutobadilika kwa vivumishi - vimilikishi wakati wa kutumia nomino za binadamu,wanyama, ndege na wadudu katika Kiswahili, huwatatiza wanafunzi Wakisii ambao kulingana na mfumo wa lugha yao ni lazima vivumishi hivyo vibadilike katika hali ya wingi.

Kutokana na utata wanaoupata, wanafunzi Wakisii hutumia vivumishi-vimilikishi visivyo vya ngeli ya {M-Wa} na hivyo kufanya makosa ambayo huathiri matokeo yao ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili. Mifano ifuatayo inadhihirisha matumizi ya vivumishi vimilikishi kimakosa:

Ekegusii	matumizi yasiyosahihi ya vivumishi vimilikishi	Kiswahili sanifu
(i) eng'ombe ya-ane	ng'ombe y-angu	ng'ombe w-angu
(ii) esese ya-ito	mbwa y-etu	mbwa w-etu
(iii) embori ya-o	mbuzi y-ako	mbuzi w-ako
(iv) etigere ya-ino	punda y-enu	punda w-enu
(v) eng'ondi ya-ye	kondoo y-ake	kondoo w-ake
(vi) engamia ya-bo	ngamia y-ao	ngamia w-ao

Makosa haya hujitokeza wakati wa matumizi ya nomino za wanyama, ndege na wadudu. Katika mfumo wa Ekegusii vivumishi- vimilikishi vinavyohusu binadamu havifanani na vile vinavyohusu wanyama, ndege na wadudu kama ilivyo katika Kiswahili. Mifano ifuatayo inathibitisha hali hii.

Ekegusii		athari za Ekegusii	Kiswahili sanifu
Umoja:	omwana o-ne	mtoto y-angu	mtoto w-angu
Wingi:	aβana βa-ane	watoto y-angu	watoto w-angu
Umoja:	eng'ombe ya-ane	ng'ombe y-angu	ng'ombe w-angu
Wingi:	chiombe chi-ane	ng'ombe z-angu	ng'ombe w-angu
Umoja:	engoko ya-ane	kuku y-angu	kuku w-angu
Wingi:	chingoko chi-ane	kuku z-angu	kuku w-angu
Umoja:	enchoke ya-ane	nyuki y-angu	nyuki w-angu
Wingi:	chinchoke chi-ane	nyuki z-angu	nyuki w-angu

Pia wanafunzi Wakisii hutatizika wakati wa kutumia vivumishi vimilikishi katika nomino za baadhi ya wanyama, ndege na wadudu walio katika ngeli ya Ekegusii ya {ri – ama} kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

	Ekegusii	athari za Ekegusii	Kiswahili sanifu
Umoja:	rikorominyo ri-ane	konokono l-angu / y-angu	konokono w-angu
Wingi:	amakorominyo a-ane	(ma) konokono (y-a) z-angu	konokono w-angu
Umoja:	riruma ri-ane	njiwa langu / yangu	njiwa wangu
Wingi:	amaruma a-ane	njiwa zangu	njiwa wangu
Umoja:	ritimbo ri-ane	duduvule langu	duduvule wangu
Wingi:	amatimbo a-ane	duvule (za) yangu	duduvule wangu

3.2.2.3 Vivumishi vya sifa

Ngeli	Kiambishi -awali	Jina	Sifa	Vivumishi
Gus.	omo-	omo-nto	o-βuya, oβo-tambe	omu-ya; omo-tambe
Kis.	m-	m-tu	u-zuri, u-refu	m-zuri; m-refu
Gus.	aβa-	aβa-nto	o-βuya, oβo-tambe	aβa-ya; aβa-tambe
Kis.	wa-	wa-tu	u-zuri, u-refu	wa-zuri; wa-refu
Gus.	e-	e-sese	o-βuya, oβo-tambe	engi-ya; en-tambe
Kis.		mbwa	u-zuri, u-refu	m-zuri; m-refu
Gus.	chi-	chi-sese	o-βuya, oβo-tambe	chingi-ya; chin-tambe
Kis.		mbwa	u-zuri, u-refu	wa-zuri; warefu
Gus.	omo-	omo-gongo	o-βuya, oβo-tambe	omu-ya; omo-tambe
Kis.i	m-	m-gongo	u-zuri, u-refu	m-zuri; m-refu
Gus.	eme-	eme-gongo	o-βuya, oβo-tambe	emi-ya; eme-tambe
Kis.	mi	mi-gongo	u-zuri, u-refu	mi-zuri: mi-refu
Gus.	ege- / eke-	ege-nto / ekerogo	o-βuya, oβo-tambe	eki-ya; ege-tambe " "
Kis.	ki-	ki-tu	U-zuri, U-refu	ki-zuri: ki-refu

		ki-ti		
Gus.	eβi-	ebi-nto eβirogo	o-βuya, oβo-tambe	eβi-ya; eβi-tambe " "
Kis.	vi-	vi-tu vi-ti	U-zuri, U-refu	vi-zuri; virefu

Gus. – Ekegusii Kis. – Kiswahili

Kama ilivyodhihirika katika matumizi ya vivumishi-vimilikishi, wanafunzi Wakisii hukanganyika wakati wanapotumia vivumishi vya sifa na nomino za wanadamu,wanyama, ndege na wadudu. Kuambatana na mfumo wa Ekegusii nomino za binadamu haziwezi kutumiwa sawa na za wanyama, ndege na wadudu.

Hali hii ya kutotumia nonimo za wanyama, ndege na wadudu hutokea kwa sababu majina yao hayaanzi kwa mofimu {o} katika umoja au {aβa-} katika wingi. Mifano ifuatayo inaonyesha makosa yanayofanywa na wanafunzi Wakisii wanapotumia vivumishi vya sifa katika hali ya umoja:

Ekegusii	Makosa katika matumizi ya vivumishi vya sifa	Kiswahili sanifu
(i) eng'ombe e-ngiya (ii) esese e-netu	ng'ombe n-zuri mbwa nene	ng'ombe m-zuri mbwa m-nene
(iii) engoko e-nke (iv) embuni en-tambe	kuku n-dogo mbuni ndefu	kuku m-dogo mbuni m-refu
(v) enchoke en-dabu (vi) enda e-mwamu	nyuki ny-eupe chawa ny-eusi	nyuki mw-eupe chawa mw-eusi

Mifano ifuatayo inaonyesha makosa yanayofanywa na wanafunzi Wakisii wanapotumia vivumishi vya sifa katika hali ya wingi.

Ekegusii	Makosa katika matumizi ya vivumishi vya sifa	Kiswahili sanifu
(i) chiombe chi-ngiya (ii) chisese chi-netu	ng'ombe n-zuri mbwa nene	ng'ombe wa-zuri mbwa wa-nene
(iii) chingoko chi-nke	kuku n-dogo	kuku wa-dogo

(iv) chimbuni chin-tambe	mbuni ndefu	mbuni wa-refu
(v) chinchoke chi-ndabu (vi) chinda chi-mwamu	nyuki ny-eupe chawa ny-eusi	nyuki w-eupe chawa w-eusi

Kadhalika wanafunzi Wakisii hufanya makosa wanapotumia vivumishi vya sifa na nominao za majina yaliyo katika ngeli za Ekegusii za {ri – ama-} kama ifuatavyo;-

Ekegusii	athari za Ekegusii	Kiswahili sanifu
Umoja: rikorominyo ri-nene Wingi: amakorominyo ama-nene	konokono kubwa (ma) konokono ma-kubwa	konokono m-kubwa konokono wa-kubwa
Umoja: rikoru ri-rabu Wingi: amakoru ama-rabu	kunguru nyeupe kunguru ny-eupe	kunguru mw-eupe kunguru w-eupe
Umoja: ritimbo ri-bariri Wingi: amatimbo amabariri	duduvule lekunde duduvule mekundu	duduvule mw-ekundu duduvule w-ekundu

3.2.2.4 Vivumishi vya {-enye} na {-enyewe}

Katika mpangilio wa Ekegusii huwa hakuna tofauti kati ya mwenye na mwenyewe.

Ekegusii	Kiswahili
omo-nyene	mw-enye (umoja)
aβa-nyene	w-enye (wingi)

Mifano ifuatayo inaonyesha kutokuwepo kwa tofauti katika Ekegusii kati ya {mwenye} na {mwenywe} katika hali ya umoja na wingi.

	Ekegusii	Kiswahili sanifu
Umoja:	(i) mwana omo-nyene enyomba (ii) omwana omo-nyene	mtoto mw-enye nyumba mtoto mw-enyewe
Wingi:	(i) aβana aβa-nyene chi-nyomba (ii) βana aβa-nyene	watoto w-enye nyumba watoto w-enyewe

Wakati wanafunzi Wakisii wanapotumia vivumishi vya {–enye} na {– enyewe}hutatizika sana wanapovitumia na nomino za wanyama, ndege na wadudu. Utata huu hujitokeza kwa sababu kulingana na mfumo wa Ekegusii

hapana uwezekano wa nonino za binadamu kutumia vivumishi sawa na vya wanyama, ndege na wadudu. Ifuatayo ni mifano kwa kuzingatia kivumishi {-enye}

	Ekegusii	Athari za Ekegusii	Kiswahili sanifu
Umoja Wingi	eng'ombe e-nyene emori chiombe chi-nyene chi-mori	ng'ombe y-enye ng'ombe z-enye …	ng'ombe mw-enye… ng'ombe w-enye
Umoja Wingi	engoko e-nyene ebichuchu chingoko chi-nyene	kuku y-enye vifaranga kuku z-enye	kuku mw-enye.. kuku w-enye ..
Umoja Wingi	enchoke e- nyene oβoke Chinchoke chi-nyene ..	nyuki y-enye asali nyuki z-enye	nyuki mw-enye .. nyuki w-enye ..

Mifano kwa kutumia kivumishi –enyewe.

	Ekegusii	Athari za Ekegusii	Kiswahili sanifu
Umoja:	eng'ombe e-nyene	ng'ombe y-enyewe	ng'ombe mw-enyewe
Wingi:	chiombe chi-nyene	ng'ombe z-enyewe	ng'ombe w-enyewe
Umoja:	engoko e-nyene	kuku y-enyewe	kuku mw-enyewe
Wingi:	chingoko chi-nyene	kuku z-enyewe	kuku w-enyewe
Umoja:	enchoke e- nyene	nyuki y-enyewe	nyuki mw-enyewe
Wingi:	chinchoke chi-nyene	nyuki z-enyewe	nyuki w-enyewe

Utata mwingine huwakumba wanafunzi Wakisii wanapotumia vivumishi –{enye} na {–enyewe} na nomino za majina yaliyo katika ngeli za ekegusii za {ri – ama } kama inavyoonyeshwa katika mifano ifuatayo kwa kuzingatia kivumishi {–enye}.

	Ekegusii	athari za Ekegusii	Kiswahili sanifu
Umoja:	riruβi ri-nyene	nyoka sumu y-enye	nyoka mw-enye…
Wingi:	ama-ruβi ama-nyene	nyoka sumu z-enye	nyoka w-enye…

3.2.2.5 { -ote / -o-ote}.

Vivumishi hivi vya Kiswahili hutumika tofauti katika muundo wa Ekegusii kama inavyoonyeshwa katika mifano ifuatayo:-

Ngeli	Kiambishi-awali	Jina	-ote
Ekegu-sii	omo-	omonto	βw-ensi
Kiswahili	m-	m-tu	w-ote
Ekegu-sii	aβa-	aβaremi	β-onsi
Kiswahili	wa-	wakulima	w-ote
Ekegu-sii	omo-	omo-te	βw-onsi
Kiswahili	m-	m-ti	w-ote
Ekegusii	eme-	eme-te	y-onsi
Kiswahili	mi-	mi-ti	y-ote
Ekegusii	e-	e-nyomba	y-onsi
Kiswahili	N-N	nyumba	y-ote
Ekegu-sii	chi-	chi-nyomba	chi-onsi
Kiswahili	N-N	nyumba	z-ote
Ekegu-sii	ri-	ri-gena	ri-onsi
Kiswahili	ji-	jiwe	l-ote
Ekegu-sii	ama-	ama-gena	o-nsi
Kiswahili	ma-	ma-we	y-ote

Katika lugha ya Kiswahili kivumishi {–ote }hutumika kuonyesha utimilifu wa kitu au jambo fulani. Pia kivumishi hiki kikirudiwa huonyesha kutozingatiwa kwa umaalumu wa kitu au jambo fulani. Katika mfumo wa lugha ya Ekegusii kivumishi {–onsi} hutumiwa sawa na kivumishi cha Kiswahili {–ote}. Tofauti iliyopo katika matumizi ya vivumishi hivi ni kwamba katika Ekegusii kivumishi {–onsi} hakirudiwi ili kuonyesha kutozingatiwa umaalum wa

kitu au jambo fulani. Hoja hii inadhihirishwa wazi katika mifano ifuatayo:-

	Umoja	Wingi
Ekegusii:	omonto βwe-nsi	aβanto βo-nsi
Kiswahili:	mtu w-ote	watu w-ote
Ekegusii:	omote βwe-nsi	emete yo-nsi
Kiswahili:	mti w-ote	miti y-ote
Ekegusii:	egetanda gio-nsi	eβitanda βio-nsi
Kiswahili:	kitanda ch-ote	vitanda vy-ote
Ekegusii:	erino rio-nsi	amaino o-nsi
Kiswahili:	jino l-ote	meno y-ote
Ekegusii	enyomba yo-nsi	chinyomba chio-nsi
Kiswahili	nyumba y-ote	nyumba z-ote

Kulingana na mfumo wa Kiswahili mifano yote iliyotolewa hapo juu inaweza kuwekwa katika hali ya kutozingatia umaalum (inavyoonyeshwa katika mifano ifuatayo) ilhali jambo hili halikubaliki katika mfumo wa Ekegusii.

	Umoja	Wingi
i.	mtu yey-ote	watu w-ow-ote
ii.	mti w-ow-ote	miti y-oy-ote
iii.	kitanda ch-o-ch-ote	vitanda vy-o-vy-ote
iv.	jino l-o-l-ote	meno y-o-y-ote
v.	nyumba y-o-y-ote	nyumba z-o-z-ote

Katika muundo wa Ekegusii kivumishi {– nde} huwekwa kabla ya {–nsi} ili kuonyesha kutozingatia umaalum wa kitu au jambo fulani kama inavyodhihirishwa kwenye mifano ifuatayo:-

	Umoja	Wingi
i.	omonto o-nde βwe-nsi	aβanto ba-nde βo-nsi
ii.	omote o-nde βwe-nsi	emete e-nde yo-nsi
iii.	egetanda ke-nde gio-nsi	eβitanda βi-nde βio-nsi
iv.	erino ri-nde rio-nsi	amaino a-nde o-nsi
v.	enyomba e-nde yo-nsi	chinyomba chi-nde chio-nsi

Kutokana na mifano iliyoonyeshwa hapo juu wanafunzi Wakisii hutatizika wanapotumia vivumishi {–ote} na {-o-ote} wakati wanapotumia majina ya wanyama, wadudu na ndege kama inavyoonyeshwa katika mifano ifuatayo:-

Makosa yanayotokana na athari za Ekegusii katika Kiswahili (Umoja)	Kiswahili Sanifu
(i) mtu yoyote (wowote)	mtu yey-ote
(ii) mti yoyote	mti w-ow-ote
(iii) kitanda yoyote	kitanda ch-o-ch-ote
(iv) jino yoyote	jino l-o-l-ote

Katika mifano iliyoonyeshwa hapo juu inadhihirika wazi kwamba kwa kuzingatia muundo wa Ekegusii, kivumishi {y-o-y-ote} hutumiwa katika ngeli zote za Kiswahili na wanafunzi wanafuata muundo huu hufanya makosa ya kisarufi. Makosa haya hudhihirika zaidi wakati majina ya wanyama, wadudu na ndege yanatumika. Mifano ifuatayo inabainisha makosa hayo.

	Makosa katika Kiswahili	Kiswahili Sanifu
i.	mbuzi yoyote (wowote)	mbuzi yeyote
ii.	paka yoyote (wowote)	paka yeyote
iii.	kipepeo yoyote (wowote)	kipepeo yeyote
iv.	kereng'ende yoyote (wowote)	kereng'ende yeyote
v.	bata yoyote (wowote)	bata yeyote

Makosa yaliyoonyeshwa hapo juu katika hali ya umoja hujitokeza pia katika hali ya wingi:

	Makosa katika Kiswahili	Kiswahili Sanifu
i.	mbuzi yoyote (zozote)	mbuzi wowote
ii.	paka yoyote (zozote)	paka wowote
iii.	vipepeo yoyote (zozote)	kipepeo wowote
iv.	kereng'ende yoyote (zozote)	kereng'ende wowote
v.	bata yoyote (zozote)	bata wowote

3.2.2.6. Vivumishi vya { -a }unganifu

Ekegusii hutumia vivumishi-unganishi ambavyo ni tofauti na vile vinavyotumiwa katika Kiswahili. Wanafunzi Wakisii hupata utata wanapotumia vivumishi-unganishi vya Kiswahili kwani hufuata muundo wa Ekegusii na hivyo kufanya makosa ya kisarufi.

Ngeli	Kiambishi	Nomino	kivumishi - unganifu	Nomino
Ekegu-sii.	omo-	omo-ana (omwana); omorugi	βwo-	omoremi
Kiswahili	m-	m-toto; mke	w-a	mkulima
Ekegu-sii.	aβa-	aβana; aβarugi	βo- βa	omoremi aβaremi
Kiswahili	wa-	wa-toto wa-ke	w-a	mkulima wakulima
	Umoja		wingi	
Ekegusii Kiswahili	(i). omwana βw-o mwarimu (ii) mtoto w-a mwalimu		aβana βa 'βaarimu watoto w-a walimu	
Ekegusii Kiswahili	(iii) omote βw-e 'nyomba (iv) mti w-a nyumba		emete y-e chinyomba miti y-a nyumba	
Ekegusii Kiswahili	(v) ekiara ki' omwana (vi) kidole ch-a mtoto		eβiara βi' omwana vidole vy-a watoto	
Ekegusii Kiswahili	(vii) eriso ri' embori (viii) jicho l-a mbuzi		amaiso y- e chimbori macho y-a mbuzi	
Ekegusii Kiswahili	(ix) enyimbo y- omouko (x) fimbo y-a kipofu		chinyimbo ch-i emeuko fimbo z-a vipofu	
Ekegusii Kiswahili	(xi) okorara gw- enchogu, kulala kw-a ndovu ..		okorara gw-e chinchogu kulala kw-a ndovu	

Ekegusii Kiswahili	ensemo y-emeremo mahali p-a kazi	Chinsemo ch-i emeremo Mahali p-a kazi
Ekegusii Kiswahili	ase enyomba y-a tata nyumbani mw-a baba	ase chinyomba ch-ia tata nyumbani mw-a baba

Katika ngeli ya {M-Wa } matumizi ya a- unganifu huwa sawa katika hali ya umoja na hali ya wingi, yaani {W-a - W-a.} Katika muundo wa Ekegusii { bw'o} huwa ni kiunganishi katika hali ya umoja na { b'o) huwa ni kiunganishi katika hali ya wingi. hivyo, wanafunzi Wakisii hukanganyika na kutumia { a-}unganifu ya ngeli zingine katika ngeli ya {M-Wa} na hivyo kufanya makosa ya kisarufi kama vile {mtoto ya}, {mkono ya} na {mti ya}

Aidha wanafunzi hawa hufanya makosa sawa na haya katika ngeli zingine kama vile {Ji –Ma} kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

	Matumizi yasiyofaa ya kiunganishi –a	Matumizi sahihi
(i)	eneo y-a…	eneo l-a
(ii)	umbo ya…	tumbo l-a
(iii)	shimo ya …	shimo l-a
(iv)	mahali ya.....	mahali p-a

3.2.2.7 Upatanisho wa Nomino- Tarakimu

Katika Ekegusii ni tarakimu mbili tu, 9 na 10 kati ya tarakimu kumi, ambazo hazichukui viambishi vya nomino kama inavyoonyshwa katika mifano ifuatayo:

Ekegusii	Kiswahili	Ekegusii	Kiswahili
eyemo	moja	ibere	mbili
isato	tatu	inye	nne
isano	tano	isano nemo (tano na moja)	sita
isano na ibere	(tano na mbili) saba	isano na isato (tano na tatu)	nane
kianda	tisa (kenda)	ikomi	kumi

Upatanisho wa nomino - tarakimu

	Ngeli	nomino	Upatanisho
Ekegu-sii.	Omo-	omoremi	Omoremi oyomo
Kiswahili	m-	mkulima	mkulima mmoja
Ekegusii	aβa-	abaremi	aβa-remi βaβere, (βatato, βane, βatano, βatano nomo, βatano na βaβere, βatano na βatato, kianda, ikomi)
Kiswahili	wa-	wa-kulima	wawili,watatu, wanne,watano, sita, saba, wanane, tisa, kumi
Ekegusii	e-	e-mbori	embori eyemo
Kiswahili		mbuzi	mbuzi mmoja
Ekegusii.	chi-	chi-mbori	chi-mbori ibere, isato, inye, isano, isano n'emo, isano na ibere,isano na isato, kianda, ikumi.
Kiswahili		mbuzi	mbuzi wawili, watatu, wanne, watano. sita, saba, wanane, tisa, kumi.
Ekegusii	ege- / eke	egechure ekenanda	egechure ekemo ekenanda ekemo
Kiswahili	ki-	ki-ti ki-nanda	kiti kimoja kinanda kimoja
Ekegusii	eβi-	eβichure eβinanda	eβichure/eβinanda βiβere, βitato, βine, βitanoβitano na kemo, βitano na βibere βitano na βitato, kianda, ikomi.
Kiswahili		paa (mnyama) vi-nanda	*paa mmoja, wawili, watatu, wanne, watano.sita, saba, wanane, tisa, kumi. / vinanda viwili, vitatu,vinne, vitano,sita, saba,vinane,tisa, kumi.
Ekegusii	omo-	omo-te/ omo-twe / omo-gongo	omo-te / omo-twe / omo-gongo oyomo

Kiswahili	m-, ki-	m-ti / kichwa / m-gongo	m-ti mmoja / kichwa kimoja / mgongo mmoja
Ekegusii	eme-	eme-gongo eme-te / eme-twe	eme-te/ emetwe / emegongo eβere, etato, ene, etano, etano nomo, etano neβere, etano ne tato, kianda, ikomi.
Kiswahili	mi- vi-	mi-gongo/ miti vichwa	miwili,mitatu,minne, mitano, minane. viwili,vitatu,vinne,vitano, vinane

Wanafunzi Wakisii hupata matatizo ya upatanisho wa nomino na tarakimu katika Kiswahili kwa sababu ya tofauti za upatanisho zilizoko baina ya Ekegusii na Kiswahili wakati wa kutumia tarakimu. Wanafunzi hawa hufanya makosa ya kisarufi hasa katika ngeli ya {M-Wa} ambapo, kulingana na muundo wa Ekegusii, nonino za wanyama, ndege na wadudu hazikubaliki kwenda sambamba na za binadamu katika hesabu. Hivyo, wanafunzi Wakisii hufanya makosa kama yafuatayo:

(Ng'ombe, simba, kuku, njiwa, mbu, chawa) moja, mbili, tatu, nne, tano, nane

Kulingana na mfumo wa Ekegusii viambishi-awali huwekwa katika tarakimu zote ila tisa na kumi. Mfumo wa Kiswahili hauna viambishi -awali katika tarakimu za sita, saba, tisa na kumi. Wanafunzi Wakisii huweka viambishi -wali katika nomino za tarakimu za sita na saba katika hali ya wingi na hivyo kufanya makosa yafuatayo ya kisarufi:

(watu, watoto, wakulima) wasita, wasaba.

(miti, mikono, migongo, mikuki,) misita, misaba.

(viti, vikombe, visima, vidole) visita, visaba.

(meno, mafiga, maneno, mafungu) masita, masaba.

SURA YA NNE

4.0 Makosa katika mazungumzo

4.1. Utangulizi.

Katika sura hii, makosa mbali mbali ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi Wakisii wakati wa mijadala yanajadiliwa. Lengo la mijadala lilikuwa kuwapa fursa wanafunzi waliohusika kutoa mawazo yao katika mazungumzo ndipo ibainishwe baadaye kama wangefanya makosa fulani. Mazungumzo ya wanafunzi mia moja arobaini na sita yalinaswa. Wanafunzi hao walitoka shule kumi na tano. Wanafunzi kumi walitoka shule kumi na nne na wanafunzi sita walitoka shule moja. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa (NUM),ilitumiwa ili kubaini na kuainisha makosa yaliyojitokeza. Matokeo yalikuwa kwamba wanafunzi walifanya makosa katika upatanisho wa kisarufi hasa kwa kutozingatia ngeli, vivumishi mbalimbali, virejeshi na viunganishi.

4.1.1 Makosa ya upatanisho wa kisarufi kuzingatia ngeli

Kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, mtafiti aliyaorodhesha makosa yaliyojitokeza ya upatanisho wa kisarufi kwa kuzingatia ngeli. Miundo ya ngeli za Ekegusii na Kiswahili ililinganishwa. Kama ilivyokuwa imebashiriwa katika sura ya tatu,wanafunzi Wakisii walizingatia muundo wa ngeli wa Ekegusii na hivyo kuathiri muundo wa ngeli za Kiswahili.

Makosa yalibainika katika upatanisho wa kisarufi kwa kuzingatia ngeli za Kiswahili zisizobadili viambishi katika hali ya umoja na wingi ambazo kulingana na Mbaabu (1985), Were (1997) na King'ei na Musau (2002) ni (N-N). Katika ngeli hii nomino hazibadiliki katika hali ya umoja na wingi. Kulingana na muundo wa Ekegusii kila nomino ina wingi kwa hivyo wanafunzi Wakisii walizipa nomino za Kiswahili za ngeli ya (N-N) viambishi vya hali ya umoja na wingi na kusababisha makosa yafuatayo wakati wa mijadala.

Ekegusii

Umoja	Wingi	Makosa ya kisarufi	Kiswahili sanifu
(i) e-riogo	ama-riogo	madawa	dawa
(ii) e-nyagitari	chi- nyagitari	mazahanati	zahanati

(iii) e-nyomba	chi-nyomba	manyumba	nyumba
(iv) e-chayo	ama-chaya	madharau	dharau
(v) e-kerengererio	e-birengererio	mafikira	fikira

Makosa yalijitokeza kwa sababu wanafunzi waliohusika walifuata ngeli ya Ekegusii ya { ri-, eri-, oko- / ama-}

Pia walifuata ngeli ya Ekegusii ya {omo – aβa} na hivyo kufanya makosa yafuatayo:

Ekegusii

Umoja	Wingi	Makosa ya kisarufi	Kiswahili sanifu
(i) tata	aba-tata	wa-baba	baba (akina baba)
(ii) mama	aba-mama	wa-mama	mama (akina mama)

Makosa ya kutozingatia ngeli katika upatanisho wa kisarufi katika mijadala yalitumiwa kama kigezo cha kuthibitisha makosa kama haya yatakayobainishwa katika uandishi wa insha na athari zake katika matokeo ya mitihani ya Kiswahili.

4.1.2. Makosa katika upatanisho wa kisarufi kwa kuzingatia vivumishi

Katika utafiti huu ilibainika kwamba wanafunzi walitumia kimakosa vivumishi mbalimbali kwenye mazungumzo yao. Katika kufanya hivyo, ilikuwa vigumu kuelewa maana hasa iliyokusudiwa. Kupoteza maana katika uandishi wa insha hupunguza tuzo za wanafunzi na kuathiri vibaya matokeo ya mtihani wa Kiswahili.

4.1.2.1. Vivumishi vya sifa

Wanafunzi walifanya makosa ya upatanisho wa kisarufi kwa kutotumia kisahihi vivimishi vya sifa kulingana na ngeli za Kiswahili.

Matumizi yasiyofaa ya vivumishi vya sifa	Matumizi sahihi
1. madhara kubwa	madhara {ma}kubwa
2. huko ni mbaya	huko ni {ku}baya
3. safari mrefu	safari {nd}efu
4. kichwa ngumu	kichwa {ki}gumu

4.1.2.2. Vivumishi vimilikishi

	Ekegusii	Matumizi yasiyofaa ya vivumishi vimilikishi	Matumizi sahihi
i.	aβasae βaito	vijana yetu	vijana wetu
ii.	eng'mbe ya-	ng'ombe ya....	ng'ombe wa...
iii.	omo- skari one	askari yangu	askari wangu
iv.	chi-sese chia-	mbwa za	mbwa wa...
v.	chi-ngendo chi-aino	mienendo zenu	mienendo yenu

Wanafunzi Wakisii walifanya makosa katika upatanisho wa kisarufi kwa kutumia vivumishi-vimilikishi. Walipata utata wa matumizi ya vivumishi-vimilikishi kwani walifuata muundo wa ngeli za Ekegusii ambazo ni tofauti na ngeli za Kiswahili. Katika ngeli za Ekegusii nomino za wanyama, ndege,wadudu haziwezi kupatanishwa na vivumishi- vimilikishi sawa na vile vya nomino za binadamu. Kwa kuzingatia muundo wa Ekegusii wa matumizi ya vivumishi-vimilikishi wanafunzi walifanya makosa ambayo yaliathiri tuzo na matokeo yao ya mtihani wa Kiswahili.

4.1.2.3. Vivumishi vya {-enye} na {-enyewe}

Ekegusii	Matumizi yasiyofaa ya vivumishi -enye	Kiswahili Sanifu
(i) βuna totagete	vyenye vile tunataka	vile tunavyotaka
(ii) chiria chikoβwatia	zenye zinafuatwa	zinazofuatwa / zenye kufuatwa
(iii) aβanto βaria mwanchete	watu wenye mnapenda	watu mnaopenda
(iv) keria βarenge βagokwana	chenye walikuwa wakisema	walichokuwa wakisema
(v) keria nkoβateβia	chenye nawaambia	ninachowaambia

Muundo wa Ekegusii unafuata matumizi ya vivumishi vya {–enye} na {–enyewe} sawa na Kiswahili lakini wanafunzi Wakisii walitatizika kuvitumia vivumishi hivi. Haikutarajiwa kwamba makosa haya yangetokea wakati wakivitumia vivumishi hivi kuambatana na ngeli za Kiswahili. Utata wa matumizi ya vivumishi vya {–enye} na {–enyewe} unaweza kubashiriwa kuwa ni athari zinazotoka katika miundo ya lugha ambazo si Ekegusii au Kiswahili.

Makosa haya yalibashiriwa kutokea katika uandishi wa insha na kuchangia katika kupunguza tuzo za wanafunzi katika kitengo cha sarufi na hatimaye kuathiri vibaya matokeo ya mtihani wa Kiswahili.

4.1.2.4. Vivumishi vya {-ote }na {-o-ote}

Katika muundo wa Ekegusii vivumishi vya{–ote} na {–o-ote}vya Kiswahili ni kama {–nde –nsi}.

Kulingana na muundo wa Ekegusii, kivumishi {y-o-y-ote} hutumiwa katika ngeli zote za Kiswahili na wanafunzi wanafuata muundo huu na kufanya makosa ya kisarufi. Makosa haya hudhihirika zaidi wakati majina ya wanyama, wadudu na ndege yanatumika. Wanafunzi walifanya makosa yafuatayo wakati wa kutumia vivumishi hivi katika mazungumzo.

	Ekegusii	Matumizi yasiyofaa	Matumizi sahihi
i.	omonto o-nde βwe-nsi	mtu wowote	mtu yeyote
ii.	aβaiβiβo-nsi	wezi yote	wezi wote
iii.	egento ke-nde gio-nsi	kitu yoyote	kitu chochote
iv.	omote βwo-nsi	mti yote	mti wote

Makosa waliyofanya wanafunzi katika kuvitumia vivumishi {–ote}na {–o-ote} kwenye mijadala yalibashiriwa kutokea katika uandishi wa insha.

4.1.2.5. Vivumishi vya {-a}unganifu

Ekegusii hutumia vivumishi-unganishi ambavyo ni tofauti na vile vinavyotumiwa katika Kiswahili. Wanafunzi Wakisii hupata utata wanapotumia vivumishi-unganishi vya Kiswahili kwani hufuata muundo wa Ekegusii na hivyo kufanya makosa ya kisarufi. Wanafunzi waliohusika katika mijadala walifanya

makosa katika matumizi ya vivumishi vya {-a} unganifu na hivyo kuonyesha jinsi athari za Ekegusii zilivyoathiri sarufi ya Kiswahili.

	Ekegusii	matumizi yasiyo ya vivumishi a-unganifu	Kiswahili sanifu
i.	ensemo y-a	eneo y-a...	eneo l-a
ii.	enda y-a	tumbo y-a...	tumbo l-a
iii.	engoro y-a	shimo y-a ...	shimo l-a
iv.	ensemo y-a	mahali y-a...	mahali p-a

Wanafunzi wahusika walifanya makosa ya kisarufi walipokuwa wakitumia vivumishi vya {-a}unganifu katika mazungumzo yao. Walitatizika kuvitumia vivumishi hivyo kulingana na ngeli za Kiswahili na hivyo wakaonyesha dalili za upungufu wao hata katika uandishi wa insha.

4.1.2.6. Vivumishi vya idadi

4.1.2.6.1. Vivumishi vya idadi ya jumla

Makosa yalijitokeza miongoni mwa wazungumzaji kwa sababu ya kutozingatia ngeli za Kiswahili. Walitatizika wakati wa kutumia vivumishi vya idadi ya jumla kuambatana na ngeli mbali mbali kama ifuatavyo:

	Matumizi yasiyofaa	Matumizi sahihi
i.	shule mingi	shule nyingi
ii.	mali mengi	mali nyingi
iii.	shida mingi	shida nyingi
iv.	mvua mingi	mvua nyingi

Kutokana na makosa yaliyoorodheshwa hapo juu inabainika kwamba wanafunzi wahusika walipata utata katika matumizi ya vivumishi vya idadi ya jumla katika ngeli ya (N- N). Hali hii inathibitisha kutokuwepo na ngeli sawa na hii katika mfumo wa Ekegusii. Makosa haya yalitumiwa kubashiri tatizo sawa kama hili katika uandishi wa insha wa wanafunzi Wakisii.

4.1.2.6.2. Vivumishi vya idadi kamili.

Katika muundo wa Ekegusii vizio vya tano na kumi hutumika katika kukamilisha idadi. Idadi yoyote chini ya tano haibadiliki lakini idadi hiyo, ila nne, huongezewa idadi inapokuwa zaidi ya tano lakini chini ya tisa. Mfano ufuatao unafafanua maelezo haya:-

Idadi (tarakimu)	matamshi	tafsiri	Kiswahili sanifu
1	eyemo	moja	moja
2	iβere	mbili	mbili
3	isato	tatu	tatu
4	inye	nne	nne
5	isano	tano	tano
6	isano ne'mo	tano na moja	sita
7	isano na iβere	tano na mbili	saba
8	isano na isao	tano na tatu	nane
9	kianda	kenda / tisa	kenda / tisa
10	ikomi	kumi	kumi

Wanafunzi Wakisii walipata utata wa upatanisho wa nomino na tarakimu katika Kiswahili kwa sababu ya tofauti za upatanisho zilizoko baina ya Ekegusii na Kiswahili wakati wa kutumia tarakimu. Wanafunzi walifanya makosa ya kisarufi hasa katika ngeli ya {M-Wa} ambapo, kulingana na muundo wa Ekegusii, nonino za wanyama, ndege na wadudu hazikubaliki kwenda sambamba na za binadamu katika hesabu. Hivyo, makosa yafuatayo yalijitokeza katika mazungumzo ya wanafunzi Wakisii.

Makosa ya upatanisho wa vivumishi na tarakimu	Kiswahili sanifu
1. wakulima tano	wakulima watano
2. wezi wasaba	wezi saba
3. mbuzi nne	mbuzi wanne
4. viboko tatu	viboko vitatu
5. miti mikumi	miti kumi
6. mkono moja	mkono mmoja

7. mtu moja mtu mmoja

Kulingana na mfumo wa Ekegusii viambishi-awali huwekwa katika tarakimu zote ila tisa na kumi. Mfumo wa Kiswahili hauna viambishi -awali katika tarakimu za sita, saba,tisa na kumi. Wanafunzi Wakisii waliweka viambishi - awali katika nomino za tarakimu za sita na saba katika hali ya wingi na hivyo kufanya makosa ya kisarufi.

4.1.2.7. Viashirii

Wanafunzi waliohusika katika mijadala walipata utata wa matumizi ya viashirii kulingana na ngeli za Kiswahili. Utata huu ulijitokeza kwa sababu tofauti za miundo ya ngeli katika lugha hizi mbili. Walichanganya ngeli walipokuwa wakitumia viashirii kama inavyobainishwa katika mifano inayofuata.

Matumizi yasiyofaa ya viashirii	Matumizi sahihi
1. hii maneno	haya maneno
2. hii ugonjwa	huu ugonjwa
3. pande hii	upande huu au pande hizi
4. hiyo tatizo	tatizo hilo
5. hiyo ndiyo mwisho	huo ndio mwisho
6. hii kilimo	kilimo hiki
7. hizi mambo	haya mambo
8. mtu hii	mtu huyu

Makosa ya matumizi yasiyofaa ya viashirii yaliyofanywa katika mazungumzo yalikuwa ni dalili ya utata unaowapata wanafunzi Wakisii wanapoandika insha za Kiswahili. Upungufu huu huwafanya wanafunzi watahiniwa kupata tuzo duni na hatimaye huchangia matokeo mabaya ya mtihani wa Kiswahili.

4.2. Makosa katika matamshi ya msamiati wa Kiswahili

Wanafunzi Wakisii wa kidato cha nne walitamka vibaya msamiati wa Kiswahili walipokuwa wakizungumza wakati wa mijadala. Waliongezea vokali zisizokubalika mwishoni mwa maneno ya Kiswahili na hivyo kupotosha maana.

Makosa hayo ni kama yafuatayo:-

Msamiati ulioongezewa vokali mwishoni	Msamiati sahihi
hasaa	hasa
mbuu	mbu
kapisaa	kabisa
seminaa	semina

Makosa kama haya yanapofanywa katika uandishi wa insha husababisha kupunguzwa kwa tuzo za watahiniwa katika kitengo cha sarufi na hatimaye kuchangia matokeo duni ya mtihani wa Kiswahili.

4.2.1. Matumizi yasiyofaa ya msamiati wa Kiswahili

Wanafunzi walitumia msamiati wa Kiswahili kimakosa katika mazungumzo yao jambo lililosababisha kutopatikana maana iliyokusudiwa.

Msamiati uliotumiwa isivyofaa	Kiswahili sanifu
barani / mjini	nchini
vijana na wasichana	wavulana na wasichana
vitu	bidhaa

4.2.2. Matamshi yasiyofaa ya msamiati wa Kiswahili

Wanafunzi Wakisii walitamka kimakosa msamiati wa Kiswahili sanifu wakati wa mazungumzo. Makosa fulani yalitokana na mazoea ya matumizi ya muundo wa Ekegusii badala ya muundo wa Kiswahili.

	Matamshi yasiyofaa ya Msamiati wa Kiswahili Sanifu	Kiswahili sanifu
1.	gonjeka	ugua / kuwa mgonjwa
2.	migorogoro	migogoro
3.	makoso	makosa

Katika muundo wa Ekegusii kitenzi kinachotokana na nomino {oβorwaire - ugonjwa } ni {korwara} ambayo wanafunzi walitafsiri moja kwa moja kuwa {gonjeka}.

Makosa mengine yaliyofanywa ya matamshi yalitokana na athari za lugha nyingine ambazo si Kiswahili wala Ekegusii. Msamiati huo ni {mazingara} badala ya {mazingira} na {wenyu} badala ya {wenu}.

4.2.3. Tafsiri kutoka Ekegusii hadi Kiswahili

Ilibainika kwamba aghalabu wanafunzi walifanya tafsiri ya moja kwa moja ya maneno na semi kutoka Ekegusii hadi Kiswahili na katika kufanya hivyo walipotosha maana iliyokusudiwa. Mifano ifuatayo inathibitisha tatizo hili:

Ekegusii	maneno / semi zilizo-tafsiriwa kimakosa	maneno / semi Kiswahili sanifu
(i) ira {amang'ana} ..	peleka {maneno}haya...	peleka {ujumbe}...
(ii) ense etigare {βosa}	nchi kubaki { bure}	nchi kubaki {tupu}
(iii) {konywa} enyasore	{kutumia bangi, pombe}	{kuvuta} bangi {kunywa} pombe
(iv) { korosia} endagera	{kutengeneza} chakula	{ kupika/ kuandaa} chakula
(v) {komoiraneria} Nyasae βuya mono)	{kurudishia} Mungu asante	{kumshukuru} Mungu

4.2.4. Matumizi ya msamiati wa Kiingereza

Ilibainika pia kwamba, badala ya wanafunzi kutumia maneno ya Kiswahili katika mijadala ya Kiswahili walitumia maneno ya Kiingereza kama yalivyo. Kwa kufanya makosa ya kimsamiati namna hii ilibashiriwa kuwa wanafunzi waliohusika wangedunisha tuzo zao katika sarufi na hatimaye kupata matokeo mabaya katika mtihani wa Kiswahili. Maneno yafuatayo ya Kiingereza yaliyotumiwa badala ya Kiswahili Sanifu.

	Kiingereza	Kiswahili sanifu
i.	condom	mipira ya kuzuia mimba na magonjwa
ii.	effective	bora / inayofaa

iii. remote mashambani / sehemu isiyo na mawasiliano mazuri

iv. area eneo / sehemu

v. bonus malimbikizo ya faida

vi. factory kiwanda

vii. line kufuata taratibu / kutii / kuafikiana


Matumizi ya msamiati wa Kiingereza yalibainisha upungufu wa wanafunzi katika umilisi wa Kiswahili. Upungufu unapotokea katika uandishi wa insha huathiri tuzo za na matokeo ya mtihani wa Kiswahili kwa wanafunzi wahusika.

4.3. Sauti za Ekegusii na Kiswahili

4.3.1. Sauti za Ekegusii.

Fonetiki ya Ekegusii haijashughulikiwa sana lakini utafiti mchache uliofanywa unabainisha kuwepo kwa sauti za vokali saba. Whiteley (1958), Bosire (1993) na Ongarora (1996) wanabainisha kwamba vokali hizi ni [a, e,ɛ , i, o, ɔ, u]. Sauti hizi za vokali zinawasilishwa kama inavyoonyeshwa katika mchoro uliopo hapa chini.

Mchoro (i) Vokali za Ekegusii



Bosire (1993), na King'ei na Musau (2002) wanabainisha katika utafiti wao kwamba kuna konsonanti kumi na nne za Ekegusii kama inavyodhihirishwa katika jedwali linalofuata.

	midomo	Midomo meno	menoni	ufizi	Kaa kaa gumu	Kaa kaa laini	koromeo
Vipasuo				t	ch	k gh	
Vikwamizo	β			s			h

Ving'ong'o / nazali	m			n	ny	ng'	
Vimadende					r		
Viyeyusho	w				y		

(sauti zimeandika kiothografia ili wasomaji wa kawaida waelewe kwa urahisi)

Katika utafiti huu imebainishwa kuwepo kwa konsonanti kumi na tatu ambazo ni [β] , [m], [t], [s], [n], [č],[r], [k], [g], [∩] [ŋ], [y] na [w] na [y].

Sauti hizi za konsonanti zinawasilishwa katika jedwali kama ifuatavyo.

	midomo	Midomo meno	menoni	ufizi	Kaa kaa gumu	Kaa kaa laini
Vipasuo				t	č	k g
Vikwamizo	β			s		
Ving'ong'o	m			n		∩ ŋ
Vidende					r	
Viyeyusho	w				j	

4.3.2. Sauti za Kiswahili

Lugha ya Kiswahili ina sauti za vokali tano ambazo ni [a, e, i, o na u]. King'ei na Musau (2002) wanaeleza kwamba lugha hii ina vitamkwa au sauti za konsonanti ishirini na nne ambazo ni [p], [b], [č], [ɟ], [t], [d], [θ], [ð], [f],[v], [g] ,[ɣ], [h], [k] , [l], [m], [n], [p], [r], [s], [z], [ʃ], [w] na [j].

Muundo wa Ekegusii hauna konsonanti za [b] na [d], mwanzoni mwa maneno. Pia hazipatikani kati kati ya irabu. [b], [d], hupatikana baada ya konsonanti za nazali za [m] na [n] peke yake ambapo huunda sauti za [mb] na [nd]

Konsonanti za Ekegusii zinapolinganishwa na za Kiswahili sanifu inabainika kwamba konsonanti zifuatazo za Kiswahili hazipatikani katika Ekegusii [p], [θ], [ð],[f],[v], [ɣ] [h],[ɟ] [l],[z], na [ʃ].

Katika utafiti wao, King'ei na Musau (2002:3) wanadai kuwepo kwa kikwamizwa [h] miongoni mwa konsonanti za Ekegusii lakini utafiti huu unabainisha kwamba kikwamizwa [h] si miongoni mwa sauti za konsonanti za Ekegusii.

Katika kukamilisha matamshi ya maneno, Kiswahili kina mpangilio wake maalumu wa kuunganisha konsonanti moja, mbili au zaidi kwa kutumia irabu. Kuambatana na mfumo wake Kiswahili hakina maneno yanayoundwa kwa kutumia konsonanti peke yake.

4.4. SAUTI NA MAHALI PA KUTAMKIA

Ngero (1996) anaeleza jinsi sauti zinavyotamkwa na mahali pa kutamkia. Katika utamkaji wa konsonanti, pumzi hupitia pango la kinywa ambapo kwa kiasi Fulani, huzuiwa. Mahali ambapo sauti huzuiliwa wakati sauti inapotolewa huitwa mahali pa kuatamkia.

4.4.1. Sauti za midomo.

Hizi ni ni / p / na / b /.

Wakati wa kuatamka sauti / p /, mdomo wa chini hugusana na wa juu. Pumzi kutoka mapafuni huzuiliwa na midomo na hatimaye kuachiliwa mara moja.

Sauti / b / hutamkiwa pale pale ambapo sauti / b / hutamkiwa lakini pumzi huachiliwa taratibu.

4.4.2. Sauti za midomo-meno.

Hizi ni / f / na / v /.

Wakati wa kutamka / f / mdomo wa chini hukaribiana na meno ya juu.

Pumzi kutoka mapafuni huzuiliwa kati yam domo wa chini na meno ya juu.

Pumzi huachiliwa mara moja.

Hali sawa hutokea wakati wa kutamka / v / lakini pumzi huachiliwa taratibu.

4.4.3. Sauti za ufizi.

Sauti za ufizi ni / t / na / d /.

Wakati wa kutamka sauti / t / na / d /, ncha ya ulimi hukaribia ufizi. Pumzi kutoka mapafuni huzuiliwa kati ya ulimi na ufizi. Tofauti iliyopo ni kwamba

wakati wa kutamka / t / pumzi huachiliwa mara moja ilhali wakati wa kutamka sauti / d / pumzi huachiliwa taratibu

4.4.4. Hali ya glota na mahali pa kutamkia na jinsi ya kuatamka.

/ p / na / b / ni sauti za midomo ambazo ni vituo ambapo / p / ni kituo si ghuna na / b / ni kituo ghuna.

Katika utamkaji wa / p /, / f / na / t / nyuzi za sauti hufunguka. Kutokana na hali hii mambo yafuatayo ni lazima yaeleweke wazi.

/ p / ni kituo si ghuna (hafifu) cha midomoni.

/ f / ni kikwaruzo si ghuna cha mdomo-meno

/ t / ni kituo si ghuna cha ufizi.

4.4.5. Mahali pengine pa kutamkia.

4.4.5.1. Sauti za kaa kaa gumu na ulimi.

Hizi ni / č / na / ɟ / na / ∩ / na / j /

Wakati wakutamka sauti hizi ncha ya ulimi hukaribia kaakaa gumu.

Sehemu ya mbele ya ulimi hujipinda kwenye ukuta wa kinywa

4.4.5.2. Sauti za kaa kaa laini na ulimi

Hizi ni / k /, /g / na / ŋ /.

Wakati wa kutamka sauti hizi sehemu ya ulimi hukaribia kaa kaa laini.

4.4.5.3. Sauti ya koromeo

Sauti ya koromeo ni / h /. Pumzi husukumwa nje kwa nguvu bila kuzuiwa.

4.5. VITUO

Vituo vimegawanywa mara mbili ambavyo ni vipasuo na vizuio-kwamiza

4.5.1. Vipasuo.

Hizi ni sauti ambazo hutolewa wakati ambapo ala za kutamkia hukutanishwa na kukusanya pumzi. Pumzi hiyo husababisha ala hizo kutenganishwa kwa ghafla kana kwamba kuna mpasuko.Baada ya kutenganishwa kwa ghafla, sauti zinatoka kwa nguvu.

	Midomo	ufizi	kaa kaa laini
Vipasuo si ghuna	p	t	k
Vipasuo ghuna	b	d	g

4.5.2. Vizuio-kwamiza

Vizuio-kwamiza hivi ni / Č / na / ʄ /.

Wakati wa kuzitamka sauti hizi, pumzi huzuiliwa na ulimi pamoja na kaa kaa gumu na zinapotoka, hutoka kwa shida ndipo zikaonekana kuwa za kukwamiza.

Sauti / Č / ni kizuiwa-kwamiza si ghuna na / ʄ / ni kizuiwa-kwamiza ghuna.

4.5.3. Vikwaruzo / vikwamizo

Hizi ni sauti ambazo, wakati wa kuzitamka, pumzi hutoka kwa kukwaruzana na kukwamizwa na ulimi pamoja na zile ala nyingine zinazotumika kuzitamka. Ala hizi huwa zimekaribiana na pumzi hupishwa kati yake.

	Mdomo-meno	ufizi	kaa kaa laini	koromeo
Vikwaruzo / vikwamizo si ghuna	f	s	ɣ	h
Vikwaruzo / vikwamizo ghuna	v	z		

4.5.4. Sauti za Nazali / vipua / ving'ong'o

Sauti hizi hutamkwa kwa kukutanisha ala za sauti ambapo kilimi hufunga pango la kinywa na hivyo pumzi hutokea puani.

Sauti hizi zote ni za mghuno.

Midomo	midomo-meno	ufizi	kaa kaa gumu
m	m	n	∩

/ m / ambayo ni nazali ya midomo-meno hutokea tu pale ambapo nazali /m / ya midomoni hufuatwa na kituo cha midomo kama vile katika {mpango}, {mbwa}na mČana

4.5.5. Sauti ya kitambaza

Sauti ya kitambaza ni / l /. Wakati wa kuitamka sauti hii, ncha ya ulimi hukutanishwa na ufizi. Ulimi hutambaza pumzi pande zake zote – kulia na kushoto. Sauti hii ni hafifu (si ghuna)

4.5.6. Sauti ya kimadende

Sauti ya kimadende ni / r /. Utamkaji wa kimadende huhusisha kufungafunga na kufunguafungua. Sauti hii hutolewa wakati ala inayotetematetema hupigapiga kwenye ala bwete. Katika utamkaji wa / r / ala inayotetematetema ni ncha ya ulimi ambayo hupigapiga kwa mfululizo kwenye ufizi.

4.6. Tatizo la kisauti.

Kama ilivyodhihirika hapo juu Kiswahili kina sauti nyingi kuliko Ekegusii. Kutokana na upungufu huu wanafunzi Wakisii hujikuta taabani wanapokuwa wakijifunza na kukitumia Kiswahili Sanifu. Hata baada ya kujifunza na kujua maneno kadhaa ya Kiswahili, wanafunzi hawa hutatizika na hata kushindwa kupambanua dhana fulani.

Kwa kutotumia kisahihi baadhi ya maneno ya Kiswahili Sanifu wanafunzi Wakisii hufanya makosa katika utamkaji na uandikaji wa maneno ya Kiswahili.

4.6.1. Mifanyiko ya kifonolojia .

Katika sehemu hii utafiti huu unabainisha jinsi wanafunzi Wakisii wanavyobadilisha sauti moja hadi nyingine hasa walipokuwa wakitamka sauti ghuna na zile ambazo si ghuna. Wakati sauti ghuna inapotamkwa kama sauti si ghuna huwa ni mfanyiko wa kifonolojia wa udhoofishaji ambapo sauti moja hupoteza nguvu na kutamkwa kama sauti si ghuna. Baadhi ya sauti ghuna ambazo zilidhoofishwa na kuwa si ghuna wakati wa mijadala ni [b], [d],[ð], na [v],

Wakati sauti si ghuna zinapotamkwa kama sauti ghuna huu huwa ni mfanyiko wa kifonolojia wa uongezaji nguvu. Hivyo basi sauti si ghuna huongezwa nguvu na kutamkwa kama sauti ghuna. Sauti si ghuna ambazo ziliongezwa nguvu wakati wanafunzi Wakisii walipozitamka ni [p], [θ], [f], [t] na [z]. Katika maelezo

yanayofuata utafiti huu unaonyesha jinsi sauti mbali mbali za Kiswahili zilivyodhoofishwa ama kuongezwa nguvu na jinsi mifanyiko hii ya kifonolojia ilivyobadilisha maana iliyokusudiwa ya maneno ya Kiswahili.

4.6.1.1. Sauti za [b] na [p]

Ekegusii hakina sauti za[b] na [P] na badala yake kina sauti [β] hivyo basi, Mkisii ambaye hajafundishwa juu ya sauti za [b]na [p] hutumia [β]. Katika utafiti huu imebainika kwamba baada ya kufundishwa wanafunzi Wakisii hutamka sauti [b]na [p] bila kutofautisha ni sauti gani ingepasa kutumiwa katika matamshi ya maneno. Hupata utata wa kimatamshi na ndipo hufanya makosa ya kimatamshi yanayopotosha maana inayokusudiwa.

[b] na [p], ni vipasuo vya midomo. [p] ni kipasuo si ghuna ilhali [b] ni kipasuo ghuna. Nyuzi za sauti hazirindimi wakati wa kutamkwa. Wakati wa kutamka [b] sauti huachiliwa taratibu huku nyuzi za sauti zikirindima.

Sauti hizi mbili [p] na [b] hazimo katika sauti za konsonati za Ekegusii. Wakati wanafunzi Wakisii wanapojifunza Kiswahili hukumbuna na sauti hizi ngeni na hutatizwa wanapotamka maneno yenye sauti hizi. Utata hutokea mwanzoni na katikati ya neno. Wanafunzi hawa huwa na utata wa kupambanua ni sauti gani itumiwe na hivyo hutamka sauti yoyote baina yao. Mifano ifuatayo inadhihirisha makosa hayo:

[b] =====→ [p] (sauti ghuna ya [b] hudhoofishwa na kuwa sauti si ghuna ya [p]. Huu ni mfanyiko wa kifonolojia wa udhoofishaji wa sauti. Wanafunzi walitamka maneno yanayofuata kwa kubadilisha sauti na hivyo kufanya makosa ya kisarufi:-(i) { barabara }: njia kubwa → {parapara}: parapara ni neno lisilo na maana

(ii) {kabisa]: mno, zaidi → {kapisa }: kapisa ni neno lisilo na maana

(iii) { karibia }: sogelea karibu→ {karipia }:kemea

Kama ilivyokwisha elezwa, wanafunzi Wakisii hubadilishana sauti za [b] na [p]. Ifuatayo ni mifano ambapo wanafunzi Wakisii walitamka [p] badala ya [b] ambao ni mfanyiko wa kifonolojia wa uongezaji nguvu.

[p] =====→ [b]. Sauti si ghuna ya [p] huongezwa nguvu na kutamkwa sauti ghuna ya [b]

(i) { pa: }: mnyama, au juu ya. → {ba:}: shida au janga

(ii) {panda}: kwea au weka mbegu ardhini → { banda}:jengo litumikalo kuwekea vitu ama wanyama.

(iii) {pili} baada ya moja → {biri}:aina ya jani la tumbaku

Ubadilishaji wa sauti moja hadi nyingine miongoni mwa wazungumzaji kulibadilisha maana ya maneno yaliyotumiwa. Matokeo yake ni kufanya makosa ya kisarufi ambayo yakiendelezwa katika uandishi wa insha utapunguza tuzo za wanafunzi na kuathiri matokeo ya mtihani wa Kiswahili.

4.6.1.2. Sauti za [t , d , θ na ð]

Sauti za [t] na [d] ni vipasuo vya ufizi. Sauti ya [t] ni kipasuo si ghuna cha ufizi. Kipasuo hiki kinapotamkwa, ncha ya ulimi hugusa mbele ya ufizi karibu na meno . Meno hushikamana kidogo. Sauti hukazwa na kuachiliwa kwa haraka. Nyuzi za sauti hazirindimi.

[d]ni kipasuo ghuna ambacho hutamkiwa kwenye ufizi. Ncha ya ulimi hupinda kidogo na kugusa ufizi . Meno huachana na sauti hutoka taratibu. Nyuzi za sauti hurindima.

Lugha ya Ekegusii haina sauti [d] isipokuwa imetanguliwa na konsonanti nazali [n] hivyo, wanafunzi wanaojifunza Kiswahili hupata utata wa kukitamka kipasuo hiki kikiwa peke yake. Utata huu hupatikana mwanzoni mwa neno . Yafuatayo ni makosa ya kimatamshi wakati sauti ghuna ya [d] ilidhoofishwa na kutamkwa kama sauti si ghuna ya [t]:-

[d] =====→ [t]

(i) {damu }: maji maji mekundu yenye uhai mwilini → {tamu}: -enye ladha nzuri

(ii) {bidi: }: mkazo, juhudi → {biti:}: halina maana

(iii) {hadi}: mpaka → {hati }: ufundi au ujuzi

Lugha ya Ekegusii haina sauti za vikwamizwa meno vya [θ] na [ð].

[θ] ni konsonanti kikwamizwa si ghuna cha meno. Hewa husukumwa nje huku ikikwamizwa menoni. Hewa hutokea pembeni mwa ulimi kwa haraka.

[ð]ni kikwamizwa ghuna cha meno. Wakati wa kutamkwa ncha ya ulimi hugusa meno ya juu. Hewa husukumwa nje taratibu huku ikikwamizwa menoni. Nyuzi za sauti hurindima.

Wanafunzi walipata utata wakati wa kutamka [θ] na [ð]. Walitamka kwa kubadilishana sauti hizi au kutumia sauti za vipasuo vya ufizi vya [t] na [d]. Sauti ghuna ya [ð] ilidhoofishwa na kutamkwa kama sauti si ghuna ya [θ]. Mifano ifuatayo inabainisha utata huu.

[ð] =====→ [θ]

(i) {ðaifu}: –siyo nguvu, nyonge → { θaifu} thaifu halina maana

(ii) {niðamu}: ustaarabuau adabu → {nithamu} halina maana

(iii) {kaða:]: idadi fulani → {kaθa:} halina maana.

Sauti si ghuna ya [θ] iliongezewa nguvu na kutamkwa kama sauti ghuna ya [ð]. Mifano ifuatayo inabainisha utata huu.

[θ] =====→ [ð]

(i) {θamani}: gharama au bei → { ðamani} halina maana

(ii) {riθi }: kumiliki badala ya → {riði}: halina maana

(iii) {θumuni}: senti hamsini → {ðumuni}: halina maana

Kadhalika mfanyiko wa kifonolojia wa udhoofishaji ulijidhihirisha katika kutamka sauti [ð] ilidhoofishwa na kuwa sauti si ghuna [t]. Ifuatayo ni mifano ya makosa yaliyofanywa kwa kudhoofisha [ð] sauti na kuwa sauti si ghuna ya [t].

[ð] =====→ [t]

(i) { ba:ði }: miongoni mwa au kati ya → { ba:ti}: baati halina maana

(ii) {biða:} mali ya kuuzwa → { bita:}:halina maana

(iii) {mawaiða}: maelekezo,ushauri → {mawaita}: halina maana

4.6.1.3. sauti za [č] na [ʄ]

Hivi ni vipasuo vya kaa kaa gumu. Wakati wa kutamka [č] na [ʄ] sehemu ya juu ya ulimi huruhusiwa kukaribia kaa kaa gumu ili hewa ipitishwe kikamilifu juu ya ulimi . Sauti [č] ni kipasuo si ghuna. Wakati wa kutamkwa ulimi huwa kati kati ya meno ya juu na ya chini. Hewa hutoka ndani kwa nguvu na kukwaruzwa menoni. Nyuzi za sauti hazirindimi.

[ʄ] ni sauti si ghuna ya kaa kaa gumu. Wakati wa kuitamka ncha ya ulimi hugusa kaa kaaa gumu. Hewa huvutwa ndani na kutoka nje taratibu.

Katika muundo wa Ekegusii kuna sauti ya [č] lakini hakuna sauti ya [ʄ]. Hivyo wanafunzi Wakisii wanaojifundisha Kiswahili hutatizika wanapotaka kutumia sauti ya [ʄ]. Matokeo ni kwamba hutumia [č] badala ya [ʄ]. Huu ni mfanyiko wa kifonolojia ambapo sauti ya ghuna ya[ʄ] hudhoofishwa na kutamkwa kama sauti si ghuna ya [č]. Mifano ifuatayo inadhihirisha utata huu:-.

[ʄ] =====→ [č] (udhoofishwaji wa [ʄ])

(i) {kiʄana }: mtu aliyepita kipindi cha kubalehe: → {kičana}:kifaa cha kutengezea nywele.

(ii) {ʄua }: fahamu, elewa → {čua}: ni kupambana

(iii) {maʄi}: ya kunywa / kuoga → {mači}:halina maana.

Wakati mwingine wanafunzi hutatizika wakati wa kutumia [č] na [ʄ] hivyo huhamisha sauti za [č] hadi za [ʄ]. Huu ni mfanyiko wa kifonolojia ambapo sauti si ghuna huongezewa nguvu na kutamkwa kama sauti ghuna. Mifano inayofuata inaonyesha utata huu ambapo maana iliyokusudiwa hubadilishwa:-

[č] =====→ [ʄ] (uongezwaji nguvu wa [č])

(i) {čanzo}: kiini, sababu. → { anzo]: halina maana.

(ii) {čini}: kutokuwa juu → { ini}: aina ya mnyama wa ajabu

4.6.1.4 Sauti za [f] na [v]

Hivi ni vikwamizwa ambavyo hutamkiwa katikati ya midomo na meno. [f] ni kikwamizwa si ghuna cha meno. Wakati wa kukitamka meno ya juu hushikana na midomo ya chini huku kukibakia mwanya ambapo sauti hupitia kwa haraka.

[v] hutamkiwa katika midomo na meno. Midomo na meno hushikana taratibu na sauti ya mghuno hutoka kwa taratibu. Lugha ya Ekegusii haina kikwamiza [v] bali huwa na kikwamiza [β].

Wanafunzi Wakisii wanapofunzwa Kiswahili hupata utata wa kutamka vikwamizwa

[f] na [v]. Katika utafiti huu ilibainika kwamba wanafunzi wahusika walivitumia vikwamizwa hivi vya midomo kwa kubadilishana. Kulingana na muundo wa Ekegusii vikwamizwa hivi havipatikani mwanzoni wala katikati ya neno. Katika mifano ifuatayo utata huo unadhihirishwa:

[v] =====→ [f] (udhoofishwaji wa [v])

(i) {mavuno}: mapato ya shambani → {mafuno}:halina maana

(ii) { vita}: mapigano. → {fita}: halina maana

(iii) {vamia}: shambulia → {famia}: halina maana

Pia wanafunzi wahusika walibadilisha sauti [f] kuwa [v] ikiimaanisha kwamba sauti si ghuna ya [f] iliongezewa nguvu na kutamkwa kama sauti ghuna ya [v]. Mifano inayofuata inaonyesha utata huu ambapo maana iliyokusudiwa hubadilishwa:-

[f] =====→ [v] (uongezwaji nguvu wa [f])

(i) {fa:}: kutosheleza au kunufaisha → { va:}:kutia vazi mwilini

(ii) {havifai}: si vya manufaa → {havivai} - havitii vazi mwilini.

(iii) {futwa}: panguswa au ondolewa → {vutwa} kupelekwa karibu

4.6.1.5. Sauti za [s], [z] na [ʃ]

Sauti [s] ni kikwamizwa si ghuna cha ufizi. Hutamkwa wakati meno ya juu na ya chini yamekaribiana sana lakini mwanya mdogo hubaki ambapo hewa hupita huku ikikwaruzwa. Ulimi huwa umenyooka na ncha yake kugusa ufizi.

Sauti [z] ni kikwamizwa si ghuna cha ufizi .Wakati wa kutamkwa ulimi hukaribiana sana na ufizi. Hewa hutolewa nje taratibu na kuwa na mkwaruzo mdogo kati ya ufizi na meno.

[ʃ] ni kikwamizwa si ghuna cha kaa kaa gumu na ufizi. Wakati kinapotamkwa ncha ya ulimi hukaribiana sana na kaa kaa gumu na ufizi. Hewa huachiliwa taratibu kupitia kando ya kaa kaa gumu.

Lugha ya Ekegusii haina sauti za [z] na [ʃ] bali [s]. Kutokana na muundo huu, wanafunzi hutamka [s] badala ya [ ] au [z] na pia hubadilisha sauti hizi kama inavyobainishwa katika mifano inayofuata.

[ʃ] =====→ [s] (Uhamishwaji wa [ʃ])

(i) {ʃ aka }: wasiwasi, kutoamini → { saka}]:kutafuta kila mahali

(ii) {zoroteʃa}: dhohofisha: haribu → {zorotesa}:halina maana

(iii) { kutoʃa}: kufikia kiwango → {kutosa}:kutumbukiza majini

[z] =====→ [s] (Uhamishwaji wa [z])

(i) {zaidi}: kupita kiasi → {saidi }: halina maana.

(ii) {tengeneza }: tengeneza ni kuboresha → {tengesa }: halina maana.

(iii) {maliza}: kukamilisha → {malisa }:halina maana.

[ʃ] =====→ [z] (uhamishwaji wa [ʃ])

(i) {juliʃa }: fahamisha → {juliza }: halina maana.

(ii) {kamiliʃa }: kutimiza → {kamiliza }:halina maana.

(iii) { elimiʃa }: kupatia elimu → { elimiza }:halina maana.

[z] =====→ [ʃ] (uhamishwaji wa [z])

(i) {zua }: zusha, buni → {ʃua }: halina maana.

(ii) {zima]: kamilifu au kufanya moto usiwake → {ʃima]: halina maana.

[s] =====→ [ʃ] (uhamishwaji wa [s])

(i) {suka}: kutengeneza nywele au vikapu: → {ʃuka}: kuteremka chini

[s] =====→ [z] (uhamishwaji wa [s])

(i) { sa: }: majira au kipimo cha wakati → { za:]: kujifungua mtoto

(ii) {sema }: kunena → {zema}:halina maana

(iii) {tosa }: tumbukiza majini → {toza } - lipisha

4.6.1.6. Sauti ya [h]

Sauti [h] ni kikwamizwa si ghuna kinachotamkiwa katika koromeo. Lugha ya Ekegusii haina sauti za kikoromeo. Kwa hivyo sauti [h] hupatikana katika Kiswahili lakini haipatikani katika Ekegusii mwanzoni na katikati ya neno. Wanafunzi Wakisii wanaojifundisha Kiswahili ama huiondoa sauti hii inapostahili au kuiongezea isipofaa inavyobainika katika mifano ifuatayo:

[h] =====→ [θ] (udondoshwaaji wa [h]

(i) { haya }: kuona aibu, kiashirii cha wingi cha ngeli Ji-Ma: → {aya}: fungu la maneno

(ii) { hatujui }: hatuelewi → {atujui }: halina maana

(iii) {hakuna } → {akuna }: halina maana.

4.6.1.7. Sauti za [l] na [r]

Katika kutamka kitambaza [l] ncha ya ulimi hujipinda na kugusa kaa kaa gumu, hewa husukumwa nje halafu huzuiwa, kisha huruhusiwa kupitia pembeni mwa kaa kaa gumu bila mkwaruzo mkubwa.

Katika kutamka kimadende [r] ncha ya ulimi hugusa ufizi na kutokana na nguvu ya hewa inayopita kati kati ya ncha hiyo na ufizi, ncha ya ulimi hupigapiga kwa haraka kwenye ufizi. Hewa hutoka kwa haraka huku kukiwa na mtetemo.

Katika muundo wa Ekegusii hakuna kitamkwa cha kitambaza [l] mwanzoni wala katikati ya neno. Wanafunzi Wakisii wanapokuwa wakijifunza Kiswahili hutumia sauti ya kimadende [r] badala ya kitambaza [l] na hivyo kubadilisha maana iliyokusudiwa ya neno.

[l] =====→ [r] (uhamishwaji wa [l])

Maana ya manenoo hubadilishwa kama inavyodhihirishwa katika mifano inayofuata:-

(i) { endelea }: kunufaika zaidi, kuzidi → { enderea}: halina maana

(ii) { lini }: kiulizi cha wakati → { rini }: halina maana

(iii) { mbali }: masafa, si karibu → {mbari }: uhusiano wa kiukoo

Wakati mwingine wanafunzi hukanganyika na hivyo hubadilishana sauti hizi mbilli na hivyo kuzua dhana ambazo hazikukusudiwa na hivyo kufanya makosa kama inavyoonyeshwa katika mifano ifuatayo:-.

[r] =====→ [l] (uhamishwaji wa [r]

Maana ya maneno hubadilika kama inavyoonyeshwa katika mifano inayofuata:-

(i) {runinga}: kifaa cha mawasiliano, kiona mbali → {luninga }:halina maana.

(ii) {rafiki]: apendwaye → { lafiki }: halina maana.

4.6.2. Hitimisho.

Katika sura hii kumedhihirishwa jinsi wanafunzi Wakisii wanavyofanya makosa ya kisarufi, kimsamiati na kimatamshi wakati wa mazungumzo. Makosa ya kisarufi yaliyobainishwa ni utozingatiaji wa ngeli za Kiswahili,vivumishi

mbali mbali na viashirii. Kumebainishwa pia matumizi yasiyofaa ya msamiati wa Kiswahili, tafsiri ya moja kwa moja kutoka Ekegusii hadi Kiswahili na matumizi ya msamiati wa Kiingereza.

Tatizo la matamshi limeshughulikiwa na kubainika jinsi wanafunzi Wakisii hutatizika wakati wanapotamka sauti za Kiswahili zisizopatikana katika Ekegusii. Nadharia ya Sifa Bainifu za Sauti imetumika kuonyesha mahali na namna ya kutamka sauti tofauti. Kadhalika, imetumika kubainisha mifanyiko mbali mbali ya kifonolojia na jinsi inavyoathiri maana ya maneno.

Sura inayofuata inabainisha jinsi makosa yaliyofanywa wakati wa mazungumzo yalivyojitokeza katika uandishi wa insha miongoni mwa wanafunzi Wakisii.

SURA YA TANO

5.0 Makosa katika uandishi wa insha kwa Kiswahili Sanifu

5.1. Makosa ya kisarufi

5.1.1 Kutozingatia ngeli

Utafiti huu umebainisha makosa ya kutozingatia ngeli za Kiswahili sanifu yaliyofanywa na wanafunzi Wakisii kwenye mtihani wa mwigo wa wilayani wa kidato cha nne. Ilibainika kwamba sawa na katika mijadala, makosa yalifanywa katika ngeli ya Kiswahili sanifu ya {N – N}. Wanafunzi walilazimisha mfumo wa ngeli za Ekegusii katika ngeli ya Kiswahili sanifu ya {N – N}.

Tofauti kubwa iliyobainika ni kwamba majina katika ngeli za Ekegusii yako katika hali ya umoja na wingi na hubadilika katika hali hizo ilhali majina yaliyo katika ngeli ya {N – N} ya Kiswahili sanifu hayabadiliki bali hufanana katika hali ya umoja na wingi. Mifano inayofuata inaonyesha tofauti hizo:

	Umoja	Wingi	Athari za Ekegusii
Ekegusii Kiswahili	ri-ruβe barua	ama-ruβe barua	 ma- barua
Ekegusii Kiswahili	e-βesa fedha	chi-βesa fedha	 mi-fedha
Ekegusii Kiswahili	eri-ogo dawa	ama-riogo dawa	 madawa
Ekegusii Kiswahili	e-retio redio	chi-retio redio	 ma- redio
Ekegusii Kiswahili	e- nyomba nyumba	chi- nyomba nyumba	 ma-nyumba
Ekegusii Kiswahili	e-nsa saa	chi-nsa saa	 ma-saa
Ekegusii Kiswahili	e-βunduki bunduki	chi- βunduki bunduki	 ma- bunduki

5.1.1.1 Kutozingatia ngeli ya { N-N }

Imedhihirishwa kwamba majina yaliyo katika ngeli ya {N-N} ya Kiswahili sanifu huwa na viambishi vya wingi katika Ekegusii. Hali hii huwakanganya wanafunzi Wakisii katika mazungumzo yao na pia wanapoandika insha kwa Kiswahili..

Kwa kujaribu kuepuka utata uliopo wanafunzi hao huanza kuyawekea maneno hayo viambishi awali katika hali ya wingi na hivyo kuvunja utaratibu wa Kiswahili sanifu kwa sababu ya athari za Ekegusii katika Kiswahili sanifu.

Yafuatayo ni makosa ya sarufi (kwa kutozingatia ngeli ya {N-N}) yaliyofanywa na wanafunzi wa kidato cha nne wilayani Kisii Kusini katika mtihani wa mwigo.

Neno (Umoja)	wingi (Kiswahili)	wingi (athari za Ekegusii)
1. barua	barua	ma-barua
2. redio	redio	ma-redio
3. fedha	fedha	mi-fedha
4. baba	baba	wa-baba
5. dada	dada	wa-dada

5.1.1.2 Ngeli ya {Ji- Ma}

Makosa machache yalionekana katika Ngeli ya {Ji- Ma} kama ifuatavyo:

Neno (Umoja)	wingi (athari za Ekegusii)	wingi (Kiswahili)
1. jiwe	ma-jiwe	ma-we
2. zuzu	wa-zuzu	ma-zuzu
3. bibi	wa-bibi	ma-bibi

5.1.2. Upatanisho wa kisarufi

Wanafunzi walifanya makosa katika upatanisho wa kisarufi ambapo walishindwa kuzingatia maendelezo sahihi ya sentensi. Wanafunzi hawa walitatizika katika kuambatanisha nomino na vitenzi kwa kuzingatia ngeli mbalimbali za Kiswahili.

Makosa haya yalitokana na athari za Ekegusii katika Kiswahili kama

inavyodhihirishwa katika sentensi zifuatazo:-

Sentensi zenye makosa	Sentensi sahihi (Kiswahili sanifu)
1. masomo inaendelea	masomo yanaendelea
2. mali yote yakateketea	mali ikateketea
3. vitu kama wembe	vitu kama nyembe
4. ambapo mahali uko	ambapo upo au mahali ulipo
5. muda zilipita	muda ulipita
6. siku ingine	siku nyingine
7. jambo ingine	jambo lingine
8. kichwa ngumu	kichwa kigumu
9. gari la polisi ilikuwa ikiija	gari la polisi lilikuwa likija

5.2.1. Vivumishi vya sifa

Makosa yalibainika katika upatanisho wa kisarufi kwa kuzingatia vivumishi vya sifa. Watahiniwa walidhihirisha jinsi walivyoathiriwa na Ekegusii hivi kwamba walishindwa kutumia vivumishi hivi vya sifa kulingana na ngeli za Kiswahili sanifu.

Yafuatayo ni makosa ya kisarufi yaliyotokana na kutozingatia ngeli wakati wa kutumia vivumishi vya sifa.

Matumizi ya sifa isivyofaa	Matumizi sahihi ya sifa
1. kichwa ngumu	kichwa kigumu
2. nini mbaya?	nini kibaya?
3. damu zito	damu nzito
4. kuku nyeusi	kuku mweusi
5. vijana vidogo	vijana wadogo
6. bahati mzuri	bahati nzuri
7. ulezi wema	ulezi mwema
8. kalamu ya maridadi	kalamu maridadi
9. kosa mbaya	kosa baya

5.2.2. Vivumishi Vimilikishi

Makosa yalibainika katika upatanisho wa kisarufi kwa kuzingatia vimilikishi. Watahiniwa walidhihirisha jinsi walivyoathiriwa na Ekegusii hivi kwamba walishindwa kutumia vimilikishi kulingana na ngeli za Kiswahili sanifu.

Yafuatayo ni makosa ya kisarufi yaliyotokana na kutozingatia ngeli wakati wa kutumia vimilikishi.

Makosa ya kisarufi	Sarufi sahihi
1. yuko na habari	ana habari
2. shoga langu	shoga yangu
3. rafiki wake	rafiki yake
4. mwenye alikuwa amelala	aliyekuwa amelala
5. vitu zake	vitu vyake
6. mabibi zao	mabibi wao
7. wako na ugonjwa	wana ugonjwa
8. mwenye ako	aliyeko/ aliyepo

5.2.3. Virejeshi

Virejeshi vilivyoshughulikiwa ni {o}, {ye}, {yo}, { cho}, {vyo}, {z},{ko}, {po}, na {mo}. Virejeshi hivi hutumika kwa kutumia kiambishi {amba } , au nafsi tatu za majina katika ngeli za Kiswahili sanifu. Ifuatayo ni mifano ya matumizi yafaayo ya virejeshi:-

1. Mtu ambaye alikuja alifukuzwa na mtoto.
2. Watu ambao walikuja walifukuzwa na watoto.
3. Mtu aliyekuja alifukuzwa na mtoto.
4. Watu waliokuja walifukuzwa na watoto.

5.2.4. Viashirii

Kiashirii ni kipashio kinachoonyesha namna kitu kilivyo au mahali kilipo. Kuna viashirii mbalimbali kulingana na nafsi za nomino na ngeli mwafaka.

Vifuatavyo ni viashirii vya nomino katika nafsi tatu ya hali ya umoja:

Nafsi ya 1 (Umoja)	Nafsi ya 2 (Umoja)	Nafsi ya 3 (Umoja)
1. huyu	huyo	yule
2. huu	huo	ule
3. hiki	hicho	kile
4. hili	hilo	lile
5. hii	hiyo	ile

Vifuatavyo ni viashirii vya namna au jinsi katika nafsi tatu ya hali ya umoja:

1. hii	hiyo	ile
2. huku	huko	kule

Vifuatavyo ni viashirii vya mahali katika nafsi tatu ya hali ya umoja:

1. huku	huko	kule
2. hapa	hapo	pale

Makosa ya kisarufi yalifanywa na wanafunzi wakati wa kutumia viashirii mbali mbali. Wanafunzi hawa walitatizika wakati wa kutumia viashirii hivi kwa kuzingatia ngeli mbalimbali za Kiswahili. Makosa haya yalitokana na athari za Ekegusii katika Kiswahili ambapo walitumia viashirii kwa kuzingatia mfumo wa Ekegusii. Yafuatayo ni makosa ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi walipotumia viashirii katika sentensi:

Makosa (Kiswahili)	athari za Ekegusii	Kiswahili sanifu
1. mtu huo	omonto oyo	mtu huyu
2. jumba hicho	rinyomba erio	jumba hilo
3. shamba ile	omogondo oria	shamba lile
4. kitendo hii	egekoro eke	kitendo hiki
5. hiyo vizazi	ekegori ekio	hicho kizazi au vizazi hivyo
6. ile gunia	egunia eria	gunia lile
7. hiyo mtu	omonto oyio	mtu huyo
8. hizo vitu	ebinto ebio	vitu hivyo
9. dirisha hiyo	etirisa eyio	dirisha hilo

10. gari hiyo omoreka oyio gari hilo

5.2.5. Viunganishi

Ilibainika katika utafiti huu kwamba wanafunzi walitumia vibaya viunganishi mbalimbali katika insha. Viunganishi vilivyowakanganya wanafunzi hao ni kama vile {na}, {ni}, {kwa}, na {katika}. Walivitumia viunganishi kwa mchanganyiko bila kujua hasa vinapopaswa kutumiwa.

5.2.5.1 Kiunganishi { na}

Sentensi zenye makosa	Sentensi sahihi
1. alimpiga na rungu	alimpiga kwa rungu
2. alitembea na mguu	alitembea kwa mguu
3. kuambukizwa na ugonjwa	kuambukizwa ugonjwa

5.2.5.2. Kiunganishi { ni}

Sentensi zenye makosa	Sentensi sahihi
1. alifika katika nyumbani	alifika nyumbani
2. tunawika katika michezoni	tunawika michezoni

5.2.5.3. Kiunganishi { kwa}

Sentensi zenye makosa	sentensi sahihi
1. alitembea kwa njia	alitembea njiani
2. alitoroka kwa jela	alitoroka katika jela / alitoroka jelani alitoroka kutoka jela
3. aliimba akiwa kwa mti	aliimba akiwa mtini
4. liko kwa mpira	liko katika mpira / liko mpirani
5. kwenda mpaka kwa dirisha	kwenda mpaka dirishani
6. nitafaulu kwa masomo	nitafaulu katika masomo

5.2.5.4 Kiunganishi { katika}

Sentensi zenye makosa	sentensi sahihi
1. alifika katika nyumbani	alifika katika nyumba
2. tunawika katika michezoni	tunawika katika michezo

5.3. Athari za Ekegusii katika matumizi ya msamiati wa Kiswahili Sanifu

5.3.1. Matumizi ya msamiati wa Ekegusii

Katika utafiti huu ilibainika kwamba wanafunzi Wakisii walitumia msamiati wa Ekegusii katika sentensi. Hali hii inadhihirisha kushabihiana kwa Ekegusii na Kiswahili hasa ikizingatiwa kuwa lugha hizi mbili ni za Kibantu. Matumizi haya ya msamiati wa Ekegusii ulitokea kwa sababu kuna maneno fulani ya Ekegusii ambayo hupatikana katika Kiswahili. Kwa hivyo kila walipoukosa msamiati mwafaka wa Kiswahili wanafunzi Wakisii walitumia msamiati wa Ekegusii wakitarajia kuwa msamiati huo ungeweza kutosheleza mahitaji ya insha.

Baadhi ya maneno yanayotumika katika Kiswahili na Ekegusii ni kama yafuatayo:-

Ekegusii	Kiswahili	Maana
- manya	-manya	-jua
- sinya	-sinya	-kinai
-chora	-chora	tengeneza picha

Hata hivyo si aghalabu maneno yapatikanayo katika Ekegusii na Kiswahili yaweze kuwa na maana sawa. Kwa mfano neno {chora} lina maana mbili katika Ekegusii yaani {kuchora picha} au {kuchagua}. Kutokana na kushabihiana kwa msamiati wa Ekegusii na Kiswahili wanafunzi walitatizwa katika matumizi ya msamiati kama inavyodhihirika katika sentensi zifuatazo:

1. Walimkecha sana kwa sababu ya kumuua James.

   Neno {kecha} humaanisha chukia kwa Ekegusii

   Neno hili si la Kiswahili. Kwa hivyo sentensi hiyo haileweki na haina maana katika Kiswahili. Sentensi sahihi ingekuwa ifuatavyo:

   " Walimchukia sana kwa sababu ya kumuua James"

2. Moyo ulitumatuma niliposikia kelele

{tumatuma} lina maana ya {kuruka ruka}katika Ekegusii lakini halina maana katika Kiswahili.

Sentensi sahihi ingekuwa ifuatavyo:

" Moyo ulinidundadunda niliposikia kelele.''

3. Tunahitaji makao {mange} kwa wagonjwa wa ukimwi

Neno {-mange} katika Ekegusii lina maana ya mengi lakini halina maana katika Kiswahili.

Sentensi sahihi ingekuwa, kama ifuatavyo

" Tunahitaji makao mengi ya wagonjwa wa ukimwi."

4. Aligaragara chini alipopigwa kwa rungu.

Neno {-garagara} katika Ekegusii lina maana ya {- gaagaa}lakini halina maana katika Kiswahili.

Sentensi sahihi ingekuwa,

"Aligaagaa chini alipopigwa kwa rungu.''

5 Kijana huyo alikuwa {mchege} sana darasani

Neno la Ekegusii {mchege} lina maana ya {mchokozi} katika Ekegusii lakini halina maana katika Kiswahili.

Sentensi sahihi ingekuwa.

" Kijana huyo alikuwa mchokozi sana darasani."

6. Aliposikia askari wakija alianza {kuchanga mbio} kwenda msituni.

Kwa Ekegusii {gochanga chimbero} ni { kukimbia mbio }kwa kasi.

Hapa neno {kuchanga mbio} limetumiwa kimakosa na halileti maana iliyokusudiwa katika Kiswahili. Zifuatazo ni sentensi sahihi:

"Aliposikia askari wakija alianza kukimbia mbio kwenda msituni"

"Aliposikia askari wakija alianza kuchana mbuga kwenda msituni"

"Aliposikia askari wakija alikimbia kwa kasi kwenda msituni"

7. Walipoona amekufa pipipi! waliondoka wakiimba kwa vigelele.

Katika Ekegusii {pipipi!} ni mlio unaonyesha kukamilika, kufikia mwisho kabisa au kwisha kabisa. Mlio huu hauna maana yoyote katika Kiswahili. Zifuatazo ni sentensi sahihi :

(a) "Walipoona amekufa kabisa waliondoka wakiimba kwa vigelele."

(b) "Walipoona amekufa fofofo waliondoka wakiimba kwa vigelele."

8. Wanajaribu{kuhaka} vidonda dawa lakini haviponi.

Neno {kuhaka} linatokana na neno la Ekegusii {goaka} ambalo lina maana ya {kupaka}.

Kwa hivyo sentensi sahihi ni "Wanajaribu kuvipaka vidonda dawa lakini haviponi."

5.3.2. Tafsiri kutoka Ekegusii hadi Kiswahili

Wanafunzi walifanya makosa ya msamiati walipotafsiri dhana fulani kutoka katika Ekegusii hadi Kiswahili. Ifuatayo ni mifano ya makosa hayo:

Sentensi zenye athari za Ekegusii	Ekegusii	Kiswahili sanifu
1. maneno mengi yametokea hivi karibuni.	amang'ana amange aβeire βwango iga.	mambo mengi yametokea hivi karibuni.
2. alitoa maneno yake yote kabla ya kufa.	agakwana amang'ana aye onsi atarakwa.	alitoa maelezo yake yote kabla ya kufa.
3. mafikirio yakaniingia nilipokuwa njiani.	eβirengererio bigansoa ekero narenge incchera.	fikra zikanijia nilipokuwa njiani.
4. "siku moja jua lilichomoza kutoka sehemu isiyo ya kuamini"	rituko erimo βogakia βoβe.	siku moja kulikucha vibaya.
5. alikuwa amebakiza moyo.	konyora otigairie enkoro	alikuwa akitoa pumzi za mwisho.
6. wakampigia chini	βakamwakera inse ase	wakamwangusha chini

kwa hasira.	oβororo.	kwa hasira.
7. alifungwa miaka isiyo ya hesabu	agasiβwa emiaka etari koβareka.	akafungwa miaka mingi.
8. aliuliza maswali yasiyokuwa na miguu.	akaβoria amaβorio ataβwati amagoro.	aliuliza maswali yasiyo na maana.

5.3.3. Matumizi ya msamiati wa Kiswahili kimakosa.

Katika kazi hii, makosa ya matumizi mabaya ya msamiati wa Kiswahili yaliyofanywa na wanafunzi Wakisii katika mtihani wao wa mwigo wa wilayani yamebainishwa.

Matumizi yasiyo sahihi ya msamiati	Matumizi sahihi ya msamiati
1. ukimwi umezorotesha maendeleo nyuma	ukimwi umezorotesha maendeleo
2. watu wameonywa wawe na taathira ya kukomesha ugonjwa	watu wameonywa wawe na tahadhari ya kukomesha ugonjwa
3. alilala usingizi wa pono	alilala usingizi pono
4 alichomwa sindano, kisu, mshale, mkuki	kudungwa sindano / kisu, kufumwa mshale / mkuki
5. watalipa malipo duni shuleni	watalipa malipo nafuu shuleni
6. alienda shule ilhali atafute mbinu za kupora mali	alienda shuleni ili apate mbinu za kupora mali
7. watu wengi wamegonjeka	watu wengi wameugua
8. alimkumbatia akitaka kumpiga	alimkaba akitaka kumpiga
9. tulienda kuchukua staftahi	tulienda kula / kunywa, staftahi
10. wanaendelea kuchafua mazingara	wanaendelea kuchafua mazingira

5.3.4. Matumizi ya msamiati wa Kiingereza

Katika utafiti huu ilibainika kwamba wanafunzi walitumia msamiati wa Kiingereza uliotoholewa moja kwa moja hata ambapo Kiswahili kina msamiati wa kujitosheleza.

Hali hii inaonyesha udhaifu na kutomakinika kwa wanafunzi hao katika matumizi mwafaka ya msamiati wa Kiswahili. Msamiati wa Kiingereza uliotoholewa moja kwa moja ambao waliutumia wanafunzi ni kama ufuatao:

Msamiati wa Kiingereza uliotoholewa	Kiswahili sanifu
1. Silesi ya mkate	kipande cha mkate
2. Hedimasta	mwalimu mkuu
3. Televisioni	runinga / televisheni
4. Lokesheni	tarafa
5. Marisiti	stakabadhi
6. Posta zenye picha	mabango yenye picha
7. gonolia	kisonono
8. Sivilisi	kaswende
9. labaratoria	mahabara
10. Geti ya shule	lango la shule
11. Stetimenti	arifa / taarifa
12. Sueta	fulana / sweta

Pia ilibainika kwamba wanafunzi walitumia msamiati wa Kiingereza moja kwa moja hali inayodhihirisha kutomakinika kwao katika Kiswahili. Ufuatao ni msamiati wa Kiingereza uliotumiwa:-

Kiingereza	Kiswahili
1. Machine	mtambo uliharibika / mashine
2. Gate	lango
3. Bus ya abiria	basi la abiria
4. Alipigwa fine	alitozwa faini
5. Office yake	afisi / ofisi yake
6. Station ya polisi	kituo cha wanausalama / polisi

7. Condom mipira ya kuzuia magonjwa zinaa au mimba.
8. Police walimshika askari / polisi walimshika

Kadhalika, wanafunzi walitumia msamiati usiofahamika. Yafuatayo ni maneno yaliyoandikwa ambayo hayana maana yoyote katika Kiswahili sanifu.

(i) kitembo (ii). Istaii (iii) ghadhada
(iv) sayanyi (v) ponga

5.3.5 Matumizi yasiyofaa ya tamathali za lugha ya Kiswahili

Wanafunzi walitumia tamathali za lugha kwa kutafsiri moja kwa moja kutoka Ekegusii hadi Kiswahili. Hali hii inaleta utata hasa kwa wale wasiojua lugha ya Ekegusii na kuwafanya wasielewe kikamilifu maana ya tamathali hizi.

Wanafunzi walitumia tamathali za lugha ya Kiswahili kimakosa na kusababisha utata kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:-

Makosa ya kisarufi	Kiswahili sahihi
1. dawa ya mto ni mto	dawa ya moto ni moto
2. mti mkubwa ukiagwa wanandege huyumba	mti mkubwa ukianguka wanandege huyumba
3. aliye kando hangiwi na mtu	aliye kando haangukiwi na mti
4. kuenda homo marejeo ni ngamani	mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani
5. umoja ni ndugu	umoja ni nguvu

5.4. Makosa ya kitahajia katika uandishi wa insha.

Utafiti huu unabainisha makosa ya kitahajia yanayofanywa na wanafunzi Wakisii wakati wanapoandika insha kwa Kiswahili sanifu.. Walifanya makosa hayo hasa katika fonimu ambazo hazipatikani katika Ekegusii lakini zipo katika Kiswahili.

5.4.1 Fonimu za Ekegusii na Kiswahili

5.4.1.1 Fonimu za Ekegusii.

Katika sehemu ya **4.3.1** hadi **4.3.2** inabainika kwamba Ekegusii kina sauti chache kuliko Kiswahili. Pia inabainika kwamba sauti ambazo haziko katika muundo wa Ekegusii huwatatiza wanafunzi Wakisii wanapozitamka. Matokeo ya utata huu ni kwamba wanafunzi hao hutamka sauti tofauti na zile zinazotarajiwa na hivyo kuleta maana tofauti na iliyokusudiwa.

Utata wa kuzitambua na kuandika sauti za Kiswahili ambazo hazimo kwenye muundo wa Ekegusii ulibainika katika uandishi wa insha. Wanafunzi Wakisii waliandika kwa kutumia fonimu za sauti walizoweza kutamka. Fonimu za konsonanti zinazopatikana katika Ekegusii ni / β , m , t , s , n , č, r , k , g , , ŋ , w na j , /. Fonimu hizi za konsonanti zinaweza kuwasilishwa katika jedwali kama ifuatavyo:

	midomo	midomo meno	menoni	ufizi	kaa kaa gumu	kaa kaa laini
vipasuo				t	č	k g
vikwamizo	β			s		
ving'ong'o	m			n		∩ ŋ
vimadende					r	
viyeyusho	w				j	

Katika muundo wa Ekegusii fonimu / b / na / d / hazitumiki mwanzoni mwa neno lolote wala hazitumiwi katikati ya irabu. Fonimu / b / hutumiwa baada ya fonimu / m / peke yake na kuwa / mb / na fonimu / d / hutumiwa baada ya fonimu / n / peke yake na kuwa / nd /.

5.4.1.2. Fonimu za Kiswahili

Kulingana na Mbaabu (1985) na King'ei na Musau (2002:3) Lugha ya Kiswahili ina konsonanti ishirini na tano ambazo huunda fonimu zifuatazo / p, b, č, ɟ, t, d, θ, ð, f, v, g ,ɣ, h, k, l , m , n, ŋ, r, s, z, ʃ, w, j./

5.4.1.3. Tatizo la kitahajia.

Kama ilivyodhihirika hapo juu Ekegusii kina sauti chache kuliko Kiswahili. Kutokana na upungufu huu wanafunzi Wakisii hupata utata wanapokuwa wakijifunza na kukitumia Kiswahili sanifu. Hata baada ya kujifunza na kujua fonimu kadha za Kiswahili, wanafunzi hawa hutatizika wanapokuwa wakipambanua na kuandika dhana fulani fulani. Kutotumia kisahihi baadhi ya fonimu za Kiswahili sanifu husababisha makosa katika uandishi wa maneno ya Kiswahili kwa wanafunzi Wakisii.

5.5. Makosa ya kitahajia katika insha za wanafunzi

Sehemu hii inashughulikia matatizo ya kitahajia yanayotokana na ukosefu wa fonimu kadhaa za Kiswahili katika muundo wa Ekegusii. Kama ulivyojitokeza utata wa kutamka konsonanti fulani za Kiswahili (4.6. hadi 4.6.7.1.) wanafunzi Wakisii walipata utata wa kuandika tahajia sahihi ya fonimu za sauti za Kiswahili ambazo hazipatikani katika muundo wa Ekegusii.

5.5.1. Fonimu za / b / na / P /

Wanafunzi Wakisii walipata utata wa kuzitambua na kuandika fonimu za / b / na / P / ilivyostahili. Walifanya makosa ya kuhamisha fonimu moja hadi nyingine na kupotosha maana iliyokusudiwa ya maneno au hata kuandika maneno yasiyokuwa na maana. Utata huu ulitokea kwa sababu katika Ekegusii sauti ghuna ya [b] hudhoofika na kuwa sauti si ghuna ya [p]. Wanafunzi waliandika jinsi walivyotamka sauti hizi.

/ b / ======→ / p / (kudhoofishwa [b] na kuwa [p] na hatimaye kuandikwa hivyo hivyo.

	(Neno)	maandishi ya kifonetiki	maana
(i)	/ bure /	[burɛ]	- bure ni bila kitu
	/pure /	[purɛ]	- punje ya nafaka
(ii)	/ bara /	[bara]	- bara ni sehemu ya ndani ya nchi

/ para / [para] - para ni mstari

(iii) / bora / [bora] - ni zuri sana
/ pora / [pora] - ni nyang'anya kwa nguvu

(iv) / baada / [ba:da] - ni nyuma ya
/ paata / [pa:ta] - halina maana

Fonimu za / b / zilibadilishwa na kuwa / p /, na hivyo kubadilisha maana iliyokusudiwa ya maneno yaliyotumika. Makosa ya kitahajia yalitokea wanafunzi walipokosea kuandika maneno yaliyokusudiwa. Matokeo ni kwamba tuzo zao zilipungua na kusababisha matokeo mabaya.

Pia fonimu za / p / ziliandikwa zikibadilishana na za / b /. Hii inatokana na mfanyiko wa kiisimu ambapo sauti si ghuna ya [p] huongezwa nguvu na kutamkwa kama sauti ghuna ya [b]. Wanafunzi waliandika walivyotamka sauti za [p] zilizoongezwa nguvu.Mifano ifuatayo inaonyesha utata huu.

/ p / =======→ / b / (kuongezewa nguvu kwa [p])

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) / paka /	[paka]	- aina ya mnyama: weka rangi
/ baka /	[baka]	- shikilia kwa nguvu
(ii) / tapakaa /	[tapaka:]	- sambaa ovyo
/ tabakaa /	[tabaka:]	- haina maana
(iii) / pungia /	[puŋg ia]	- aga watu kwa kupeperusha mkono.
/ bungia /	[buŋgia]	- halina maana

5.5.2. Fonimu za / d /, / θ /, / ð /

Mifano inayofuata inaonyesha makosa ya kitahajia yaliyofanywa na wanafunzi Wakisii katika uandishi wa insha kwa kutumia fonimu za / d /, / θ /, / ð /. Makosa haya yalitokana na mifanyiko ya kifonolojia ambapo, ama sauti ghuna zilidhoofishwa na kutamkwa kama sauti si ghuna au sauti si ghuna zikaongezewa

nguvu na kutamkwa kama sauti ghuna. Wanafunzi waliandika walivyotakma sauti mbali mbali na hivyo kufanya makosa ya kitahajia ambayo yalipoteza maana iliyokusudiwa ya maneno.

/ d / ====→ / t / (udhoofishwaji wa [d])

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) damu	[damu]	- maji maji mekundu ya mwili yenye uhai
tamu	[tamu]	- enye ladha nzuri
(ii) daka	[daka]	- shika kwa ghafla
taka	[taka]	- hitaji: uchafu
(iii) dawa	[dawa]	- kiponyeshacho,au kuondoa maumivu
tawa	[tawa]	- halina maana

/ ð / ====→ / t / (udhoofishwaji wa [ð])

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) dhambi	[ðambi]	- maasi au kutenda kinyume cha shera
tambi	[tambi]	- aina ya nafaka, vitambaa vya kuwashia taa
(ii) kadhaa	[kaða:]	- idadi isiyojulikana
kataa	[kata:]	- tokubali

/ð / ====→ / θ / (udhoofishwaji wa [ð])

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) dhani	[ðani]	- kisia
thani	[θani]	- halina maana

(ii) tahadhari [tahaðari] - jikinga

tahathari [tahaθari] - halina maana

5.5.3. Fonimu za / f / na / v /

Wanafunzi walifanya makosa ya kitahajia wakati walipotumia fonimu za / f / na / v / ambapo walizitumia kwa kubadilishana kwa sababu ya kutokuwa na uhakika wa kuzitumia inavyotakikana. Mifano inayofuata inabainisha makosa hayo.

/ v / ====→ / f / (kudhoofishwa kwa [v])

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) vaa	[va:]	- tia nguo / viatu mwilini / miguuni
faa	[fa:]	- tosheleza, - nayopasa
(ii) vipande	[vipande]	- sehemu ndogo ndogo
fipande	[fipande]	- halina maana

/ f / ====→ / v / (kuongezwa nguvu kwa [f])

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) fika	[fika]	- ni kuwadia
vika	[vika]	- ni kuvalisha
(ii) kufuli	[kufuli]	- kifaa cha kufungi mlango
kuvuli	[kuvuli]	- halina maana

5.5.4. Fonimu ya / ɣ /

Hii ni mojawapo ya fonimu ambazo hupatikana katika Kiswahili lakini si katika Ekegusii. Wanafunzi walifanya makosa ya kitahajia katika insha zao mahali fonimu hii ilipohitajika.

/ ɣ / ====→ / g / (kudhoofishwa kwa [ɣ])

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) faragha	[faraɣa]	-a siri
faraga	[faraga]	- halina maana
(ii) ghulamu	[ɣulamu]	- mvulana.
gulamu	[gulamu]	- halina maana
(iii) ghala	[ɣala]	– mahali pa kuhifadhia vitu
gala	[gala]	- halina maana

5.5.5. Fonimu ya / h /

Sauti ya koromeo ya [h]haipo katika Ekegusii. Katika utafiti huu ilibainika kwamba wanafunzi walifanya makosa ya kitahajia kwa kutotumia fonimu za sauti hii. Walipata utata wakati wa fonimu ya sauti hii katika hali ya kukanusha au katika wakati unaoendelea hali ya kawaida. Pia wanafunzi hawa walitumia fonimu / h / mahali isipotakikana na kuzua dhana ambazo hazikuwa zinakusudiwa. Mifano ifuatayo inathibitisha utata huo.

/ h / ====→ / Ø / (kudondoshwa kwa [h])

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) hakugundua	[hakugundua]	- hakujua
akugundua	[akugundua]	- halina maana
(ii) halali	[halali]	- jambo la haki au sawa sawa
alali	[alali]	- halina maana
(iii) haraka	[haraka]	- upesi
araka	[araka]	- halina maana

Wanafunzi walifanya makosa ya kuchopeka sauti [h] mahali pasipofaa na hivyo kusababisha utata wa maana iliyokusudiwa. Mifano ifuatayo inadhihirisha utata huu.

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) au	[au]	badala ya , labda
hau	[hau]	halina maana.
(ii) mikoa	[mikoa]	sehemu za utawala katika taifa kubwa kuliko wilaya
mikoha	[mkoha]	halina maana

5.5.6. Fonimu za sauti [č] na [ʄ].

Kama ilivyoelezwa awali, lugha ya Ekegusii haina kizuio-kwamiza ghuna [ʄ]. Wanafunzi Wakisii hupata utata wakati wanapotumia fonimu ya sauti hii. Badala ya kutumia fonimu / ʄ / hutumia/ č /. Mara nyingine wanafunzi hao hutumia sauti zote zikibadilishana kimakosa na kusababisha makosa ya kitahajia. Tatizo hili linatokana na mifanyiko ya kifonolojia ambapo kizuio-kwamiza ghuna [ʄ] hudhoofishwa na kutamkwa kama kizuio-kwamiza si ghuna [č].

/ ʄ / ====→ / č/ (udhoofishwaji wa [ʄ]

Neno	ya kifonetiki	maana
(i) kuja	[kuʄa]	- kurejea, kufika
kucha	[kuča]	- kupambazuka: sehemu ya mkono au mguu yenye makali
(ii) nje	[nʄe]	- siyo ya ndani
nche	[nče]	- halina maana

/ č / ====→ / ʄ / (uongezwaji wa nguvu wa [č]

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) mchana	[mčana]	- kati kati ya siku

mjana	[mʄana]	- halina maana
(ii) chongo	[čongo]	-enye jicho moja lisiloona
jongo	[ʄongo]	– halina maana

5.5.7. Fonimu za / l / na / r /

Kama ilivyoelezwa awali lugha ya Ekegusii haina kitambaza si ghuna [l]. Hivyo, wanafunzi Wakisii hukanganyika wanapotumia fonimu ya sauti hii. Badala kitambaza si ghuna / l / hutumia sauti ya kimadende / r /. Hali kadhalika wanafunzi hao hutumia fonimu ya kitambaza / l / badala ya fonimu ya kimadende / r / na kufanya makosa ya kitahajia. Mifano ifuatayo inabainisha utata huu.

/ l / ====→ / r / (uhamishwaji wa [l])

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) aila	[aila]	ukoo
aira	[aira]	halina maana
(ii) ajali	[aʄali]	mkasa, bahati mbaya, balaa
ajari	[aʄari]	halina maana

/ r / ====→ / l / (uhamishwaji) wa [r]

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) rungu	[ruŋgu]	- kifaa kinachochongwa kutokana na mti
lungu	[luŋgu]	- halina maana
(ii) karo	[karo]	- ada, malipo
kalo	[kalo]	- halina maana

5.5.8. Fonimu za / s /, / ʃ / na / z /

Lugha ya Ekegusii ina sauti ya [s] lakini haina sauti za [ʃ] na [z]. Kutokana na ukosefu huu wanafunzi Wakisii hupata utata wanapotakiwa kutumia fonimu za sauti hizi mbili. Katika uandishi wao huzitumia kimakosa ambapo huzitumia kwa kubadilishana au kutumia / s / pekee. Pia mara nyingine hutumia moja yao mahali ambapo / s / inatakiwa kutumiwa. Utata huu wa uhamishaji wa sauti fulani hadi nyingine kimatamshi yalijitokeza wakati wanafunzi walitumia fonimu kimakosa. Hivyo walibadilisha maana iliyokusudiwa au kuzua neno lisilo katika Kiswahili sanifu ambalo huwa halina maana yoyote. Mifano ifuatayo inaonyesha utata huu.

/ ʃ / ====→ / s / (uhamishwaji wa [ʃ]

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) sheria	[ʃeria]	- utaratibu wa kufuatwa
seria	[seria]	- halina maana
(ii) shangaa	[ʃaŋga:]	-duwaa, shikwa na bumbuazi
sangaa	[saŋga:]	- kusimama kwa gari kwa muda

[ʃ] ====→ / z / (uhamishwaji [ʃ]

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) rembesha	[rembeʃa]	- fanya maridadi
rembeza	[rembeza]	- halina maana
(ii) lisha	[liʃa]	- patia chakula
liza	[liza]	- fanya kulia

/ z / ====→ [ʃ] (uhamishwaji [ʃ]

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) zika	[zika]	- fukia ardhini
shika	[ʃika]	- kamata

/ z / ====→ / s / (uhamishwaji wa [z]

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana ya neno
(i) poteza	[poteza]	- elekeza vibaya, potosha.
potesa	[potesa]	- halina maana
(ii) tazama	[tazama]	- angalia
tasama	[tasama]	- halina

/ s / ====→ / ʃ / (uhamishwaji wa [s]

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) msaada	[msa:da]	- usaidizi
mshaada	[mʃa:da]	- halina maana

/ s / ====→ / z / (uhamishwaji wa [s]

Neno	maandishi ya kifonetiki	maana
(i) pangusa	[paŋgusa]	- ondoa uchafu
panguza	[paŋguza]	- halina maana
(ii) anasa	[anasa]	- upotovu, starehe mbaya
anaza	[anaza]	- halina maana

SURA YA SITA

6.0 MATOKEO YA UTAFITI

Katika sura ya tatu vipengele mbali mbali vya lugha za Ekegusii na Kiswahili vililinganishwa kwa kufuata misingi ya Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi. Ulinganishaji huu ulitoa mwongozo wa kutambua vipengele tofauti vya lugha hizi ambavyo huleta utata miongoni mwa wanafunzi Wakisii.

Katika sura ya nne makosa ya kisarufi, kimsamiati na kimatamshi yaliyofanywa na wanafunzi Wakisii katika mijadala yamebainishwa na kuainishwa. Sura ya tano imebainisha makosa ya kisarufi, kimsamiati na kitahajia yaliyofanywa na wanafunzi wakisii katika insha walizoandika katika mtihani wa mwigo wa wilayani. Makosa ya kisarufi, kimsamiati na kitahajia katika mijadala na uandishi wa insha yamebainishwa na kuainishwa kwa kufuata misingi ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Sura hii ya sita inachanganua na kufafanua jinsi makosa yaliyofanywa na wanafunzi Wakisii katika mijadala yalivyojitokeza katika uandishi wa insha. Inadhihirishwa pia jinsi makosa hayo ya kisarufi, kisamiati na kitahajia yalivyochangia matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili kwa wanafunzi Wakisii wa kidato cha nne wilayani Kisii Kusini.

6.1 **Makosa katika mijadala**

Kama ilivyodhihirishwa katika sura ya tatu, wanafunzi walifanya makosa mbali mbali ya kisarufi,matumizi ya msamiati na matamshi. Jedwali lililopo hapa chini linadhihirisha kiwango cha makosa yaliyokusanywa katika kila kitengo kutoka shule kumi na tano zilizohusishwa.

Jedwali (iv) ***Makosa katika mijadala***

shule	Idadi ya wanafunzi	Makosa ya sarufi	Makosa ya msamiati	Makosa ya matamshi	Jumla ya Makosa kwa kila shule	wasta ni
A	10	11	4	67	82	8.2
B	6	16	8	38	62	6.2

C	10	16	12	55	83	8.3
D	10	13	6	71	90	9
E	10	19	6	47	72	7.2
F	10	11	3	39	53	5.3
G	10	4	1	26	31	3.1
H	10	11	3	34	48	4.8
I	10	14	1	3	18	1.8
J	10	21	3	23	47	4.7
K	10	24	5	45	74	7.4
L	10	13	1	35	49	4.9
M	10	15	2	51	68	6.8
N	10	18	5	10	33	3.3
P	10	13	2	23	38	3.8
Jumla	146	219	62	567	848	5.8
Asili-mia	100%	25.8%	7.3%	66.9%	100%	

6.1.1. Wastani wa makosa kwa kila kitengo katika mijadala

Jedwali (d) linaonyesha viwango vya makosa yaliyofanywa na wanafunzi katika mazungumzo kwenye mijadala waliyotayarishiwa. Viwango hivyo ni kama vifuatavyo:

Jumla ya makosa ya sarufi yaliyofanywa na wanafunzi 146 ni 219 ambapo ni wastani wa kosa 1.5 kwa kila mwanafunzi.

Jumla ya makosa ya msamiati yaliyofanywa na wanafunzi 146 ni 62 ambapo ni wastani wa makosa 0.4 kwa kila mwanafunzi.

Jumla ya makosa ya kihija yaliyofanywa na wanafunzi 146 ni 567 ambapo ni wastani wa makosa 3.8 kwa kila mwanafunzi.

Kwa jumla wastani wa makosa ya wanafunzi ni 5.8 kwa kila mwanafunzi.

6.1.2. Mchango wa makosa kwa kila kitengo katika mijadala

Makosa ya kimatamshi yalichangia kwa asilimia 66.9 katika makosa yote.

Makosa ya sarufi yalichangia kwa asilimia 25.8 katika makosa yote.

Makosa ya msamiati yalichangia kwa asilimia 7.3 katika makosa yote.

Kutokana na matokeo haya, inabainika kwamba wanafunzi waliohusishwa katika mijadala walikuwa na matatizo mengi katika matamshi yakifuatiwa na yale ya kisarufi na hatimaye ya msamiati. Jambo lililojitokeza ni kwamba licha ya kuwa wanafunzi waliohusika katika mijadala walichaguliwa kwa kutumia mtindo wa bahati na sibu, wazungumzaji wengi walichukua muda mfupi sana (badala ya dakika tano walizopewa) kuwasilisha hoja zao. Bila shaka walifanya hivyo ili kuepuka kufanya makosa mengi.

Mbinu ya kutumia mazungumzo (katika mijadala) haikuweza kubainisha ujuzi kamili wa wanafunzi katika Kiswahili sanifu. Hivyo kulihitajika mbinu bora zaidi ambayo ni uandishi wa insha. Wanafunzi huwa na fursa ya kufikiria kwa makini kabla ya kuandika mawazo yao bila wasi wasi kama ilivyojitokeza katika mijadala.

Insha za wanafunzi zilipatikana katika kituo cha usahihishaji wa mtihani wa kidato cha nne wa mwigo wilayani Kisii Kusini. Wakati huu kituo cha kusahihishia mtihani kilikuwa katika shule ya upili ya Serikali ya wasichana ya Sengera.

6.1.3 Makosa katika uandishi wa insha

Jedwali (e) linabainisha kiwango cha makosa yaliyokusanywa kutoka katika insha za watahiniwa wa kidato cha nne kwenye mtihani wa mwigo kutoka shule kumi na tano wilayani Kisii Kusini.

Jedwali (v) ***Makosa katika insha***

shule	Idadi ya wana-funzi	Makosa ya sarufi	Makosa ya msamiati	Makosa ya tahajia	Jumla ya Makosa kwa kila shule	wastani
A	10	68	17	106	191	19.1
B	6	58	26	147	231	38.5

C	10	32	25	138	195	19.5
D	10	57	34	181	272	27.2
E	10	32	27	147	206	20.6
F	10	67	33	193	293	29.3
G	10	50	25	102	177	17.7
H	10	50	27	119	196	19.6
I	10	35	30	105	170	17
J	10	63	20	98	181	18.1
K	10	56	17	215	288	28.8
L	10	68	28	58	154	15.4
M	10	59	42	162	263	26.3
N	10	56	28	194	278	27.8
P	10	50	26	126	202	20.2
Jumla	146	801	405	2,091	3,297	22.58
Asili-mia	100%	24.3	12.3	63.4	100%	

6.2. Wastani wa makosa

6.2.1 Wastani wa makosa kwa kila kitengo katika insha

Jedwali (e) linaonyesha viwango vya makosa yaliyofanywa na wanafunzi katika uandishi wa insha. Viwango hivyo ni kama vifuatavyo:

Jumla ya makosa ya sarufi yaliyofanywa na wanafunzi 146 ni 801 ambapo ni wastani wa makosa 5.5 kwa kila mwanafunzi.

Jumla ya makosa ya msamiati yaliyofanywa na wanafunzi 146 ni 405 ambapo ni wastani wa makosa 2.8 kwa kila mwanafunzi.

Jumla ya makosa ya kihijai yaliyofanywa na wanafunzi 146 ni 2,091 ambapo ni wastani wa makosa 14.3 kwa kila mwanafunzi.

Wastani wa makosa ya wanafunzi ni 22.6 kwa kila mwanafunzi.

6.2.2. Mchango wa makosa kwa kila kitengo katika insha

Makosa ya kimatamshi yalichangia kwa asilimia 66.9 katika makosa yote.

Makosa ya sarufi yalichangia kwa asilimia 25.8 katika makosa yote.

Makosa ya msamiati yalichangia kwa asilimia 7.3 katika makosa yote.

Wanafunzi walidhihirisha kwa kikamilifu ujuzi wao wa Kiswahili sanifu katika uandishi wao wa insha. Ni katika insha ambapo makosa mengi yalibainika tahajia yakifuatiwa na ya sarufi na hatimaye ya msamiati.

6.2.3. Matamshi na hijai

Kulingana na matokeo ya jumla, kunadhihirika uhusiaano wa karibu sana uliopo kati ya matamshi na hijai

Matamshi yalichangia kwa asilimia kubwa sana (66.9) katika makosa yote jumla kwenye mijadala. Hijai nayo ilichangia kwa asilimia kubwa (63.4) ya makosa makosa yote katika insha.

Kutokana na matokeo haya mtafiti amethibitisha kwamba, kwa kiwango kikubwa, watahiniwa waliandika jinsi walivyotamka.

Mifano ifuatayo inadhihirisha madai haya:

Makosa	Kiswahili sanifu	Makosa	Kiswahili sanifu
1. senyewe	zenyewe	2. shihada	ziada
3. lasima	lazima	4. tokesha	tokeza
5. potesa	poteza	6. fukusa	fukuza
7. surura	zurura	8. wisala	wizara
9. singatia	zingatia	10. sungumsia	zungumzia

Kuna makosa ya sarufi na msamiati yaliyofanywa na wanafunzi wakati wa mijadala na ambayo yalijitokeza tena katika insha. Ifuatayo ni mifano ya makosa hayo:

Makosa ya sarufi	Kiswahili sanifu
1. madhara kubwa	madhara makubwa
2. huko ni mbaya	huko ni kubaya
3. tunazo mahindi	tuna (yo) mahindi

4. vijana yetu — vijana wetu
5. wake zao — wake wao
6. ng'ombe ya.... — ng'ombe wa...
7. -ako na — -ana
8. askari yangu — askari wangu

Jambo lililobainika wazi hapa ni kwamba athari za lugha ya kwanza katika matamshi ya lugha ya pili hudhihirika pia katika tahajia wakati wa kuandika insha katika lugha hiyo ya pili. Jambo hili lilithibitika wakati athari za lugha ya Ekegusii katika matamshi ya Kiswahili sanifu zilidhihirika katika hijai wakati wa kuandika insha kwa Kiswahili sanifu.

Aidha, kama ilivyoelezwa, makosa ya sarufi na msamiati yanayofanywa na wanafunzi wanapokuwa wakizungumza wakati wa mijadala hujitokeza katika insha zao. Kwa hivyo, utafiti huu unathibitisha kuwepo tatizo lililokuwa likishughulikiwa.

6.3. Hitimisho na mapendekezo

6.3.1. Hitimisho

Utafiti huu umeshughulikia athari za Ekegusii katika Kiswahili na jinsi athari hizi zinavyochangia matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili wa kidato cha nne kwa wanafunzi Wakisii wilayani Kisii Kusini.

Athari za Ekegusii ambazo zilishughulikiwa ni katika vitengo vya sarufi, msamiati na hijai. Matokeo yamebainisha kwamba wanafunzi Wakisii wilayani Kisii Kusini wameathiriwa na lugha yao ya kwanza hivi kwamba athari hizo hujitokeza sana wanapokuwa wakizungumza na hata wanapoandika. Matokeo ya tatizo hili ni kupoteza tuzo nyingi wakati insha zao zinaposahihishwa hali inayosababisha wapate alama duni na hatimaye matokeo kuwa mabaya kote wilayani.

Ingawa kuna uwezekano wa kuwepo sababu zingine tofauti zinazokuwa zinachangia matokeo haya mabaya, utafiti huu umejikita katika eneo la isimu ambapo pia umeshughulikia vitengo vya sarufi, msamiati na kihijai.

6.3.2. Mapendekezo.

Utafiti huu umethibitisha kwamba athari za Ekegusii katika Kiswahili zinachangia matokeo mabaya ya mtihani wa Kiswahili wa kitaifa kwa wanafunzi Wakisii wa kidato cha nne wilayani Kisii Kusini.

Athari hizi zimekithiri katika hijai, sarufi na msamiati zikifuatana hivyo. Ili kurekebisha hali hii na kuboresha matokeo ya somo hili na kukikuza Kiswahili wilayani Kisii na kwingineko nchini Kenya mtafiti anatoa mapendekezo yafuatayo:-

Wataalamu wa Kiswahili waandike vitabu vingi vitakavyozingatia zaidi hijai, sarufi na msamiati. Wanafunzi wakiwa mahiri katika vitengo hivi muhimu sana wataweza kuandika insha bora ambazo zitawapa tuzo za juu na hatimaye wapate alama bora katika mitihani ya Kiswahili.

Wanafunzi wapewe mazoezi mengi katika mazungumzo (mijadala) na uandishi wa insha. Wanafunzi waepuke kutumia lugha yao ya kwanza (Ekegusii) katika mawasiliano yao kama wakati wa michezo, mapumziko na shughuli nyinginezo. Matumizi ya Kiingereza katika masomo mengi na shughuli nyinginezo yalionekana kuchangia kutozingatiwa kwa Kiswahili sanifu. Matumizi ya Ekegusii yaliongoza kwa sababu wanafunzi takribani 99.9% yakifuatiwa na Kiingereza ilhali Kiswahili kilipewa nafasi ya mwisho.

Tume ya kuwaajiri walimu iwapeleke walimu waliohitimu wa jamii zingine za Kenya katika wilaya hii. Walimu hawa wanaweza kuyakabili matatizo yaliyotajwa hapo juu ambayo huathiri vibaya matokeo ya wanafunzi Wakisii katika mtihani wa kitaifa wa Kiswahili katika kidato cha nne na kuendelea katika masomo ya juu.

M A R E J E L E O

Ashton E.O. (1944), Swahili grammar, Longman, Nairobi.

Besha, R.M. (1991)."*The acquisition of Swahili by adult Maasai Speakers*: Possible areas of conflict." In Rottland F. and Omondi L. (ed),*Proceedings of the third Nilo-Saharan Linguistic Collaquim,*Kisumu,Kenya, August 1986, Helmet Verlag; Hamburg.

Bosire E. J. (1993). *Ekegusii: A Comparative study of Rogoro and Maate Dialect*, University of Nairobi

Campell, Z.M.. Qorro, M.A.S. (1997) *Language Crisis in Tanzania.* Mkuki na Nyota Publishers, Dar-es-salaam.

Corder S.P. (1978). "*The Significance of Learners' errors*" in Richards, J.C. (ed) , *Error Analysis; Perspectives on Second Language acquisition.*Longman, London.

Dulay, H.C. & Burt, M.K. (1974). "*Errors and strategies on child's second Language Learning*". In Tesol quarterly, Vol. 8 pp129-136.

Dulay H.C., Burt, M.K. & Krashen, S.D. (1982). *Language Two*. Oxford University Press, New York.

Ellis, R. (1985). *Understanding Language Two Acquisition* Oxford University Press,Oxford.

Etherton, A.R.B. (1977). "*Error Analysis Problems and Procedures*" In English Teaching journal vol. 32 No.1 pp 67-78

Fisiak, J. (1981). "*Some introductory notes concerning contrastive Linguistics.*" In Fiask J. (ed) *Contrastive Linguistics and the language Teacher* , Pergamon Press, London.

Fries, C.C. (1945). *Teaching and Learning English as a Foreign Language.* University of Michigan Press, Ann Arbor.

Halliday, M.A.K. et. al. (1964). *The Linguistic Sciences and Language Teaching.* Longman, London.

Idarus, A.S. (1983) "*Makosa yafanywayo mara kwa mara katika matumizi ya Kiswahili."* In *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*, TUKI, Dar-es-Salaam (Kur.174- 88)

James, C (1971). "*The exculpation of contrastive Linguistics*." In Nickel, G (ed) *Papers in contrastive Linguistics.* Cambridge University Press, Cambridge.

_____(1980) *Contrastive Analysis*; Longman, London.

Kapinga M.C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili sanifu,* University of Dar-es-salaam.

Kimemia J.N. (2001). *Kiswahili. The Dilemma of Developing the National Language*. Egerton University Press.

King'ei G.K. na Musau P.M. (2002). *Utata wa Kiswahili Sanifu*, Didaxis Nairobi.

Krashen, S.D. (1981). *Second Language Acquisition and Second Language Learning*, Pergamon Press, London.

Lado, R. (1957). *Linguistics Across Cultures*. University of Michigan Press Michigan.

Larsen-Freeman, D. and Long, M.H. (1994). *An introduction to Language Two Acquisition Research.* Longman, London.

Littlewood, W. (1984). *Foreign and Second Language Learning.* Cambridge University Press, Cambridge.

Polome E.C. (1967), Swahili Language Handbook, Center for Applied Linguistics, Washington D.C.

Republic of Kenya, Ministry of Education (1992 & 1998), *K.N.E.C's annual Reports*, Government Printer, Nairobi.

Selinger, H.W. & Shohamy, E.(1986). *Second Language Research Methods.* Oxford University Press, London.

Selinker, L. (1972). " Inter language" in IRAL Vol.10 pp.209-231.

Skinner, B.F.(1957*). Verbal Behaviour*. Appleton-Century Inc. New York

Sridhar S.N. (1981) "*Contrastive Analysis,Error Analysis and Inter Language*; Three phases in one goal." In Fisiak J. (ed), *Contrastive Linguistics and Language Teacher*. Pergamon Press,London

Van E.T. et. Al (1984). Applied Linguistics and the Learning and Teaching of Foreign languages. Edward Arnold. London.

Wanyoike, E.N. (1978)."*Vikwazo katika mafunzo ya Kiswahili Kenya.*" Katika LUGHA Vol. 5 No. 3 (Kur. 35-42.) Kenya Language Association, Nairobi.

Were, E.A. (1996*). First Language influence on Kiswahili composition writing*: The case of Babukusu students of Kanduyi, Bungoma. Unpublished M.A. Thesis, Kenyatta University.

Whiteley, W.H. (1974). *Language in Kenya*, Oxford University Press, Nairobi.

VIAMBATISHO

Kiambatisho (A)

Mwongozo wa utuzaji wa mtihani wa kitaifa wa Kiswahili kwa kidato cha nne.

Mwongozo wa kusahihisha insha umetolewa na Baraza La Mitihani ya Kitaifa nchini Kenya. Mwongozo huu umeorodhesha hatua muhimu za kuzingatiwa wakati wa kutuza insha za watahiniwa. Miongoni mwa mambo ya kuzingatiwa ni sarufi,msamiati na tahajia, mambo ambayo utafiti huu umeshughulikia. Mwongozo huu ulikusudiwa kutumiwa kusahihisha insha mbili (a) na (b) ambazo zilikuwa na tuzo 20 kila moja. Mtafiti aliziunganisha zote mbili na kuwa moja na kuwa na tuzo 40 ambazo ni tuzo jumla za insha ya Kiswahili.

Alama na tuzo za mtihani wa insha zilipangwa kama inavyoonyeshwa hapa chini.

Alama	**Tuzo**
A+	37 - 40
A	35 - 36
	31 - 34
B+	27 - 30
B	25 - 26
	21 - 24
C+	17 - 20
C	15 - 16
	11-14
D+	7 –1 0
D	5 - 6
	2 - 4

Usahihishaji

Usahihishaji kwa kila kitengo ulifanywa ifuatavyo:

	Kitengo	**tuzo**
a)	maudhui	12
b)	mtindo	5
c)	sarufi	10
d)	tahajia	8
e)	msamiati	5
	Jumla	**40**

Mtafiti alivizingatia vitengo vitatu (a), (b) na (c) ambavyo vilikuwa na jumla ya tuzo 23 kati ya tuzo zote 40.

Kiambatisho (B)


Majina ya shule zilizohusishwa kwenye utafiti

Shule zifuatazo za upili wilayani Kisii Kusini zilihusishwa wakati wa ukusanyaji wa data kwa njia ya mijadala na insha za wanafunzi

Shule ya upili ya mseto ya Nyabine.
Shule ya upili ya mseto ya Etago
Shule ya upili ya mseto ya Riagumo
Shule ya upili ya wavulana ya Nduru
Shule ya upili ya mseto ya Nyangweta
Shule ya upili ya mseto ya Eberege
Shule ya upili ya mseto ya Mokubo
Shule ya upili ya wavulana ya Riokindo
Shule ya upili ya wasichana ya Serikali, Sengera
Shule ya upili ya wasichana ya Sengera Parish
Shule ya wavulana ya Sameta
Shule ya upili ya mseto ya Sameta
Shule ya upili ya mseto ya Nyabite
Shule ya upili ya mseto ya Nyachogochogo
Shule ya upili ya wasichana ya St. Theresas, Nyangusu

KIAMBATISHO (c) i

INDEX NUMBER 711313010



Shule ya Upili ya Mtakatifu Charles
S.L.P 1504,
Kisii.
18.7.2002.

Kwa Rafiki yangu Alice,

Rafiki ~~yangu~~ Alice ningependa kuchukua fursa hii kukusalimu mahali ulipo huku nikiamini kwamba uko salama wa salimu.

Tangu ulipokwenda huko ngambo natujawahi kuonana ana kwa ana lakini sasa ningependa kukusuliza hali ya nyumbani ili nawewe ujue hali ya kweru inaendelea.

Ninafikiria ulipokwenda masomo yako. Ulituacha wengi wetu tukiwa salama, lakini vile ninaona sasa ukirudi kuroka hapo hutaweza kuamini mambo ambao yametukia. Rafiki yangu ninaelezea unajua ugonjwa wa ukimwi. Huu ugonjwa umeenea kisijini mwetu zaidi. Wengi wetu wameketa rono na wengine wako hatarini ningependa kukuomba ushirikiane zaidi ile tuweze kuyalinda masilai yako mwenyewe usiwe kama vijana wa hapa nyumbani ambao ndio imegunduliwa ya kwamba wengi wao ndio wako na ukimwi.

Vile ulajua huu ugonjwa hauna dawa, na vile wataalamu hawajapata hiyo dawa, Serikali imeamua kusema kwamba, yeyote atakayepatikana na virusi vya ukimwi, yaani mtu akichukuliwa hospitalini na kupatikana ana maradhi hayo, Madaktawa wanaweza kumdunga sindano ya kifo ili huu ugonjwa usienee kabisa

Serikali pia inaendelea kuwasaidia watu ambao hawajapata ugonjwa huo kwa kuwaelezea

Jinzi watakavyoishi ili wasije wakaambukizwa na maradhi hayo.

Pia shuleni wanafunzi wanaendelea kupimwa na Madakitari na kuchukua wangu hayo virusi manakamani kwa sababu wakiachwa huu ugonjwa utaendelea kuzambaratika zai vile dawa yake haijapatikana.

Rafiki yangu ni hayo tu ya huzuni yanaendelea kutendeka hata nyumbani na mengine tutaona mungu akitwaria tuwes-kuonana ana kwa ana.

Rafiki yako Divinnah.

3/4 (—2 Urefu)

MWIZI KUIBA MAHINDI YA SHULE

Ilikuwa ni siku ya Jumatatu wakati niliamka kwenda shuleni, lua nalikuwa limekuja kwa sababu ilikuwa ni wakati wa mapungulia ngoma nyuni wa angani walikuwa wakiimba nyimbo zao za kawaida. Nami nililoga chapuchapu na kuuchukua MKOPA wangu na kuhama skulini.

Njiani nilikuwa nikienda mwendo wa kukuru kakara huku nikiamini kwamba nitafika shuleni mapema kwa vile niliamka mapema.

Shule naikuwa mbali na kwetu, na tulikuwa tunanitasika kuamdhuria saa kumi mbili unusu. Punde si punde nikafika shule wanafunzi walikuwa wameshika nawakuwa wachache. Punde niri ~~tititi~~ tuliPOkuwa + kituo darasani, tukasikia sauti iKiPaswa mwizi! mwizi! mwizi! Tulipo angalia upande sauti ilikuwa natoka, Tukashituka ghaya ya kushituka kumwona mwanafunzi wa shule yetu akimpazia mwizi sauti aliyeku akiiba mahindi shambani.

Baada ya sekunde kuwa ~~d~~akika, tuka-mwona huyo mwizi akitoroka huku gule mwanafunzi ~~wan~~ mwenzetu akimfuata unyounyo. Wanenga hakukosea kunena kuwa "Siku za mwizi ni arobaini" wanafunzi wote walipunutika na kumkimbiza mwizi na baa ya muda mfupi mwizi akashikwa na wanafunzi. Kwa kweli, wanafunzi walim mia na kumfanyia maajabu kwa sababu hakuna mwalimu alikuwa amefika skuli mwizi alinyororokwa na kamasi huku

akiangalia kama mbwa anayetoka masini.

Kwa vile wengi wa wanafunzi nawaju uwari wa mtu, wao waliona ulikuwa ni mchezo tu! nawakuwa wanajua walikuwa wanamuumiza-lyata ingawa alikuwa anaiba mahindi ya shule.

Wakati sio wakati, mwalimu hedimasta akafika shuleni na kushitukia kisa. kilichokuw kinaendelea. mwalimu hakuona ribaya vile huyo mwizi alipigwa kwa sababu vitu vingi vilikuwa vikiibwa na havikuwa vinapatikana kama vitabu.

Shule yetu haikuwa mbali na kituo cha Polisi na ilikuwa karibu na barabara kuonbwa ambao magari yalikuwa yanapita. Punde si punde gari ya Polisi likaonekana likipita. Hapo mwalimu hakusita kupaaza sauti na kulizimamiza lile gari.

Baada ya kuongea na askari, na mwalimu akawaonyesha magunia mawili huyo mwizi alikuwa ameyajaza na kuwaambia askari wamchukue ili kezi yake isikilizwe baadaye. Mwisho, mwizi huyo alitiwa katika gari ya Polisi nasi wanafunzi tukasha ngilia kwa ushuaa wetu.

Udhaifu:

(Sarufi, hijai.)

KIAMBATISHO (c) ii

INDEX NO. 029

SWALI LA KWANZA.

Q	Jumla
04	10

School ya Studies

Jeremiah Macoki,
S.L.P 441,
Kisii.
19/07/2002.

Kwako Dandi,

Kwa hakika mwenzangu tangu nilipoanza nchini, Kinalo jambo na mambo ya kukuambia. Lakini kabla ya hayo yote Pokea salaamu zangu zizizo na kifani. Naam nikitalaji yu mzima nani hapa vile vile.

Tangu aliponiacha hatujawahi kusungumza kwa njia yoyote ile na hali hivi sasa ni kasibu mwaka mzima umepita. Hapa nchini kunao vitu vingi hutokea maisa kwa maisa. Je Maisha ngambo yako namna gani? Natalaji maisha yamekuwenbea vizuri na huwa italuchia siku ozuri maishani mwako. Hata hivyo ni kutia bidii katika kazi zetu tunayoyafanya.

Mwenzangu dunia hii iko na mambo si hapa. Kumbuka vile tuliyokuwa tunatembea watu walikuwa na mzeno ambao unaoona dunia ni chuma. Kwa hakika ni kweli. Hapa nchini kuna jambo ambalo linawasumbua Wanandii ni ni ugonjwa ulioya sana usiokuwa na tiba ambao unaaminika ni ugonjwa mbaya hasa kwa binadamu ugonjwa wa ukimwi. Sidani kama unayapata mapata habari za kile siku kwa mneathiri watu wengi hapa nchini kwetu 'kenya'.

Kwa hakika tangu nilipotoka hapa na kuanda ngambo ukimwi umewafanya watu wengi na watoto kuachwa mayatima kutokana na vifo. Kama unavyojua ukimwi hauna tiba. Mimi mwenzangu Nastanjabika kuona vijana wa siku hizi kama wasafiki wenzetu wulioona nao kufanya mapenzi kiholela. Singalipenda kuona vizuri kuingia katika maisha ya hatari, je sewe wewe?

Sasikali yetu inajaribu inavyo ili kuona kwamba huu ugonjwa wa ukimwi unapungua na hatimaye mambo mengi kama yafuatayo: Kwanza kapisa inafanya mipango ya kuagiza

madawa ya kutibu ili mtu asiwe anakaa hivyo bali anafanya kazi ndogo ndogo kusudi asaidiane na fikira nyingi. Pili Sesikali imefanya juhudi za kuagiza mipira ya kupuzy ili kuzuia mtu asipate viini ya ukimwi na ukiyatumia hivyo mipira Utubuje choonì an kuchomwa. Tena Sesikali inao mipango ya kuwazindua wananchi jinsi ya ugonjwa Watajikinga na huo ungonjwa. Ingali Mipango ya utandawazi hiko kila nilaya nchini. Jambo jingine ni kuwa Wajana wanaumbwa kuwa na safiki mmoja Sababu ni kuwa wengi wetu hatuwezi kuhumilia hali wakati wa kuoa. Je utawezaje kuvumilia hali upate jiko?. Mwanzangu ni vigumu kuwanya. Wakati Mwingine Sesikali inafanya mipango ya kuwapika Sitibu Katika vibindi ya Sudio na Sunjinga ili Watu wajichadhasi na ugonjwa huu. Sesikali inawaomba Wazazi kuwazindua Watoto wao jinsi watakavyodikinga na ugonjwa huu na kuwasaidi Wasifanye mapenzi ishidda. Na mwizo Sesikali imefanya mipango ya kujangiza pesa ambazo zinatumiwa kwa wale ambao wanoathirika na ugonjwa huo hili wawezo kuendamba wenzao kuwa ni ugonjwa mbaya kwa kutembea mahospitali mbalimbali nchi. Piw kanisani Sesikali imewapatia Masisi wa Maniisa mbalimbali vitabu ya kusoma hili kujikinga na ugonjwa huo.

Mwanzangu nadhani ni haya tu ningekujuzia kwa barua yangu. Kwa kweli ningependa uadi uniandikia barua kuniambia kuzijibu hali yako na jinsi unavyoendelea. Sina Mengi ya kukuambia. Ahsanteni.

Mimi Safikiyako
Jeremiah Makasi.

06/20

Udhaifu:
1) Hoja/mandhui
2) Sarufi.
3) Hijai

SWALI LA NNE

INDEX NO 029

SIKU ARUBAINI ZA MWIZI.

Itiri majizi tulivyokuwa katika bweni la Shule yetu, tukiwa tunajiandaa kuingia usingizi, tuliyetuswa na Mgowe kutoka bweni lingine. Mala tu wanafunzi wakaanza kutoka mmoja mmoja kuenda nje. Walikuwa wakizigamburua nyayo zao. Sikuwa na la kufanya basi sikuwa na hasaka kwa kutaka kuona hizo ilikuwa inaendelea basi hasaka hadaka haina bakaka.

Muda si mrefu nikasikia sauti kali kama ni ya Mgana. Salaale!! kwani nilichukua nguo zangu na kubifaa hala hala ili kuona ni nini kinachoendelea. Hakuna hata anayetambua mwenzake Sababu kulikuwa na giza totoro. Ama kwa kweli usiku huo ule kulikuwa na kasidi kama bakafu. Taa za Shule zilikuwa zimewaka kama mwangaza. Wanafunzi walikuwa wanaenda hadi palipotokea mgowe. Nilipofika kasibu walikuwa mamejaa sisisi huko hakukuwa na nafasi ya kupiteu hata kufenga kamasi. Lakini kwa akili yangu kwani akili ni nywele nilijaribu kusukuma ule umati wa wanafunzi ili kuona nini kilikuwa huko. Hawkeni

Jamani kulikuwa kumejaa nabsanketi ya wanafunzi na yalikuwa yamegegemagwa nje ya bweni. Kumbe binadamu kama hapa. Kutazama vizuri mwanafunzi mmoja alikaliwa kando huko damu inojaa pale nche lakini aliuawa hana wasiwasi wowote. Papo hapo kilancha wa Shule aliuliwa aendi hadi nyumba ya nairobi ule mwalimu mkuu ili azipate jini ya jambo hilo. Mala baada ya muda mrup! kijana kasimama twa! na kutimua mbio huko wanafunzi kumpata. Shoot huko nikiwa mojawapo ya wale waliompata. Mgowe yalijaa kwani lakini ni kuwa kulikuwa na wanafunzi ambao walikuwa wakimbiaji kuthiki ya Swaba, Senze yeye?

Mwanafunzi huyo alipoona ngozi zinamwisia jamani akagenka tena kuwasambulia wanafunzi wezake. Kumbe watu ni Shetani. Jiwe alilojikuwa hata kuwezi kutuburtu kusimama lakini ni kama kwamba kumkamua simba baali akiwa

KIAMBATISHO (C) iii

7111010335

1	2	3	4	5
11	-	-	12	23

S. L. P. 2168,
KISII.
16/7/2002

Kwa mpendwa hiko,

Hinafuraha kupata barasi hii ya kukuandi kia barua huko nikiahani u mzima kwa makariwa ya mwenyezi Mungu. Mimi ni mzima ila tu kazi ngingi zilizoko hapa afya shuleni kwa matayarisho ya mtihani wa mwaka.

Mbona umekyamaza kwa muda hivyo! Mara ngingi nimewasiliana na wakazi wako ngumbani kuwauliza hali yako kwa sababu simu yetu hapa ngumbani iliharibika kwa sababu ya ukosefu wa pesa ndio maana hapa ya kunya kingi ambacho kimezidi.

Sababu kubwa ya kukuandikia barua hii ni kukujulisha juu ya nchi yetu kenya ambayo sasa hivi haistahili kuitwa nji yetu. Na kama nawezha kukuuliza hapo wa Agombo ugonjwa wa ukimwi umefika huko! Na kama umefika ni watu kama wangapi hivyi wanakufa kwa siku?

Ni mshangao mkuu kwamba marafiki wetu wote kina Jane numy James Kirancha, Lane-l Asiego walikufa kutokana na ugonjwa huu wa ukimwi, Bila kumsahau Mwalimu wetu mkuu wa shule ya msingi. Huu ugonjwa ulale ulaka sio wototo sio wazee sio vivara hata maofisaa wakubwa.

Serikari yetu imeanzisha vifaa mbali mbali ili kujaribu kupambana na ugonjwa huu. Vifaa hivyo ni kama, ni lazima na ilkimu la kila mkazi kupanga uzazi ili kuzuia watoto wanaweza kutunza visuri na kuelimisha kwani elimu ndio maisha ya maisha ni kutokana na elimu ambapo watu huiua kuji kinga na ugonjwa wa ukimwi

Hi kweli waswahili walinena kwamba mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

Juma alikuwa mwana wa pekee wa Mary na James. Hawakubarikiwa kupata mtoto mwingine, kwa sababu ya kazi yao nzuri na mshahara mnono, walimlea Juma kama mwana wa watu. Juma alipotaka hiki alipewa, alipoulizia kile alicholetewa na kadhalika.

Juma alipotimiza umri wa miaka kumi na tano hivi tabia yake ilianza kupotosha, alisitakiwa mara kwa mara kwa wazazi wake ambao walimtetea na kusema kwamba watu walikuwa na wivu juu ya mtoto wao wa pekee.

Hi ukweli walidhani mtoto akilelewa wembe mpe Juma alizidi na tabia yake kwa sababu ya kichwa alichopewa na wazazi wake kwa bahati mbaya babake Juma alikata roho kwa ajali ya barabara.

Mary alipojaribia haja muili ulimtegulia, mambo yaka mkwama kuoni, na vimurimuri kumpita machoni. Hakuona maisha mbeleni, kwa sababu ya mapenzi alijokuwa naye kwenda kwa James. Lakini kwa sababu kuu ni tuzima na kuishi ni bahati waliendelea na maisha yao ya kawaida.

Baada ya majuma mawili hivi Juma alisitakiwa kama mmoja wa wezi waliobia ngombe ya watu kijijini, na kuuza kwa soko ya mbali. Kukamatikwa na kuchukuliwa mahakamani ambapo wazazi wao walilipishwa pesa nyingi sana.

Mary alijaribu kumkanya mwanaye lakini Juma hakuona dafu aliendelea zaidi, akutupilia shule mbali na kuwa jizi kuu katika mtaa huo. Hata ngombe alisikiwa na kuchapwa vibaya zaidi, Mara ngapi aliwekwa gerezani na kutolewa na mamake kwa kulipa pesa. Hata akafikiwa kiwango cha kupenda gerezani kuliko nyumbani, Na kuzoea mateso na viboko vya humo gerezani.

Huko nyumbani mmoja alivikuwa, akawalaumu, mabaabu akamukuumu babake Juma Zaidi kwa kumtunza mtoto wa tabia mbaya kama wanavyo walinena maji yakimwagwa hayazoleki na mwanito huja baada ya mkaja.

Ilikuwa siku ya Juma na tulikuwa katika mkutano wetu wa kawaida shuleni wa maombi wakati wa alasiri tulipo sikia makelele za watu, "Mwizi!! Mwizi Mwizi!! Mwizi!" tusaidie kumshika, hukuu kutoka nyuma kulikuwa na ghasi gari la askari likimfuata mbio na A walikuwa ndani.

Mwalimu mkuu alituashauri tuwape mkono kumshika mwizi huyo kwani umoja ni nguvu na utengano ni uchaitullikimbika mwendo wa ngamia na kila mmoja kuingia up wake baada ya dakika isiriini hivi tulisiki Vilimbi ikilia kwamba amekamatwa na wananchi alib bega kwa bega kuelekea kuliko sirikali mishwa gari, kish Askari mmoja alituambia kwamba Juma alikuwa mmoj wa wezi mbao wanatibwa wakiishikwa wakiiba katika banki kuu ya kenya na hapo akakaribia kutoroka. Mu atiporatiza mwizi huyo alituwa katika gari ya polisi nasi wanachuzi tukashangilia kwa ushujaa wetu.

12

Ubaya
Sarufi
Hijai

KIAMBATISHO (C) iv

INDEX NO: 711612006

1

1 3 5
04 07 11 pk 9

RIAGUMO MIXED SEC SCHOOL,
P.O. BOX 70,
NYAMARAMBE.
18/1/2002.

Kwa rafiki Juma,

-Nimashikiri na kuamini kabika jina la mungu kuwa uko salama salimini na familia yako ya pia, Hapa nimi pia niko vyema bali cu nimashukuru kwa barakati za mitihani wa kitaifa wa kidato cha nne mwako huu.

Kwa kaikika mpenzi, unepotea kwa (mda) mrefu bila ya kujuliana kali ituijo karo na kapa nyumbani. Hapa nchini mwetu kuna vita vingi vya (fifo) kutokana na (kusaka) kwa ugunduzi wa utimwi ambao ni kateri sana vile ujuavyo na kauna dawa. Mamia ya (wakinchi) (wakuza) kila siku na watu wengi wamekaki (wachane) na pia watoto wengi kuwa (chokoraa) wa (mitaani) kapa kenya.

Watu (wengi) (wengi) wameanza kusema kuwa ukimwi ni uchawi na kwa vile ukimwi kaipo wao wameanza kusanya mapenzi kiholela kstela bila ya kangaliba wakisema eti "Ngoma itulizwe ipasavyo". Wengine wamezidi na ulevi ambapo wao wunapoamka kuingia kwenye vilabu vya (bombe) wengine kwenye baa na mwishowe wao kuishia na ngoma za kimapenzi. Watu wengine ambao ni matajiri wenye pesa wameanzisha watoto wa Shule kwa sababu ya pesa na wanawapeleka kwenye (vijindio) ambapo wanakata nyama na machoma pamoja "Nyama choma" na mwishowe wanaingia kwenye baa wanalevya halafu ngoma itulizwe.

Wanainchi wengi wamekimbilia (kondomu) wakidhani zitawakinga kutokana na ukimwi lakini wapi wao kuishia kingilijua wakati ugonjwa umeingia mwilini ndipo wanaanza kuyemba nyuma wao ili awaokoe

lakini mungu na ana waangalia na kusema siokoe.

Kwa vile visa vimezidi, serikali yetu kama Kenya mashanga jitikuda ngumu ili kupunguza visa ukimwi. Jusi jusi raisi wa Kenya alikuwa akituma mkutano kuhusu ukimwi na walijadili jinsi wanavyoweza kusaidia kuenea kwa janga hili ambalo limeikumba dunia nzima.

Wasiri wa afya alisema kuwa, serikali imeanza kuweka ambayo inashughulikia ukimwi na pia kuanzisha vikundi vinavyo sungoka kote nchini ili kuwaelimisha wakenya jinsi ya kujikinga kudokana na ukimwi na pia kuwaonyesha vile ukimwi inaambukizwa kusoka kwa mtu mmoja kati mwingine kwa njia ya vidio. Pia imeweka vipindi vingine kwenye redio ambayo kuwaelimisha wanainchi jinsi ya kujikadhari na ukimwi kama vile "wakati ni sasa, ughikwapo shikamana".

Serikali pia Inaziza mipira ya kusuia mandhi yanayoambiza kudokana na mapenzi kama kondomu ambazo wizimewasaidia wananchi sana kukinga janga ili la ukimwi.

Serikali imeanza msako mkali ili ya wanao-consenza janga na vingwaji vingine ambayo ni uya kulevya na pia kuacha ya kulevya kama vile mariguana.

Mpenzi, hapa Kenya tu na mabadiliko mengi sana ya kijamii, labda uko uingereza mambo ni mazuri kuliko hapa kwetu lakini, nyumbani ni nyumani, jaribu Sikuu moja ututembelee usone vile hali imezorotoka.

Ni nyimi wako mpendwa,
Obura Evans,
Shanghitoma.

Udhaifu
- hati chafu
- tahajia

7/6/2006

3

Mpiga ngumi kuuza mkonowe.

Habo kale palikuwa na kijana mmoja kwa jina mboma. Yeye alikuwa mtoto wa mzee mmoja katika kijiji cha Chanda na mamake alikuwa mwalimu aliyekuwa akifunza shule ya msingi Hiokuwa karibu na nyumbani mwake.

Kijana huyo alikuwa akienda shuleni kama kawaida na mamake alikuwa akimpenda sana kwa wazazi wake walivyo wa kuwa vile alikuwa akikuwangwa alama karibu zote katika kila mtihani aliokuwa akifunza. Kwa mia mmoja, akiwa katika shule ya msingi alikuwa mpole, mwenye nidhamu, mwenye moyo mwema na pia alikuwa na heshima kwa walimu, wazazi na pia kwa wanafunzi wenzake. Alifanya mitihani wa darasa la nane na kufaulu kujiunga na shule ya upili ambapo wazazi wake walifurahi sana.

Akiwa katika shule ya upili ya mkoa, mtoto huyo alianza kuchelewa tabia na akawa kinyume na tabia zile alizokuwa nacho awali, yeye alijiunga na vijana wenzine ambao walikuwa na tabia za kunywa pombe shuleni na pia wezi wa vitabu, nguo za wanafunzi wenzao na kuziuza ili wapate pesa za pombe.

Mama ya mtoto huyo alikuwa akijisikia na kujipiga kifua akisema kuwa naye ana shujaa wa kategemewa sikio sijuo bila yeye kujua eti mtoto ameku-wa chachandu anayechelea makaa.

Mtoto huyo alipokuwa na harakati zake za uchumbazi kama kawaida yake, alimwibia mtoto mmoja godoro na vitambaa vya kulalia. Mtoto huyo alipopiga ripoti kwa walimu, godoro hilo lilianza kutafutwa na kwa bahati mbaya, lilipatikana kwa huyo kijana. Papo hapo, mwalimu mkuu wa shule hiyo alimfukuza kutoka shuleni.

Shuka za kulala si vitanda

Mamake alipoingia shuleni kumwona mtoto
wake, aliambiwa kuwa kijana wako alifukuswa
shule wiki mbili zilizopita kutokana ~~na~~ kizi na pia ~~utovu~~
ulevi. Mama huyo alikasirika kasha kosa akiscma kuwa
Mtoto wake hanezi a kufanya hivyo kwani tangu
utoto wa mwanawe hayo ~~hawezi~~ hayajawai kutokea
Na huyo mama hakujua kuwa alikuwa akipigania
mtoto wake ambaye ni muwizi kupita (kiasi) pia aka sahau
methali isemao "mpiga ngumi ukuta huumiza mkono we."

~~walimu~~
-tahejia

CHA I

KIAMBATISHO (C) v

INDEX. 711201/016

4.

1	4	J
14	12	26

SHULE YA UPILI AA NYAMAGWA
S. L. P. 3023,
KISII.

TAREHE MBILI, JULAI, 2002.

Kwa rafiki mpendwa,

Ningependa kuchukua fursa hii ili kukuarifu mengi kuhusu mambo mbalimbali hapa nchini huku nikitaraji kuwa maisha kwako hapo ni mazuri. Kwangu mimi, maisha sio mazuri sana kwa vile tunaendelea kukumbwa na visa kadha wa kadha kutokana na ugonjwa hatari wa ukimwi unaoangamiza wengi.

Ukiwa hapo, ningetumaini kukupatia habari kuhusu jitihada zinazofanywa na Serikali yetu ili kupunguza vifo hivi. Kwanza kabisa, Serikali imepata kutoa elimu kuhusu uambukizo zaidi na dalili ya kuepuka na viini vya ugonjwa huu kupitia kwa redio na vitabu mbalimbali. Hii ni kutokana na watu kutoelewa ugonjwa huu vizuri.

Serikali imeonya pia wale ambao wanafanya mapenzi yasiyo halali kama vile mapenzi kabla ya ndoa na mapenzi yanayotokana na kutoaminika kwa watu wawili au zaidi ambao wameoana ndoa. Hii ni kwa sababu huenda kati ka kuambukiza magonjwa baina ya watu wazima.

Kulingana na hayo, Serikali imetengeneza miche mbalimbali ambapo wale watu ambao wameguduliwa kuwa na ugonjwa huu, hupelekwa na kutunzwa hadi kufa kwao. Hii ni kwa sababu wakiendelea kuishi na watu wengine bila shaka wataendelea kuambukiza huo ugonjwa.

Vifaa vya kupima viini vya huu ugonjwa wa ukimwi vimetengenezwa na Serikali. Inahitaji watu kupimwa damu yao kabla ya kufanya ndoa. Na bei ya hii kazi ya kupima damu ni ya chini sana ili kuwezesha hata wale maskini bila wapate kupimwa.

Hii ni kwa sababu imeonekana kuwa idadi ya watu kufa kutokana na ndoa ya watu ambao wako na ugonjwa huu wakati wa ndoa.

Kwa kumalizia, Serikali imeomba mizaada ya vifaa vya kutumia wakati wa kufanya mapenzi kwa wale watu wasiojiamini kama vile mibira ya "Kondom". Pia wameitaka maelezo chinsi vile mtu anavyo-hitajika kutumia. Sisi tunaendelea kuomba kama nchi kwa jumla ili mola aendelee kutulinda na kutuongoza. Pia nategemea kupata barua kutoka kwako ukiniarifu juu ya hali huko ngambo.

Wako mwaminifu,

~~Udhaifu~~
- Sarufi
- Lugha
- Lugha ya mama
- ~~Ufupi wa insha~~ - 2

16 - 2 = 14

B

(14)

KILICHO NA MWANZO, KINA MWISHO. ✓

Katika mwaka uliopita tulipata kukumbwa na matatizo kadha wa kadha kama sisi wanafunzi. Haya yalitokana na masingizio ambayo hayakuwa mazuri sana sana baina ya wanafunzi wenzetu. Mara kulitokea wizi wa viatu katika mabweni, na pia wizi wa vitabu katika madarasani.

Tulijaribu kuvumilia haya yote kwa vile hata ukitangaza, hakuna aliyekuwa tayari kutoa ushirikiano wowote kuhusu wizi. Ulifika wakati mmoja ambapo mwalimu mkuu alituita pamoja na kutuarifu juu ya mbinu ambazo zingetuwezesha kupata hawa watu waliousika.

Basi alituambia kwamba lazima kiranja wa kila darasa achakachishe wakati ambapo kila mwanafunzi ametoka kwenda labda masaleni au kwa sababu fulani. Pia walo watalipuliwa kusimamia mabweni mbalimbali wachakachishe ni nani aliyebaki ndani wakati wengine wametoka.

Baada ya hayo hatukupata shida yoyote kwa wakati mrefu sana. Lakini ilipofika kati ya muhula wa tatu, sanduku la ya mwanafunzi mmoja ilipotea ikiambatanwa na nguo za shule zilizoanikwa nje ya bweni. Bidhaa hizi zilipotea wakati wa usiku ambapo kila mtu alihitajika kuwa darasani.

Sasa hili lilikuwa ni jukumu letu kama wanafunzi kufanya jitihada katika utafiti ili tuweze kupata hivi vitu. Bila shaka tulianzia walo ambao mizigo yao ilikuwa inaonekana kuwa sio mizuri vile. Kulikuwa na wanafunzi wanne katika kidato cha pili, mmoja katika kidato cha tatu na wawili katika kidato cha nne.

au thibitisha ✓

Basi hatungekuwa na budi kuanzia kidato cha pili, Tulipowaita majina, (ilitimilika) wazi kuwa wote walikuwepo darasani usiku huo. (Bila) kufika kidato cha tatu, na gyge alikuwa darasani. Katika kidato cha nne tulipata kwamba wanafunzi kumi walikuwa darasani ila tu; mmoja ambaye alitoweka kutoka darasani wakati wa usiku.

Tulipompatia wakati wa kujitetea, alishindwa na papo hapo wanafunzi wakaanza kumpiga huku wakipiga magoti. Mwalimu mkuu hangeweza kusaidia ila tu kupiga simu katika polisi iliyokuwa karibu. Muda si muda askari waliwasili shuleni, na wanafunzi kuona hivyo wakaacha kumpiga na kutoroka mbali. Mwisho, mwizi huyo alitiwa garini ya polisi nasi wanafunzi tukashangilia kwa ushujaa wetu.

Udhaifu
- lugha ya mama
- hijeri
- uf pi we isila -2

14 - 2 = 12

(12) B-

EGE VE ...RARSKY
...VE